# Nipashe

Jumatatu Agosti 5, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579988

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



ST.JOSEPH UNIVERSITY In Tanzania

"WHERE YOUR DREAMS ARE NURTURED"

Calling all Old Students of SJCET, SJCIT, SJCMC, SJCHS and SJUIT-ARUSHA

SJUIT invites its Alumnus for the Alumni meet from 4:00PM-9:00PM on 24th August, 2019, "Entrance is free". For details www.alumni.sjuit.ac.tz


For more information contact: +255 676 504 147 +255 745 281 505




## Taboa yafunguka kizuizi cha Polisi mabasi saa 24

UKURASA 2

# Walimu wamwomba JPM kuumaliza mgogoro wao



UKURASA 3

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### CUF WAOMBA TAMKO MIKUTANO YA HADHARA

CHAMA cha Wananchi (CUF), kimemwomba Rais John Magufuli, kutoa tamko la kuruhusu vyama vya siasa nchini...

UKURASA WA 4

### LUKUVI AAGIZA UCHUNGUZI MIPAKA MSIMBAZI CENTER

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ameiagiza Idara ya Ardhi Manispaa ya Ilala...

UKURASA WA 4

### WCF KUANZISHA MFUMO KUDAI FIDIA KWA MTANDAO

MFUKO wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), uko mbioni kuanzisha mfumo wa waajiri na wafanyakazi kuwasilisha...

## Sababu za ndege kuua zaelezwa

UKURASA 2



Watumishi wa afya wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kagera, wakifanya mazoezi ya namna ya kuvaa vifaa kinga kwa ajili ya kumhudumia mgonjwa anayehisiwa kuwa na maambukizi ya ugonjwa wa ebola. **PICHA: UBRAHIM HAMIDU**

## Kishindo SADC kuanza leo

UKURASA 2


MICHEZO SIMBA YAAHIDI MAAJABU YA MWAKA KESHO UK.31

MAONI, KATUNI UK.6



Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola (kushoto), akiteta jambo na Kamanda wa Polisi mkoani Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Hamisi Issah, baada ya kumaliza mkutano wa kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili waendesha bodaboda na Bajaj mkoani hapo, ulioandaliwa na Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM). Kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Usalama Barabarani mkoani hapo, Zauda Mohammed. **PICHA: JAMES LANKA**

# Kishindo cha SADC kuanza Dar leo

**Na Beatrice Moses**

KISHINDO cha maandalizi ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali za Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kinaanza leo, wakati Rais John Magufuli, atakapofungua maonyesho ya Awamu ya Nne ya Wiki ya Viwanda ya Jumuiya hiyo.

Maonyesho hayo ni hatua ya utangulizi wa Mkutano wa 39 wa Wakuu wa nchi 16 za SADC watakaoambatana na viongozi na maofisa waandamizi wa nchi zao.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kuhusu maonyesho hayo, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya, alisema serikali imejipanga vizuri kutumia fursa hiyo ya kuwa mwenyeji wa mkutano huo.

Maonyesho hayo yanafanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam.

Alisema yatafungwa na Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein Agosti 8, mwaka huu.

Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ni 'Mazingira Wezeshi ya Biashara kwa Maendeleo Jumuishi na Endelevu ya Viwanda na kuongeza biashara na ajira katika ukanda wa SADC'.

"Mwitikio ni mkubwa hadi sasa wamejindikisha washiriki 2,026 kati yao 1,766 ni Watanzania, washiriki waonyeshaji ni 938, bado wanaendelea kujisajili," Manyanya alisema.

Naibu Waziri huyo alibainisha kuwa maonyesho hayo yanafanyika pia katika viwanja vya Karemjee na Gymkhana, na yanawakutanisha wazalishaji na wadau mbalimbali wa bidhaa za viwandani na wafanyabiashara kutoka nchi 16 za SADC.

"Pamoja na kuonyesha bidhaa mbalimbali, pia kutafanyika midahalo na majadiliano ikiongozwa na wabobezi wa kibiashara," Manyanya alisema.

Alisema miongoni mwa mambo yatakayojadiliwa ni sekta ya dawa na vifaa tiba, nishati na madini.

Alisema Maonyesho ya Wiki ya Viwanda ya SADC ni hatua mojawapo ya kuonyesha kwa vitendo utekelezaji wa Mkakati wa Viwanda wa SADC (2015- 2063).

Agosti 9, mwaka huu, wageni watatembelea baadhi ya viwanda na maeneo mbalimbali ya biashara yaliyopo Tanzania Bara na Zanzibar.

Wageni hao watapata nafasi ya kujifunza zaidi kuhusu juhudi zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi nchini za ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika

INAENDELEA UK.8

# Taboa yafunguka kizuizi cha Polisi usafiri saa 24

**Na Salome Kitomari**

CHAMA cha Wamiliki wa Mabasi nchini (Taboa), kimeliomba Jeshi la Polisi kuharakisha taratibu za kuhakikisha ulinzi na usalama kwenye maeneo yenye wasiwasi ili mabasi yaruhusiwe kusafiri kwa saa 24.

Julai 7, mwaka huu, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, aliagiza mabasi yaruhusiwe kusafirisha abiria kwa saa 24 nchini, lakini Agosti 2, Jeshi la Polisi lilitangaza kusitisha huduma hiyo kwa baadhi ya mikoa mpaka hapo litakapojiridhisha na hali ya usalama.

Akizungumza jana na Nipashe kwa njia ya simu, Katibu Mkuu wa Taboa, Enea Mrutu, alisema wamepokea uamuzi wa Jeshi la Polisi kwa sura mbili.

Alisema sura ya kwanza ni furaha kwa kuwa wanakwenda kujipanga namna ya kukabiliana na majambazi wanaoteka magari na kupora abiria kwenye maeneo yanayoonekana siyo salama.

Vile vile, alisema kwa upande mwingine wamepokea kwa shingo upande kwa kuwa wanakwenda kupunguza mapato na kuongeza matumizi ya magari na abiria kwa ujumla. "Tunaliomba Jeshi la Polisi lijipange vizuri angalau kwa mwezi mmoja wakamilishe masuala yote muhimu waturuhusu tuendelee kusafirisha abiria hadi usiku," alisema na kuongeza:

"Awali safari hizi zilipigwa marufuku kutokana na ajali iliyotokea nyakati za usiku mkoani Dodoma na chanzo kuwa ni mwendokasi, lakini siyo suala la usalama kama walivyoliteta, sawa, hatupingi ila tunawaomba waharakishe ili turuhusiwe kusafirisha muda wote."

Kwa mujibu wa Mrutu, iwapo watasafirisha muda wote itasaidia kupunguza idadi ya magari ambayo tajiri atayasafirisha kwa wiki kutoka manne hadi mawili, huku gharama za uendeshaji ambazo zilisababishwa na magari kulala njiani zitapungua.

Alisema pia wasafiri watakuwa na uhakika wa kusafiri siku hiyo hiyo na kufika kwa kuondokana na gharama za kulala njiani na muda unaopotea.

"Mabadiliko haya hatujayapokea kwa raha kwa kuwa tulisharuhusiwa na kuanza kufurahia kutoa huduma hii, tunawaomba baada ya kukamilisha masuala ya usalama waruhusu magari kusafirisha," alisisitiza.

Baada ya Waziri Lugola kutangaza kuruhusu wasafirishaji kusafirisha abiria saa 24, waliieleza Nipashe kuwa wamefurahishwa na uamuzi huo kwa kuwa ilikuwa ni kilio chao cha muda mrefu na kwamba kero iliyobaki ni idadi kubwa ya maeneo ya ukaguzi na vituo vya mabasi vya halmashauri ambavyo wanaingia kwa ajili ya kulipa ushuru.

Agosti 2, mwaka huu, Jeshi la Polisi lilitangaza mikoa ambayo huduma ya usafiri saa 24 haitakuwapo kuwa ni Dar- Kahama- Kigoma, Dar-Tabora-Katavi, Kahama-Geita-Kagera, Kahama kwenda mikoa mingine iliyopo mpakani na Dar-Tabora kwenda wilaya zake.

Kamishna wa Operesheni na Mafunzo kutoka Makao Mkuu ya Polisi, Liberatus Sabas, alisema wamefikia uamuzi huo kutokana na changamoto mbalimbali na kutoa muda wa kujipanga.

Alisema njia zitakazoruhusiwa iwapo mabasi yatafika usiku ni Morogoro, Shinyanga na Kahama na kwamba mabasi kutoka Kanda ya Ziwa yalikuwa yanalala Morogoro na kutoka Dar es Salaam, yanalala Shinganya.

## Sababu za ndege kuua zaelezwa

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), imeeleza chanzo cha ajali ya ndege iliyotokea mkoani Tabora na kuua watu wawili, kuwa ni kufeli kwa injini wakati wakiwa angani.

Ajali hiyo ilitokea katika Kijiji cha Mahompa, Kata ya Igigwa, wilayani Sikonge, na kuhusisha ndege yenye namba za usajili ZU-TAF aina ya Sling Aircraft yenye uwezo wa kubeba abiria wanne ikiwa na uwezo wa kilogramu 900.

Katika ajali hiyo wakurugenzi wawili wa mradi wa U Dream Global, Des Werner (58) (aliyekuwa rubani wakati wa ajali) na Werner Froneman (36), walifariki papo hapo kwa kuungua moto.

Ndege hiyo ilikuwa ikitokea Entebbe, Uganda kwenda Malawi kupitia Tanzania.

Kwa mujibu wa taarifa kwenye mtandao wa kampuni hiyo, U Dream Global ni programu inayofadhiliwa na Megan Werner ambaye ni mtoto wa Des Werner, kwa lengo la kuwezesha na kuhamasisha ubunifu kwa vijana wadogo kwenye usafiri wa anga.

Akizungumza juzi Mkurugenzi Mkuu wa TCAA, Hamza Johari, alisema ndege hiyo iliyokuwa na watu wawili walipofika Tabora waliomba kibali cha kutua kwa dharura kutokana na hitilafu iliyojitokeza.

"Waliomba kibali cha kukatiza anga letu tukawapa walipofika karibia uwanja wa ndege wa Tabora wakahisi kuna tatizo wakaomba kutua kwa dharura, wakashuka wakashughulikia ndege yao wakaomba kuondoka wakaondoka," alisema.

Alisema dakika tano baada ya kutoka uwanjani hapo waliomba tena kibali cha kuteremka baada ya kuona hitilafu kwenye injini, lakini hawakujulikana waliko hadi zilipopatikana taarifa za kuungua kwa ndege hiyo. "Walivyopanda juu dakika tano wakaripoti tena kwenye mnara wetu wa kuongozea ndege kwamba wanahisi kuna hitilafu kwenye injini wanaomba watue tena, tuliwaruhusu, lakini hatukuwasikia tena," alisema Johari.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, timu ya wataalamu itakwenda eneo la tukio kwa ajili ya kufanya uchunguzi na baadaye taarifa kamili itatolewa.

INAENDELEA UK.8

## HABARI KITAIFA

# CUF waomba tamko mikutano ya hadhara

**Na Mary Geofrey**

CHAMA cha Wananchi (CUF), kimemwomba Rais John Magufuli, kutoa tamko la kuruhusu vyama vya siasa nchini kufanya mikutano ya hadhara kwa ajili ya kujiandaa na chaguzi wa serikali za mitaa. Wito huo unatolewa ikiwa ni siku moja tangu, Jeshi la Polisi Wilaya ya Kipolisi Buguruni, kuzuia mkutano wa hadhara wa CUF, uliokuwa ufanyike katika kata ya Vingunguti kwa lengo la kuhimiza wananchi kujitokeza kujiandikisha kwenye daftari la kudumu la wapigakura na kupiga kura katika uchaguzi wa viongozi wa serikali za mitaa, utakaofanyika Oktoba mwaka huu.

Akizungumza na wanahabari jijini Dar es Salaam, Naibu Mkurugenzi wa Sheria na Haki za Binadamu wa CUF, Salvatory Magafu, alisema Rais Magufuli alipiga marufuku ya kufanyika kwa mikutano ya hadhara na kuahidi kuruhusu muda wa uchaguzi ukifika.

"Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ni muhimu kwa nchi hii hivyo ni muda mwafaka wa kuruhusu mikutano ya hadhara kuanza kufanyika muda huu wa kuandikisha wapigakura," Magafu alisema.

Alisema Rais Magufuli alipiga marufuku mikutano ya hadhara isipokuwa wabunge, madiwani au kiongozi wa mtaa kwenye eneo lake la utawala katika majimbo, kata au mitaa, vijiji na vitongoji. "Ndugu wanahabari pamoja na tamko hili kukiuka katiba ya nchi ya mwaka 1977 ambayo imekuwa ikifanyiwa marekebisho ya mara kwa mara, pia ni kinyume cha sheria nyingine za nchi hii na matamko ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika ambayo sisi kama nchi wanachama tumesaini na kuridhia, tunamsihi Rais Magufuli kuruhusu wakati huu tuanze kufanya mikutano ya kisiasa," Magafu alisema.

Alifafanua zaidi kuwa katika siku za hivi karibuni baadhi ya viongozi wa serikali, walinukuliwa wakidai hawana taarifa juu ya vyama vya siasa kuzuiwa kufanya mikutano ya hadhara.

Alisema Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Jaji Francis Mutungi, alidai kutopokea barua kutoka chama chochote cha siasa kulalamikia chama chake kufanya mikutano. Magafu alisema kutokana na kauli hiyo, CUF kiliandika barua ya kuomba kufanya mkutano wa hadhara ambao hata hivyo ulizuiliwa.

"Agosti 2, tulipokea barua ya zuio la kutofanyika kwa mkutano kutoka Ofisi ya Mkuu wa Polisi wilayani Buguruni yenye na kumb: BUG/SO.7/2/A/VOL./191 kwa madai kuwa kuna zuio la serikali kufanya mikutano ya hadhara. Utaona wazi kuwa maelezo ya zuio hilo yanapingana na kile ofisi ya msajili imekitamka hivi karibu," Magafu alisisitiza.

# Walimu wamwomba JPM kuumaliza mgogoro wao

**Na Mary Geofrey**

CHAMA cha Kutetea Haki na Maslahi ya Walimu Tanzania (Chakamwata), kimemwomba Rais John Magufuli kuingilia kati msuguano ulipo wa kukipiga vita chama hicho, kilichoanzishwa kwa lengo la kuwakomboa walimu kiuchumi nchini. Ombi hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Mratibu wa Chakamwata Mkoa wa Dar es Salaam, Emmanuel Patrick, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu zuio walilopewa na Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri la kufanya mkutano wao mkuu wa dharura uliokuwa ufanyike jana wa kuchagua viongozi wa bodi ya udhamini.

Alidai mkutano huo ulizuiliwa na Ofisi ya Msajili kwa madai ya kutokuwa na bodi ya wadhamini kwa ajili ya kusimamia chama hicho, kwa mujibu wa katiba yao Ibara 5(1) na Ibara ya 25-30 ilhali mkutano huo ulikuwa na lengo hilo.

"Tunamwomba mwalimu mwenzetu, Rais Magufuli aturuhusu tukutane naye, tumweleze namna watu ambao wana dhamana ya kusimamia walimu wanavyotaka kukwamisha juhudi zake, kwa sababu kumekuwa na mipango ya makusudi ya kutaka kukiua chama hiki chenye malengo ya kukomboa walimu wa nchi hii kwa maslahi ya taifa," Patrick alisema. Alidai kuwa sababu za kupigwa vita hiyo hadi kuzuiliwa kufanya mkutano huo uliokuwa unashirikisha wajumbe 200 kutoka mikoa yote nchini ni wanachama wengi wa Chama cha Walimu (CWT) kukihama chama hicho na kujiunga na Chakamwata, ambacho kimejikita kutetea maslahi ya walimu na siyo kuwanyonya. Alidai chama hicho kimekuwa kikikata asilimia moja ya mshahara wa mwalimu fedha ambayo mwalimu anapostaafu hurudishiwa asilimia 50 ya ada alizolipa wakati wa utumishi wake.

"CWT wao wanakata asilimia mbili ya mshahara wa mwalimu na anapostaafu hawana wanachowalipa na ikitokea akakoma uanachama, hawezi kurudishiwa fedha yoyote wakati Ukamwata mwanachana anarejeshewa nusu ya fedha alizochangia kwenye mfuko huo pindi tu atakapojiondoa na ndio sababu wamekuwa wakitupiga vita," alisema.

Alidai chama hicho kilichoanzishwa mwaka 2015 kina wanachama 12,000 nchi nzima na kati ya hao, 9,000 ni walimu wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Naye Mwenyekiti wa Chakamwata taifa, Japhet Joseph, alisema chama hicho kimesajiliwa na kinatambulika kisheria hivyo, aliisihi serikali kuingilia kati mgogoro uliopo ili chama hicho kiendelee kutimiza wajibu wake kisheria.

Alidai kuwa, CWT ambacho kilianzishwa mwaka 1993 kilifanya usajili wa bodi ya wadhamini mwaka 2015 na kwa kipindi chote hicho walifanya kazi chini ya viongozi waliokuwa madarakani hivyo hawaoni sababu ya wao kuonekana wamekiuka sheria katika kipindi kifupi.

Kuhusu barua waliyoandikiwa na kusainiwa na Kaimu Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri, Pendo Berege, ilieleza kuwa Msajili hakitambui chama hicho kutokana na kukosa uhalali wa kuendesha chama bila kuwa na bodi ya wadhamini kama ambavyo katiba inaelekeza.


LSG Sky Chefs

## PUBLIC AUCTION

| S/N | NAME OF ASSET | TYPE | REF# | Quantity |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Vegetable Spinner | | ICSL01 | 1 |
| 2 | Bread Package machine | | ICSL02 | 1 |
| 3 | VEHICLE (Mercedes - Benz) | High Loader | Lsg 07 | 1 |
| 4 | VEHICLES (Mercedes-Benz) | High Loader | Lsg 04 | 1 |
| 5 | VEHICLE (VW CADDY) | Volkswagen) | Lsg 11 | 1 |
| 6 | Micro wave | | ICSL03 | 1 |
| 7 | Electrical Hotplate Cooker | | ICSL04 | 1 |
| 8 | Electrical Burn Marine | | ICSL05 | 1 |
| 9 | Gas Stove 6 burner | | ICSL06 | 1 |
| 10 | Deep Frier | | ICSL07 | 1 |
| 11 | Flat Top Griller | | ICSL08 | 1 |
| 12 | Titin Pan Gas | | ICSL09 | 1 |
| 13 | Bread Rolls Machine | | ICSL10 | 1 |
| 14 | Tv Flat Sceen 32 inch (SONNY) | | ICSL11 | 1 |

**The Auction forms are available for collection at LSG SKY CHEFS office located at Julius Nyerere International Airport – Cargo Terminal and can be collected from Monday the 5th to Friday the 10th of August 2019.**
**The Auction will be held on Tuesday the 14th of August at 10:00AM.**

**For more Details Call:**
**Phone: +2552 2284 3541, Mobile: 0655 563 231/0756 563 231**
**Mail:petro.linganda@lsg.co.tz**

215359702



Sky Works® Consultancy

Bibi Titi Mohammed Road
The Uhuru Heights,
Mezzanine Floor, M5
P.O. Box 77534, Dar Es Salaam,
United Republic of Tanzania

**TENDER FOR TRANSPORTING PETROLEUM PRODUCTS – TRANSIT ONLY**

**GENERAL INTRODUCTON**

1. **SkyWorks Consultancy Ltd.** is engaged in consultation for Supply and Logistic of All Petroleum Product in East, South and central Africa, located in Dar es Salaam. This inquiry is being issued on behalf of our client, a leading Logistics company registered in Tanzania hereinafter referred to as COMPANY, that intends to execute the Work of logistic ("WORK") in accordance with the terms and conditions of this Tender.
2. Now **SkyWorks Consultancy Ltd.** invites sealed tender from Sole Proprietorships / Partnerships / Companies (hereinafter called APPLICANT) from all over Tanzania to submit tender document as per below criteria.
3. The scale of this project is to transport over 12 Million Liters of fuel to begin with, starting September 2019.

**GENERAL REQUIREMENT**

1. The Invitation for Bids is open to all Transport / Logistics Companies.
2. A firm shall submit only one Tender, in the same tendering process, either individually as a tenderer or as a partner in a joint venture. No firm can be a subcontractor while submitting a tender individually or as a partner of a joint venture in the same tendering process.
3. The tenderer shall bear all costs associated with the preparation and submission of its tender, regardless of the conduct or outcome of the tendering process.
4. Certified Company certificates (TIN, VRN, Certificate of incorporation, Business License, Sumatra Certificate, Valid W&MA Calibration certificate, TRA Certificate).
5. Copies of its audited financial statements for the past two fiscal years.
6. List of major supply contracts conducted within the last two years.
7. Company has to be licensed by the regulatory authority in the country for transporting petroleum products.
8. Details for service and maintenance garage.
9. All trucks should have tracking system to be monitored all the time during trip, which needs to be linked to the "Company" tracking system.
10. Tender securing declaration in any format.
11. Health, Safety and Environment (HSE) Policy.
12. Good in Transport (GIT) insurance Policy.
13. Copy of TRANSIT permit (C65 or equivalent).
14. Company has to be able to DELIVER products in THESE SIX destination countries (ZAMBIA, DRC (LUBUMBASHI), MALAWI, RWANDA, BURUNDI and UGANDA.
15. Duly filled in Tender signed by authorized person and submitted either by Email or physically on below address.

**DEADLINE** : **Tuesday 13th August 2019**
**ADDRESS** : **Plot number 63/27, Bibi Titi Mohammed Road, The Uhuru Heights, Mezzanine floor, M5, P.O. Box 77534, Dar Es Salaam, United Republic of Tanzania**
**EMAIL** : **info@skyworks.co.tz, skyworkstz@gmail.com**

**NOTE;** Only shortlisted will be contacted and INVITED to discuss Cost, volume to be carried and other Commitment procedures. The COMPANY reserves the right to accept / reject any tender at their sole discretion.

A BKS Company

115358902

# Wakulima waitwa kujiunga na NSSF

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Omar Mgumba, amewaomba wakulima nchini kujiunga na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) kwa kuwa ni wadau wakubwa kwenye sekta ya isiyo rasmi.

Amesema kwa mujibu wa mabadiliko ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2018, Shirika limepewa mamlaka ya kuandikisha watu walio kwenye sekta binafsi na isiyo rasmi wakiwamo wakulima, hivyo ni budi kutumia fursa hiyo kujiandikisha.

Mgumba aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, katika Maonyesho ya Wakulima (Nanenane), yanayoendelea katika viwanja vya Nyakabindi, Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu.

"Ukizungumza sekta binafsi na isiyokuwa rasmi, idadi kubwa ya wadau wake ni wakulima wa nchi hii na hasa wale wadogo wadogo," alisema.

Alisema wakulima na wananchi wengine watakaojiunga na NSSF watanufaika na huduma mbalimbali ikiwamo mafao ya uzeeni, uzazi, huduma ya afya na mikopo.

Mgumba ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini, alisema kwa sasa wakulima wamepata sehemu salama ya kupata

INAENDELEA UK. 8

# Lukuvi aagiza uchunguzi mipaka Msimbazi Center

**Na Munir Shemweta**

WAZIRI wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ameiagiza Idara ya Ardhi Manispaa ya Ilala kufufua upya mipaka ya eneo la Msimbazi Center, jijini Dar es Salaam ambalo linamilikiwa na Kanisa Katoliki kwa ajili ya kutatua mgogoro kati ya kanisa hilo na mmiliki wa kituo cha mafuta cha Victoria.

Lukuvi alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipokutana na pande zote mbili, Kanisa Katoliki na mmiliki wa kituo cha mafuta cha Victoria, Harold Matemba, pamoja na muuzaji wa eneo la Victoria.

Uamuzi wa kukutana na pande hizo mbili unafuatia Waziri Lukuvi kutembelea eneo hilo Jumatano iliyopita akiwa katika ziara yake ya kushughulikia migogoro ya ardhi na matapeli wa ardhi nchini.

Alisema, kumbukumbu za wizara yake zinaonyesha eneo hilo ni sehemu ya eneo lilitolewa kwa Msimbazi Mission mwaka 1980 na lina hati inayomilikiwa na Kanisa Katoliki, huku mmiliki wa kituo cha mafuta cha Victoria akidai kuuziwa eneo hilo na mmiliki wa awali ambaye naye aliuziwa mwaka 2002 na Oscar Mweyeya.

Imedaiwa mmiliki huyo

INAENDELEA UK. 8




Mkurugenzi Mkuu wa Songas, Nigel Whittaker, akikabidhi medali na kombe kwa Faudhia Juma Said na Zaina Yassin washindi wa kitengo cha Biolojia kutoka Shule ya Sekondari ya Mtwara Girls, wakati wa maadhimisho ya mashindano ya Sayansi yajulikanayo kama Young Scientist Tanzania, yaliyofanyika katika ukumbi wa JNICC, jijini Dar es Salaam. Songas imekuwa moja kati ya wadhamini wa mashindano hayo kwa muda wa miaka minane katika juhudi za kuunga mkono serikali kuboresha sekta ya elimu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# WCF kuanzisha mfumo wa kudai fidia kwa mtandao

**Na Mwandishi Wetu,** SIMIYU

MFUKO wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), uko mbioni kuanzisha mfumo wa waajiri na wafanyakazi kuwasilisha madai ya fidia kwa njia ya mtandao.

Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Mfuko huo, Anselim Peter, alisema hayo jana kwenye maonyesho ya Nanenane yanayofanyika kitaifa kwenye viwanja vya Nyakabindi nje kidogo ya mji wa Bariadi, mkoani Simiyu.

Peter alisema lengo la kuanzisha mfumo huo ni kusogeza karibu huduma za mfuko kwa wateja na wadau wake na hivyo kurahisisha upatikanaji wa huduma.

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi unashiriki katika maonesho ya Nanenane kwa lengo la kupata fursa ya kuwaelimisha waajiri na wafanyakazi kuhusu shughuli za mfuko ambazo ni kulipa fidia, utaratibu wa kufuata ili kuwasilisha madai kabla ya kulipwa fidia.

"Pia katika banda la WCF hapa Nyakabindi, wataalamu wetu watatoa elimu kuhusu mfuko, kusajiliwa, kuwafahamisha taratibu za michango, taratibu za madai ya fidia na pia kupokea maoni ya wadau kuhusu mfuko. Lakini pia tunatoa huduma kwa vitendo jinsi wanavyoweza kufanya kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya wafanyakazi wake kwenye orodha iliyoko WCF, kuprinti cheti, na pia kulipa michango ofisini kwako," alifafanua Peter.

Wakati huo huo, Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, aliupongeza mfuko huo kutokana na ushiriki wake katika mpango wa mkoa kujenga kiwanda cha kutengeneza vifaa tiba. Alisema huo ni utekelezaji kwa vitendo azma ya serikali ya awamu ya tano katika kuanzisha na kuimarisha viwanda ambavyo vitaipeleka nchi katika uchumi wa kati.

"Nishukuru na kutambua mchango mkubwa wa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, Masha Mshomba na WCF kwa ujumla kwa sababu ni partner (mshirika) mkubwa kwenye mipango yetu ya ujenzi wa kiwanda cha vifaa tiba," alisema Mtaka.

Alisema uongozi wa mkoa walishirikiana na WCF katika hatua mbalimbali za kushirikiana katika ujenzi wa kiwanda hicho, na kwamba hivi sasa wizara iko katika nafasi nzuri ya kutangaza zabuni ili kumpata mkandarasi atakayejenga kiwanda hicho.

"Kwetu sisi kama mkoa WCF imetoa ushirikiano mkubwa katika mipango yetu ya kushiriki katika uchumi wa viwanda wametoa ushirikiano mkubwa," alisema.




TANGAZO

# KILIMANJARO CO-OPERATIVE BANK LIMITED

## AUDITED FINANCIAL STATEMENTS

**ISSUED PURSUANT TO REGULATIONS 7 AND 8 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS, 2014**

### STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 31ST DECEMBER 2018
(Amounts in shillings)

| | | Current Year 31st Dec 2018 | Previous year 31st Dec 2017 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **ASSETS** | | |
| 1 | Cash | 8,057 | 25,944 |
| 2 | Balances with Bank of Tanzania | 431,181 | 2,228,205 |
| 3 | Investments in Government securities | - | - |
| 4 | Balances with other banks and financial institutions | 1,979,765 | 590,379 |
| 5 | Cheques and items for clearing | (107,289) | 80,568 |
| 6 | Inter branch float iterms | - | - |
| 7 | Bills negotiated | - | - |
| 8 | Customers' liabilities for acceptances | - | - |
| 9 | Interbank Loans Receivables | - | - |
| 10 | Investments in other securities | - | - |
| 11 | Loans, advances and overdrafts (net of allowances for probable losses) | 377,305 | 3,438,777 |
| 12 | Other assets | 129,152 | 920,257 |
| 13 | Equity Investments | - | - |
| 14 | Underwriting accounts | - | - |
| 15 | Property, Plant and Equipment | 1,229,188 | 1,292,676 |
| **16** | **TOTAL ASSETS** | **4,047,358** | **8,576,806** |
| **B.** | **LIABILITIES** | | |
| 17 | Deposits from other banks and financial institutions | - | - |
| 18 | Customer deposits | 5,139,155 | 9,843,521 |
| 19 | Cash letters of credit | - | - |
| 20 | Special deposits | 338,053 | 338,055 |
| 21 | Payment orders/transfers payable | - | - |
| 22 | Bankers' cheques and drafts issued | 40,772 | 14,784 |
| 23 | Accrued taxes and expenses payable | 19,060 | 127,702 |
| 24 | Acceptances outstanding | - | - |
| 25 | Interbranch float items | - | - |
| 26 | Unearned income and other deferred charges | - | - |
| 27 | Other liabilities | 180,478 | 24,448 |
| 28 | Borrowings | - | - |
| 29 | **TOTAL LIABILITIES** | **5,717,518** | **10,348,510** |
| 30 | **NET ASSETS/(LIABILITIES)(16 minus 29)** | **(1,670,160)** | **(1,771,704)** |
| **C.** | **SHAREHOLDERS' FUNDS** | | |
| 31 | Paid up share capital | 7,363,802 | 1,512,496 |
| 32 | Capital reserves | 453,542 | 453,542 |
| 33 | Retained earnings | (6,873,651) | (3,888,172) |
| 34 | Profit (Loss) account | (2,623,756) | 29,813 |
| 35 | Other capital accounts | 9,903 | 120,617 |
| 36 | Minority Interest | - | - |
| 37 | **TOTAL SHAREHOLDERS' FUNDS** | **(1,670,160)** | **(1,771,704)** |
| 38 | Contingent liabilities | - | - |
| 39 | Non performing loans & advances | 1,615,762 | 790,779 |
| 40 | Allowances for probable losses | 1,272,968 | 99,361 |
| 41 | Gross Loans and advances | 1,716,357 | 3,594,118 |
| 42 | Other non performing assets | 66,083 | 35,009 |
| **D.** | **SELECTED FINANCIAL CONDITION INDICATORS** | | |
| (i) | Shareholders Funds to total assets | -41.27% | -20.66% |
| (ii) | Non performing loans to total gross loans | 94.14% | 22.00% |
| (iii) | Gross loans and advances to total deposits | 31.34% | 35.30% |
| (iv) | Loans and advances to total assets | 9.32% | 40.09% |
| (v) | Earning assets to Total Assets | 32.26% | 41.43% |
| (vi) | Deposits Growth | -47.79% | 21.41% |
| (vii) | Assets growth | -52.81% | 27.82% |

### STATEMENT OF COMPREHENSIVE INCOME FOR THE YEAR ENDED 31ST DECEMBER 2018
(Amounts in shillings)

| | | Current Year 31st Dec 2018 | Previous Year 31st Dec 2017 |
|---|---|---|---|
| 1 | Interest Income | 295,320 | 492,097 |
| 2 | Interest Expense | 243,212 | 437,488 |
| 3 | Net Interest Income ( 1 minus 2) | **52,108** | **54,609** |
| 4 | Bad Debts Written -Off | - | - |
| 5 | Impairment Losses on :Loans and Advances | 1,198,260 | 39,579 |
| **6** | **Non Interest Income:** | **78,743** | **1,671,367** |
| | 6.1 Foreign Currency Dealings and Translation Gains/ (Loss) | - | - |
| | 6.2 Fees and Commissions | 74,335 | 100,359 |
| | 6.3 Dividend Income | - | - |
| | 6.4 Other Operating Income | 4,408 | 1,571,008 |
| **7** | **Non Interest Expenses:** | **1,556,347** | **1,656,584** |
| | 7.1 Salaries and Benefits | 590,830 | 478,834 |
| | 7.2 Fees and Commission | 58,753 | 69,110 |
| | 7.3 Other Operating Expenses | 906,764 | 1,108,640 |
| **8** | **Operating Income/ (Loss)** | **(2,623,756)** | **29,813** |
| **9** | **Income Tax Provision** | **0** | **0** |
| **10** | **Net Income / (Loss) After Income Tax** | **(2,623,756)** | **29,813** |
| **11** | **Other Comprehensive Income (itemize)** | | |
| **12** | **Total Comprehensive Income/(loss) for the year** | | |
| 13 | Number of Employees | 32 | 32 |
| 14 | Basic Earnings Per Share | 0 | 0 |
| 15 | Number of Branches | 1 | 1 |
| **SELECTED PERFORMANCE INDICATORS** | | | |
| (i) | Return on Average Total Assets | 0.39% | 0.39% |
| (ii) | Return on Average Shareholders' Fund | -1.65% | -1.65% |
| (iii) | Non Interest Expense to Gross Income | 736.40% | 78.40% |
| (iv) | Net Interest Income to Average Earning Assets | 2.73% | 1.70% |

### STATEMENT OF CASH FLOWS FOR THE YEAR ENDED 31ST DECEMBER 2018
(Amounts in shillings)

| | | Current year 31st Dec 2018 | Previous year 31st Dec 2017 |
|---|---|---|---|
| I: | **Cash flow from operating activities:** | | |
| | Net income (Loss) | (2,623,756) | 29,813 |
| | **Adjustments for:** | | - |
| | - Impairment/Amortization | 10,838 | 7,225 |
| | - Prior Year Adjustment | (40,686) | (28,937) |
| | - Depreciation | 63,489 | 53,819 |
| | - Net change in Loans and Advances | 3,061,472 | (454,932) |
| | - Gain/loss on Sale of Assets | - | - |
| | - Net change in Deposits | (4,704,366) | 1,714,471 |
| | - Net change in Short Term Negotiable Securities | | |
| | - Net change in Other Liabilities | 47,388 | 73,299 |
| | - Net change in Other Assets | 710,240 | (84,786) |
| | - Tax Paid | | - |
| | - Others (specify) | | 1,059 |
| | - Due to other banks | 25,988 | |
| | ***Net cash provided (used) by operating activities*** | **(3,449,393)** | **1,311,031** |
| II: | **Cash flow from investing activities:** | | |
| | Dividend Received | - | - |
| | Purcharse of Fixed Assets | - | (35,969) |
| | Proceeds from Sale of Fixed Assets | - | - |
| | Purchase of Non-Dealing Securities | - | - |
| | Proceeds from Sale of Non-Dealing Securities | - | - |
| | Others (Adjustment on Property Plant and Equipment) | - | - |
| | ***Net cash provided (used) by investing activities*** | **-** | **(35,969)** |
| III: | **Cash flow from financing activities:** | | |
| | Repayment of Long-term Debt | - | - |
| | Proceeds from Issuance of Long Term Debt | - | - |
| | Proceeds from Issuance of Share Capital | 5,851,306 | 77,150 |
| | Payment of Cash Dividends | - | - |
| | Net Change in Other Borrowings | - | - |
| | Others (specify) | (3,015,291) | (898,615) |
| | ***Net Cash Provided (used) by Financing Activities*** | **2,836,015** | **(821,465)** |
| IV: | **Cash and Cash Equivalents:** | | |
| | **Net Increase/ (Decrease) in Cash and Cash Equivalents** | **(613,378)** | **453,597** |
| | **Cash and Cash Equivalents at the Beginning of the Quarter/Year** | **2,925,096** | **2,471,499** |
| | **Cash and Cash Equivalents at the end of the Quarter/Year** | **2,311,718** | **2,925,096** |

### STATEMENT OF CHANGES IN EQUITY AS AT 31/12/2018
(Amount in thousands shillings)

| Current Year | Share Capital | Share Premium | Retained Earnings | Regulatory Reserve | General Provinsion Reserve | Others | Total |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Balance as at 1st January, 2017** | **1,435,346** | **-** | **(3,771,725)** | **5,045** | **28,060** | **453,543** | **-1,849,731** |
| Profit for the year | - | - | 29,813 | - | - | - | 29,813 |
| Other Comprehensive Income | - | - | - | - | - | - | - |
| Transactions with owners | 77,150 | - | - | - | - | - | 77,150 |
| Dividends Paid | - | - | - | - | - | - | - |
| Regulatory Reserve | - | - | | 87,976 | - | - | 87,976 |
| General Provision Reserve | - | - | | - | (466) | - | (466) |
| Others | - | - | (116,447) | - | - | - | (116,447) |
| **Balance as at 31st December, 2017** | **1,512,496** | **-** | **(3,858,359)** | **93,021** | **27,594** | **453,543** | **(1,771,705)** |
| | | | | | | | |
| **Balance as at 1st January, 2018** | **1,512,496** | **-** | **(3,858,359)** | **93,021** | **27,594** | **453,543** | **(1,771,705)** |
| Profit for the year | - | - | (2,623,757) | - | - | - | (2,623,757) |
| Other Comprehensive Income | - | - | - | - | - | - | - |
| Transactions with owners | 5,851,306 | - | (3,015,292) | - | - | - | 2,836,014 |
| Dividends Paid | - | - | - | - | - | - | - |
| Regulatory Reserve | - | - | | (83,925) | - | - | (83,925) |
| General Provision Reserve | - | - | | - | (26,788) | - | (26,788) |
| Others | - | - | | - | - | - | - |
| **Balance as at 31st December, 2018** | **7,363,802** | **-** | **(9,497,408)** | **9,096** | **806** | **453,543** | **(1,670,160)** |

The above extracts are from the financial statements of the Bank for the year ended 31st December,2018 which have been prepared in accordance with International Financial Reporting Standards (IFRS).The financial statements were audited by MUHASIBU CONSULTANTS and received a qualified report.The financial statements were approved by the Board of Directors on 27th July, 2019 and signed on their behalf by:

| Name | Signature | Date |
|---|---|---|
| 1. Dr G Machimu, CHAIRMAN, BOARD OF DIRECTORS | .......................... | 05th August 2019 |
| 2. Ms A.A. Mshana ,VICE CHAIR PERSON BOARD OF DIRECTORS | .......................... | 05th August 2019 |

215359602

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF, klabu tupieni jicho mabadiliko ya kanuni

**ZIBAKI** siku 18 kabla ya msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara kuanza rasmi, ligi hiyo ikitarajiwa kushirikisha timu 20 kama ilivyokuwa msimu uliomalizika wa 2018/19.

Kuelekea msimu huo mpya kwa sasa timu zipo katika maandalizi makubwa zikicheza mechi kadhaa za kirafiki kujaribu vikosi vyao kabla ya mtanange huo kuanza rasmi Agosti 23, mwaka huu.

Maandalizi hayo kwa timu pekee, bali pia tumeshuhudia Shirikisho la Soka nchini (TFF), kwa kushirikiana na kamati yake ya waamuzi na Chama cha Waamuzi nchini, likiendesha semina kwa waamuzi pamoja na mazoezi ya utimamu kimwili.

Lengo la semina hiyo ikiwa ni kuwafanya waamuzi kuwa fiti kimwili lakini pia kuelewa mabadiliko muhimu yaliyojifanyika katika sheria mbalimbali za mchezo huo.

Hilo ni jambo la msingi ambalo pia linatakiwa kuambukizwa kwa klabu na TFF haina budi kuwakumbusha wanachama wake ambao ni klabu kutoa darasa kwa wachezaji, viongozi na hata mabenchi yao ya ufundi.

Hadi sasa ni Klabu ya Simba pekee ambayo tulishuhudia ikitoa darasa hilo la mabadiliko ya kanuni mbalimbali za soka kwa wachezaji wake kabla ya kuelekea kambini Afrika Kusini.

Kutokana na malalamiko mengi yaliyoelekezwa kwa waamuzi msimu uliopita, Nipashe tunaona ipo haja kubwa kwa kila klabu kualika wataalamu wa soka ili kutoa darasa hilo la mabadiliko ya kanuni hizo.

Tunaamini waamuzi pekee kupewa darasa hilo haitasaidia kuondoa malalamiko kwa kuwa bado wachezaji watakuwa wakiamini wameonewa pindi wanapoadhibiwa kulingana na mabadiliko hayo ya kanuni kutokana na kutozifahamu. Tayari TFF kupitia Chama cha Waamuzi nchini imeshakamilisha wajibu wake kwa waamuzi watakaochezesha Ligi Kuu na Ligi Daraja la Kwanza, hivyo ni wakati wa klabu sasa kutoa darasa kwa wachezaji wao na mabenchi yao ya ufundi kabla ya ligi kuanza.

Nipashe kama wadau wa soka hatutaki kabisa kuona malalamiko ya msimu uliopita kwa waamuzi yakijirudia tena msimu huu mpya.

Lakini wasiwasi wetu ni kwamba msimu huu kuna uwezekano mkubwa waamuzi wakabebeshwa lawama zisizowahusu kutokana na wachezaji, makocha, viongozi wa klabu na hata mashabiki kutofahamu mabadiliko hayo.

Hivyo kuna haja kubwa kwa TFF kuzisisitiza klabu kuona haja ya kutoa darasa kwa wachezaji wao ili kuepuka lawama zinazoweza kuelekezwa kwa waamuzi kutokana na uelewa mdogo wa mabadiliko ya kanuni zilizofanyiwa marekebisho.

Lakini pia sote tunafahamu kama si kushuhudia baadhi ya wachambuzi wa soka na wanahabari kupitia vyombo vyao vya habari (si Nipashe) kutokana na uelewa wao mdogo wa kanuni, wakiongeza mihemko kwa mashabiki wa soka, hivyo waamuzi kuonekana wamevurunda na kuadhibiwa.

Kwa mantiki hiyo, TFF haina budi kutazama upande huu wa pili kwa kuwaandalia semina wanahabari kabla ya ligi kuanza na kuweza kukumbushana baadhi ya kanuni zilizofanyiwa marekebisho jambo litakalosaidia kufikisha ujumbe/habari sahihi kwa mashabiki.

Lengo letu ni kuona malalamiko yakipungua kama si kuisha kabisa na hatimaye kupatikana bingwa halali ambaye ataiwakilisha vema nchi kwenye michuano ya kimataifa na hilo litawezekana tu kwa TFF kulimulika hili pamoja na kutatua changamoto mbalimbali zilizojitokeza msimu uliopita.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Timu zijipange Ligi Kuu, itakuwa ngumu mno

**KILA** timu kwa sasa imejichimbia kambini kujiandaa na Ligi Kuu Tanzania Bara inayotarajiwa kuanza Agosti 23, mwaka huu.

Makocha wapo kwenye hekaheka za kuwaweka fiti wachezaji pamoja na kuwapa ufundi ili ligi ikianza waanze kukifanya kile ambacho waliwaagiza.

Ni kipindi kinachohitaji utulivu na umakini wa hali ya juu, kwani mara nyingi tunaona ligi ikianza makocha wanakuwa na ama na vipindi vifupi, au hawana kabisa muda wa kuwafundisha tena wachezaji hao, zaidi ya kurekebisha tu makosa madogo madogo kutokana na ratiba kubana.

Kinachotakiwa sasa kwa makocha na wachezaji, huu ndiyo wakati wa kujiandaa kwa usahihi na ukamilifu kwani inavyoelekea msimu huu ligi itakuwa ngumu zaidi kuliko hata ya msimu uliopita.

Tuliona Ligi Kuu msimu uliopita ilivyokuwa ngumu, Simba, Yanga na Azam zilivyokuwa zikikimbizana kuusaka ubingwa. Ilipofika katikati, tuliona Azam pumzi ikianza kukata, Yanga ikizidi kupepea kileleni.

Lakini Simba ilipotoka kwenye mechi za kimataifa iliingia na gia mpya, na wakati huo Yanga nayo ilionekana kuishiwa pumzi na kuwafanya Wekundu wa Msimbazi kutwaa ubingwa.

Hata hivyo, timu zote tatu za juu zimepata nafasi ya kuiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya kimataifa, huku KMC, bila kujijua, ikifanikiwa kupata 'zari', la kucheza Kombe la Shirikisho baada ya kukamata nafasi ya nne. Nafasi hizi zilitangazwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf) wakati ligi imeshamalizika.

Na hii ilitokana na uwakilishi mzuri wa Simba kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa kiasi cha kufika robo fainali. Nina uhakika, kama Caf ingeitangazia mapema TFF kuwa nafasi tatu za uwakilishi wa michuano ya kimataifa zimeongezeka, ligi ingeweza kuwa ngumu zaidi ya ilivyokuwa.

**Hata hivyo, timu zote tatu za juu zimepata nafasi ya kuiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya kimataifa, huku KMC, bila kujijua, ikifanikiwa kupata 'zari', la kucheza Kombe la Shirikisho baada ya kukamata nafasi ya nne. Nafasi hizi zilitangazwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf) wakati ligi imeshamalizika.**

Kwa sasa timu zote 20 zinajua kuwa kuna nafasi tatu za moja kwa moja za kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa. Kutokana na hali hiyo, hakuna timu itakayokubali kupoteza mechi kirahisi kama ambavyo tulikuwa tukishuhudia huko nyuma, baadhi ya timu zikishaona nafasi za juu kuna timu ambazo zina pointi nyingi ambazo haziwezi kufikia, basi zinaamua kufa moyo na kupoteza kirahisi.

Timu zitakuwa zikipambana kutafuta nafasi ya kwanza, pili ya tatu mpaka ya nne, maana lolote linaweza kutokea.

Kwa maana hiyo hata timu iliyokuwa chini, nayo itakuwa ikipambana ipate hata nafasi ya nne, kwa sababu moja inaweza kutokea kama ilivyotokea kwa Azam, timu ya tatu kutwaa Kombe la FA na kupata nafasi ya moja kwa moja kuiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho, hivyo anayeshika nafasi ya nne akaikwaa kiulaini kama ilivyokuwa kwa KMC.

Nafasi kutoka moja tu ya bingwa kuwakilisha nchi, hadi tatu, mpaka nne zitaifanya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2019/20 kuwa ngumu na isiyotabirika kwa sababu kila timu sasa itataka kuwa ndani ya nafasi hizo.

Kinachotakiwa sasa timu zote ni kufanya maandalizi kabambe, na kila timu ikitegemea upinzani mkali kutoka kwa nyingine na hatutarajii kuona malalamiko yasiyo ya msingi wala mashiko.

Ni timu zilizojipanga vema kwa maandalizi ndizo zitakazofanya vizuri kama waamuzi watakuwa wakichezesha kwa haki.

HABARI KITAIFA




Meneja Mwandamizi wa Kitengo cha Hazina Benki ya TPB, Wenceslaus Fungamtama, akikabidhi msaada wa matangi mawili yenye ujazo wa lita 5,000 kwa Diwani wa Kata ya Bitale, John Bwami, kwa ajili ya Shule ya Msingi Bitale Maalumu, mwishoni mwa wiki Manispaa ya Kigoma. **MPIGAPICHA WETU**

# Wito kwa wakulima kujifunza teknolojia mpya

**Na Mwandishi Wetu**

WAKULIMA nchini wametakiwa kutumia Maonyesho ya Wakulima Nanenane kwa kujifunza teknolojia mpya pamoja na kujifunza mbinu bora za kilimo cha kisasa.

Hayo yameelezwa jana mkoani Morogoro na Mkurugenzi wa Sera, Utetezi na Ushawishi wa Baraza la Kilimo Tanzania, Timothy Mmbaga, katika mahojiano maalum wakati wa Maonyesho ya Wakulima katika viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, na kusema teknolojia za kilimo, uvuvi, ufugaji zote zinapatikana katika maonyesho hayo.

Kuhusu changamoto ya masoko ya mazao ya wakulima, alisema baraza limekuwa likifanya kazi kubwa hasa kupitia programu yake ya ubia wa kilimo Tanzania kwa kuwaunganisha wakulima na masoko.

"Sisi kama baraza tunasema tatizo letu kubwa haliko kwenye bei ya mazao, kinachotakiwa kufanyika ni kuongeza juhudi kwenye ubora lazima mazao yetu yawe bora zaidi, lakini pia lazima tuongeze uzalishaji, wakulima lazima wahamasishwe kutumia pembejeo za uhakika kwenye kilimo ili kupata mazao mengi, hivyo ni muhimu sana wakulima kuzingatia mbegu bora katika uzalishaji," alisema.

Kuhusu wakulima kuanza kulima kilimo cha kibiashara ili kuendana na mazingira yaliyopo, alisema: "Tukiamua kufanya kilimo biashara sisi kama baraza tunaamini hii nchi itazalisha chakula kingi sana, Tanzania pekee ina uwezo wa kulisha nchi zote zinazotuzunguka... tunaamini wakulima wapo na wawekezaji wapo, tatizo kubwa hapa ni hizi sera zetu hatujaziweka vizuri, wakulima watakuwa na uwanda mpana zaidi wa kuzalisha na kuuza bidhaa zao bila kuingiliwa na mtu au taasisi yoyote."

Ofisa shughuli wa Programu ya Ubia wa Kilimo Tanzania katika baraza hilo, Suzan Masagasi, alisema ili kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi ni muhimu kwa wakulima kuanza kutumia teknolojia mpya na za kisasa hasa katika kilimo cha mpunga na mahindi.

"Tumekwisha kufundisha wakulima wote wa Kanda ya Kaskazini hasa katika maeneo yenye ukame ili waweze kutumia teknolojia ya kilimo hifadhi kwa mazao ya mahindi, teknolojia hii inamsaidia mkulima kuvuna licha ya uwapo wa uhaba wa mvua," alisema.

Mkulima wa mpunga kutoka Kijiji cha Mkindo Kata ya Mkindo wilayani Mvomero mkoani Morogoro, Mwanaid Hamza, alisema tangu aanze kutumia teknolojia ya kilimo shadidi, ameanza kuona matokeo chanya kupitia kilimo kwani kwa sasa ana uhakika wa kutumia mbegu kidogo na kupata mazao mengi.

"Kabla ya teknolojia hii nilikuwa natumia kilo 25 hadi 26 za mbegu ya mpunga na mavuno yake yalikuwa madogo sana ili kuwa kwa ajili ya chakula, lakini tangu nianze kutumia kilimo shadidi nimefaidika sana," alisema na kuendelea:

Mwenyekiti wa wauzaji wa pembejeo wilayani Kilombero mkoani Morogoro, John Mvunjapori, alisema licha ya juhudi zinazofanywa ili kumsaidia mkulima, lakini bado mkulima wa Tanzania anakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa pembejeo za uhakika na kwa wakati.

# NBC yaiahidi ushirikiano serikali

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), imesema itaendelea kushirikiana kikamilifu na serikali ya awamu ya tano katika azma yake ya kuwaletea wananchi wake uchumi wa kweli na maendeleo.

Akizungumza wakati wa kongamano la wadau juu ya upatikanaji wa fedha na usimamizi wa hatari zinazoweza kujitokeza katika miamala ya kifedha mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa Idara ya Hazina na Masoko wa NBC, Peter Nalitolela, alisema NBC imejizatiti kushirikiana na serikali na taasisi zake kuhakikisha nchi inafaidika na fedha inazotumia katika miradi mikubwa ya maendeleo inayoendelea kufanyika.

Alisema kongamano hilo lililohudhuriwa na wadau kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Tanesco, TPDC na Wizara ya Fedha na Mipango lilikuwa na lengo kubwa la kuangalia vyanzo mbalimbali vya fedha vinavyopatikana katika miradi mbalimbali mikubwa inayofanywa na serikali pamoja na kuangalia usimamizi wa hatari katika miamala ya kifedha inayoweza kutokea katika miradi hiyo.

"Kama mjuavyo miradi mbalimbali mikubwa inayofanywa na serikali ya awamu ya tano kama vile mradi wa reli ya kisasa (SGR), mradi wa umeme wa Mto Rufiji wa Stiegler's Gorge, ujenzi wa barabara na madaraja, baadhi ya miradi hufanywa kwa mikopo kutoka pande tofauti, hivyo tulitaka kuonyesha uwezo wetu kama NBC katika kusaidia upatikanaji wa fedha na pia linapokuja suala la uzimamizi wa hatari za kifedha katika miamala hiyo.

"Kilicho kikubwa ni kwa NBC kuangalia uwezo wetu kwa njia tofauti tofauti ikiwamo katika kukopesha, lakini pia kuona serikali haipati hasara kutokana na masuala ya riba, fedha za kigeni na kushuka kwa thamani ya shilingi, hivyo NBC tumejiandaa kushirikiana na serikali kikamilifu katika kutimiza azma yake, kwa uwezo wetu tunaweza kushirikiana zaidi na zaidi," aliongeza Nalitolela.

Alisema kama NBC inamilikiwa kwa pamoja na Serikali ya Tanzania, Benki ya Absa ya Afrika Kusini pamoja na Benki ya Dunia, hii huiweka NBC katika nafasi nzuri ya kusaidia juhudi za serikali.

Katika kongamano hilo pia NBC ilileta wataalamu kutoka benki mama ya Absa ili kuonyesha uzoefu wao walioupata kupitia miamala waliyofanya na serikali za nchi mbalimbali barani Afrika.

## Watakiwa kuongeza thamani bidhaa

**Na Felix Andrew**

WAKULIMA, wafugaji na wavuvi nchini wametakiwa kuongeza thamani bidhaa zao kwa kuhakikisha kuwa zinathibitishwa ubora wake katika Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Athuman Ngenya, kwenye banda la TBS katika Maonyesho ya Nanenane yanayofanyika kitaifa eneo la Nyakabindi mkoani Simiyu.

Dk. Ngenya alisema wazalishaji wa bidhaa za kilimo wanatakiwa kuongeza thamani ya mazao yao kwa kuchakata na kufungasha kwa kuzingatia viwango vya kitaifa vilivyopo na hatimaye kupata leseni ya kutumia alama ya ubora ya TBS kwenye bidhaa zao.

Kwa upande wa mazao ya mifugo na uvuvi, alisema pia thamani ya mazao yao itaongezeka kwa kusindika na kufungasha bidhaa hizo kwa kuzingatia viwango vilivyopo na kwamba huduma ya uthibitishaji wa bidhaa za wazalishaji wadogo wadogo na wakati inatolewa bure kwa miaka mitatu ya kwanza.

Alisema kwa kuthibitisha ubora wa bidhaa hizo mkulima, mvuvi na mfugaji hatakuwa na kikwazo chochote cha kibiashara kwani bidhaa hizo zitakubalika ndani na nje ya nchi.

Aliongeza kuwa TBS inapohakiki ubora wa bidhaa hizo zinakubalika mahali popote kwani maabara za shirika zina vyeti vya umahiri na wataalamu waliobobea katika upimaji, hivyo majibu ya ufaulu wa sampuli yanapotoka yanakubalika mahali popote duniani.

"Ninawasihi waache kuuza bidhaa zao kiholela kwani kwa kufanya hivyo bidhaa hizo zinauzwa kwa bei ya chini kwa kuwa zina kuwa hazina thamani kutokana na ubora wake kutothibitishwa na Shirika la Viwango Tanzania," alisisitiza.

Alisema TBS iko kwa ajili ya kuwezesha biashara, hivyo wananchi wanapaswa kuondoa dhana potofu ya kuona kama ni kituo cha polisi, badala yake walitumie Shirika hili kikamilifu kwani lilianzishwa kwa ajili ya kuwahudumia watu wote kwa kuhakikisha kuwa wanatengeneza na kupata bidhaa bora wakati wote.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa TBS, Roida Andusamile, alisema wakiwa katika maonesho hayo wamejipanga kutoa elimu kwa wakulima, wavuvi na wafugaji wote wanaoshiriki kwa kuwapitia katika mabanda yao na kuwaeleza utaratibu wakufuata ili kuthibitisha ubora wa bidhaa wanazotengeneza.

Andusamile alisema pia watatumia fursa ya maonyesho hayo kupokea maoni na ushauri kutoka kwa wadau mbalimbali; lengo likiwa ni kuboresha huduma zitolewazo na shirika.

## HABARI KITAIFA

# Ajitoa kusikiliza kesi ya mauaji ya kukusudia

**Na Hellen Mwango**

NAIBU Msajili Pamela Mazengo, amejitoa kusikiliza kesi inayomkabili Godfrey Nkwambi, baada ya mshtakiwa huyo kudai kwamba hana imani naye na kwamba hawezi kumtendea haki dhidi ya tuhuma za kumuua kwa makusudi mke wake Bahati Hussein.

Mazengo alipangiwa kusikiliza kesi hiyo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyopewa mamlaka ya kusikiliza kesi za mauaji. Nkwambi alikutwa na kesi ya kujibu Julai 9, baada ya upande wa Jamhuri kufunga ushahidi wake na mahakama hiyo kupanga mshtakiwa huyo kujitetea Julai 18, mwaka huu.

Hata hivyo, mshtakiwa alidai kuwa hawezi kujitetea kwa sababu ni mgonjwa na mahakama ilipiga kalenda mpaka Julai 24, mwaka huu, lakini akadai kuwa hana imani na msajili huyo kwa madai hata mtendea haki.

Msajili alijitoa kusikiliza kesi hiyo na kurejesha jalada kwa Naibu Msajili wa Kanda ya Dar es Salaam kwa ajili ya kupangiwa msajili mwingine wa kuisikiliza. Upande wa Jamhuri unaongozwa na Wakili wa Serikali, Erick Shija.

Mapema mahakamani hapo, watoto wawili wa marehemu akiwamo mtoto wa miaka 10, wakati mama yake anauawa alikuwa na miaka mitano, alidai mahakamani siku ya tukio usiku wakiwa wamelala alimwona baba yake wa kambo (mshtakiwa) akimnyonga mama yake Bahati. Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa Juni 21, 2014 eneo la Ulongoni Nkwambi alimuua kwa makusudi mke wake Bahati.

Mshtakiwa alifunguliwa kesi na kufikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam na kusomewa mashtaka ya mauaji ya kukusudia dhidi ya mke wake.

# Kishindo cha SADC kuanza Dar es Salaam leo

INATOKA UK. 2

Mashariki, Dk. Damas Ndumbaro, alisema Agosti 10 ndipo mkutano huo unaanza rasmi kwa wataalamu ambao ni makatibu wakuu wa wizara husika kutoka nchi mbalimbali, ambao watakutana na Katibu Mkuu wa wizara hiyo atakabidhiwa kuwa mwenyekiti wa wataalamu hao.

Alisema baada ya hapo watakutana mawaziri wanaohusika na utakelezaji, ambapo Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, atakabidhiwa Uenyekiti wa Baraza la Mawaziri wa SADC.

Alisema pia katika mkutano unaohusisha wakuu wa serikali na nchi 16, Rais Magufuli atakabidhiwa uenyekiti wa SADC, kisha Agosti 16 kutakuwa na Mkutano wa Troika ambao utawahusu marais watatu, aliyekabidhi uenyekiti wake ambaye ni Rais wa Namibia, Have Geingob, anayempokea ambaye ni Rais Magufuli na aliyemaliza uenyekiti wake Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa.

"Tunawahamasisha wananchi na wadau wote kwa ujumla kuchangamkia fursa hii, wajasiriamali, hadi mamalishe wamejisajili maonyesho hayo hayana kiingilio ni bure, wajisajili kwenye tovuti ya SADC Tanzania ili wapate tiketi," alisema.

Kwa upande wake Ofisa Mwandamizi wa SADC anayeshughulikia masuala ya viwanda na ushindani na biashara, Dk. Johansein Rutaihwa, alisema Tanzania imepiga hatua kubwa kiuchumi kwa kufikisha asilimia saba ikifuatiwa na Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC) ambayo uchumi wake umekua kwa asilimia 6.3.

Alisema mkakati wa SADC ni kuwezesha nchi kukuwa kiuchumi ili wananchi wa nchi wanachama waweze kuishi kwa dola 2000 hadi 9000 ifikapo mwaka 2050.

Alisema katika kuhakikisha mkakati waliojiwekea unafanikiwa, wamekubaliana kudhibiti rushwa na ufisadi kwa kuhakikisha fedha za umma haziishii mikononi mwa watu bali zinatumika kutekeleza sera zilizowekwa.




# Sababu za ndege kuua zaelezwa

INATOKA UK. 2

Aidha, taarifa iliyosambaa kwenye mitandao ya kijamii, baadhi ya mashuhuda walisema waliona ndege hiyo ikiyumba na baadaye kusikia mlio mkubwa na moshi mwingi.

Taarifa ya Msemaji wa Idara ya Mawasiliano ya Kimataifa na Ushirikiano, Clayson Manyela, ilisema lengo la shirika hilo ni vijana kuunda ndege ambayo ilitumiwa na vijana kusafiria kutoka Cape Town, Afrika Kusini hadi Cairo, Misri na kwamba iliyopata ajali haikuwa kwa ajili ya safari hiyo iliyofanyika Julai 8, mwaka huu.

"Ndoto ya vijana hawa ilikuwa ni kusafiri kutoka Captown hadi Cairo kwa ndege waliyoiunda wenyewe," ilisema taarifa hiyo ambayo pia iko kwenye mtandao wa 24 news wa Afrika Kusini.

Shuhuda wa ajali hiyo, Mkombozi Kasemwa, alisema aliona ndege ikitokea kaskazini na muda kidogo ilikata kona kuelekea Mashariki, kidogo ikarudi kaskazini ikapiga hatua kidogo kurudi mashariki ikakata kona tena kurudi Kaskazini tukasikia mngurumo imeanguka na moshi mwingi imelipuka.

"Tulikuja eneo la tukio tukakuta moto unawaka na wananchi wakawa wanawatoa marehemu.

Mkuu wa Wilaya ya Sikonge, Peter Magiri, alisema raia hao wawili ni wakazi wa Daban Afrika Kusini na kwamba miili yao imehifadhiwa katika Hospitali ya Mkoa wa Tabora Kitete.

# Wakulima waitwa kujiunga na NSSF

INATOKA UK. 4

hifadhi kwa watakaojiunga na NSSF.

Alisema uwapo wa shirika hilo wana uhakika kwamba kilimo chao kitakuwa endelevu kwa sababu wakulima wadogo watakaojiunga watapata faida ya mikopo itakayowasaidia kuendeleza kilimo chao kwa kununua mbegu na pembejeo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Busega, mkoani Simiyu, Tano Mwera, aliwaomba wananchi wa wilaya hiyo na wa Mkoa wa Mara, Mwanza, Shinyanga, Simiyu hasa walioko kwenye sekta binafsi na isiyo rasmi kujiunga na NSSF.

Tano alisema sasa shirika hilo limeanzisha mpango wa taifa wa sekta isiyo rasmi, hivyo aliwataka wananchi kujiunga na mpango huo ili waweze kunufaika na mafao mbalimbali.

Alisema zipo faida nyingi kwa mtu aliyejiunga na Hifadhi ya Jamii, kuwa na uhakika wa maisha yake ya sasa na ya baadaye.

Jackson Alfred ni mwanachama wa Shirika hilo kwa miaka 17, alisema anajisikia fahari kuwa mwanachama kwa kuwa anapata faida mbalimbali ikiwamo huduma za matibabu.

Aliwasihi wananchi walioko kwenye sekta rasmi na isiyokuwa rasmi kujiunga na NSSF ili waweze kufaidika na mafao mbalimbali yanayotolewa.

Meneja wa NSSF Mkoa wa Simiyu, Tullo Masanja, alisema katika maonyesho hayo wanatoa huduma mbalimbali ikiwamo kuandikisha wanachama wapya kutoka sekta rasmi na isiyokuwa rasmi.

# Lukuvi aagiza uchunguzi mipaka Msimbazi Center

INATOKA UK. 4

alitengenezewa mchoro mpya tofauti na ulioko wizarani.

Lukuvi alimtaka mpimaji wa Manispaa ya Ilala, Lugano Mwambuluma, kuhakikisha anafufua mipaka ya eneo hilo kwa kupima na kulinganisha mchoro wa eneo hilo uliopo manispaa na ule wa wizara na kumkabidhi matokeo ya upimaji huo ndani ya wiki moja kuanzia Agosti 2, 2019.

Waziri Lukuvi alisema, hataki kuamini moja kwa moja kwa moja kama eneo lenye kituo cha mafuta cha Victoria, linamilikiwa kihalali na mmiliki wake Matemba kama anavyodai mpaka hapo atakapopata jibu kutoka kwa wataalamu aliowatuma kuhakiki eneo hilo.

Pia amewaasa wananchi kutonunua maeneo mtaani na kutaka kabla ya kununua ardhi lazima wakajiridhishe wizarani iwapo eneo wanalotaka kununua mmiliki wake anamiliki kihalali.

Alisema, mtu yeyote anayetaka kununua eneo lazima akajiridhishe katika Ofisi za Msajili wa Hati ili kubaini uhalali wa umiliki wa muuzaji wa eneo huo.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Nicodemus Mkama, akimpongeza Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, kwa mafanikio makubwa ya hatifungani ya NMB ambayo ilipata mafanikio ya asilimia 333 kwenye hafla ya kuorodhesha rasmi hatifungani hiyo jijini Dar es Salaam juzi. Wengine ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Soko la Hisa la Dar es Salaam, Moremi Marwa (Wa kwanza kushoto) na Mkuu wa Uhusiano na Uwekezaji wa Benki ya Stanbic, Manzi Rwegasira, mwanzo kulia.

# Sensa ya kilimo, uvuvi, ufugaji mbioni

**Na Ashton Balaigwa,** SIMIYU

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS) inakusudia kufanya sensa ya kilimo, uvuvi na ufugaji nchini ili kupata matokeo ya mchango wa sekta hiyo, kwenye pato la Taifa na kupanga mikakati mingine mipya.

Kwa kuanzia, timu ya wataalamu wa NBS ipo mkoani Morogoro kwa ajili ya kufanya zoezi la majaribio katika mikoa sita ya Bara na miwili Zanzibar na kuwataka wananchi kutoa ushirikiano wa kutosha ili kusaidia kupatikana kwa takwimu hizo.

Akizungumza katika Maonyesho ya Kilimo ya Nanenane yanayoendelea mkoani Simiyu, Mtakwimu Mwandamizi kutoka ofisi hiyo, Samwel Kawa, alisema kupatikana kwa takwimu hizo zitawezesha kupanga, kupima na kufuatilia Tathimini ya Programu ya Pili ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP II) . Alisema pia kupatikana kwa takwimu hizo kutasaidia kufikia uchumi wa kati wa Tanzania ya viwanda pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa pili wa Taifa wa Maendeleo na Usalama wa Chakula pamoja na vita dhidi ya umaskini. Kawa alisema sensa ya kilimo ya mwisho ilifanyika mwaka 2007/2008, hivyo kufanyika kwa sensa mpya kutatoa takwimu mpya kuhusu uzalishaji wa mazao, idadi sahihi ya mifugo pamoja na mazao yatokanayo na mifugo. "Lengo la sensa hii ni kupata taarifa sahihi za hivi karibuni za 2018/19 zinazohusiana na uzalishaji wa mazao, idadi ya mifugo na mazao yatokanayo na mifugo," alisema Kawa.

Kwa upande wake, Ofisa Masoko wa Ofisi hiyo, Andrew Punjila, alisema sensa hiyo itakusanya taarifa kuhusu takwimu na hali ya takwimu nchini. Alisema kupitia takwimu hizo, itasaidia serikali kujua mchango wa sekta katika pato la taifa, kupima mikakati yake ya kufikia Tanzania ya viwanda na inatoa fursa kwa wadau wengine kujua fursa na changamoto ya sekta hiyo.

# Wanawake wahamasishwa kugombea

**Na Sabato Kasika**

WANAWAKE wametakiwa kuwa mstari wa mbele kujitokeza katika kuwania nafasi za uongozi katika siasa kwenye ngazi mbalimbali ili kuongeza idadi ya wanawake kuchaguliwa badala ya kutegemea viti maalum.

Wito huo ulitolewa juzi jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Taasisi ya Kuwezesha Wanawake na Kulinda Watoto iitwayo Ekama Developement Foundation Tanzania, Kokuteta Mutembei.

Mkurugenzi huyo alikuwa akizungumza katika hafla ya kutunuku vyeti kwa wanawake kutoka vyama mbalimbali vya siasa waliopata mafunzo ya siasa na uongozi yaliyotolewa na taasisi hiyo kwa muda wa mwaka mmoja.

Alisema, wanawake wanatakiwa kuondokana na dhana ya kuendelea kuongozwa kwa kila nafasi za uongozi ndani ya vyama vya siasa bali wajiongeze kwa kuwania wenyewe uongozi.

"Wanawake ni kundi ambalo ni mdau mkubwa, hasa katika demokrasia ya vyama vingi, wanawake wanashiriki katika siasa kwa nafasi mbalimbali kama wagombea na wapigakura," alisema Mutembei.

Aliongeza kuwa wanawake pia ni wahamasishaji kwenye kampeni, wasimamizi kwenye uchaguzi na waandishi wa wapigakura, lakini ushiriki wao wa moja kwa moja kwenye maamuzi ya kisiasa bado uko chini ya asilimia 50.

"Hii inatokana na mtazamo wa kijamii na wanawake wenyewe kuhusu siasa, hivyo nyie mliopata mafunzo mkawe chachu kwenye maeneo yenu, muwanie uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa," alisema.

Alisema wasiishie hapo tu bali hata katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 wajitokeze kuwania udiwani na ubunge ili ikiwezekana, idadi ya madiwani na wabunge wa kuchaguliwa iwe sawa kati ya wanawake na wanaume.

"Wanawake tutumie fursa ya uchaguzi wa serikali za mitaa kuwania nafasi mbalimbali za uongozi, tusisubiri nafasi za viti maalum au kuteuliwa, kwani tuna uwezo wa kusimama wenyewe kuhakikisha tunapata nafasi za uongozi kama walivyo wanaume," alisema.

Mutembei alisema, maratajio yake ni kwamba wanawake waliopata mafunzo hayo watakuwa mfano kwa wengine, kwa vile wamefundisha mbinu zote za kuwawezesha kuwania uongozi katika ngazi mbalimbali kwenye siasa.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, wahitimu wa mafunzo hayo walikuwa ni zaidi ya 20, na walitoka katika vyama vya siasa vikiwamo vyenye wabunge vikiwamo vya CCM, Chadema, NCCR-Mageuzi, ACT-Wazalendo.

# Bodaboda Dar es Salaam waiomba serikali

**Na Yasmine Protace**

MADEREVA wa bodaboda, wameiomba serikali iwaruhusu wafanye biashara kwa kuingia katika maeneo ya Kariakoo, vituo vya afya na mjini, jijini Dar es Salaam.

Ombi hilo lilitolewa na Mwenyekiti wa Umoja wa Bodaboda Mliman City, Jafary Yahaya, katika uzinduzi wa kituo hicho.

"Tunaiomba serikali itusaidie, ituruhusu tufanye kazi maeneo ya mjini, Kariakoo na maeneo ya vituo vya afya," alisema.

Aliongeza kuwa kutoingia kunawafanya wafanye biashara katika mazingira magumu.

Alisema kikundi chao kilianzishwa mwaka 2014 na kusajiliwa mwaka jana, ambapo sasa kuna wanachama 25, na kuwa malengo ya kikundi chao ni kumiliki shamba kubwa ambalo litawawezesha kujiongezea kipato.

Alisema kuna mfadhili wanamwomba ajitokeze aweze kuwasaidia wapate shamba ambalo litawasaidia kujiongezea kipato.

Akizungumzia kikundi chao anasema kuwa kila mwana kikundi ana bima ya afya na kikundi kimefanikiwa kufungua akaunti mwaka jana, ambapo mpaka sasa wana zaidi ya shilingi milioni moja.

Akizungumzia mafanikio ya kikundi, alisema kila mwanachama ambaye atapatwa na tatizo la kiafya, kikundi kinamchangia kila siku Sh. 1,000.

Kuhusu kukuzwa mtaji wao katika benki, alisema wanachama kila wiki wanachangia shilingi 20,000 kwa ajili ya kuziweka benki.

Alisema kuwa wanakumbana na changamoto ya kutoruhusiwa kuingia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, mjini, Kariakoo na vituo vya afya.

Changamoto nyingine ni kutokuwa na bodaboda za kumiliki wao, na kuwa bodaboda wanazoendesha ni za watu wengine, wao ni vibarua.

Ofisa Mtendaji Kata ya Makongo, Husina Hondo, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa kituo hicho, alisema changamoto hizo atazifikisha kwa wakubwa ambao ndio watazitolea majibu.

Alikipongeza kikundi hicho na kuvitaka vingine viige mfano kwa kuweka akiba na kuwa na kadi za bima. Alisema vikundi vikiwapo ni rahisi kupatiwa mikopo ambayo inatolewa na serikali.

# Mbunge atoa mifuko 100 ya saruji shuleni

**Na Sabato Kasika**

MBUNGE wa Musoma Vijijini mkoani Mara, Prof. Sospeter Muhongo, ametoa mifuko 100 ya saruji ili kusaidia katika ujenzi wa sekondari mpya inayojengwa kwa nguvu za wananchi wa vijiji vya Kakisheri na Kigera Etuma.

Prof. Muhongo alitoa mifuko hiyo juzi wakati akiendesha harambee ya kuchangia ujenzi huo kwenye kijiji cha Kigera Etuma ambako sekondari hiyo inajengwa ikiwa ni ya pili katika Kata ya Nyakatende.

Mbali na mbunge huyo, wakazi wa vijiji vya Kakisheri na Kigera Etuma waliokuwapo kwenye harembee hiyo, walichangia fedha taslimu Sh. 324,000 na mifuko mingine 68 ya saruji.

Mwenyekiti wa kikundi cha wadau wakuu wa mradi wa ujenzi wa sekondari hiyo, Nyakiriga Kabende, alisema ujenzi unaendelea kwa kasi na akawaomba wadau wengine kuunga mkono juhudi za wananchi wa vijiji hivyo.

Mbunge wetu ni mdau mkubwa wa maendeleo ya elimu na ameendesha harambee ya kuchangia ujenzi wa sekondari yetu na yeye mwenyewe akatoa mifuko 100 ya saruji," alisema Kabende.

Kabende alisema, wakazi wa vijiji hivyo waliona kwamba sekondari moja ya Nyakatende iliyopo Kata ya Nyakatende haitoshi, hivyo wameamua kujenga nyingine kwa nguvu zao

"Hadi sasa maboma ya vyumba viwili vya madarasa yamefikia hatua ya kuezekwa, na pia yapo matofali ya kutosha kujenga jengo la utawala, na wananchi wanaendelea kutoa michango," alisema.

Alifafanua kuwa wamekubaliana kila mwenye umri wa kuanzia miaka 18 achangie tofali moja, na kwamba mawe, kokoto, mchanga na maji vinasombwa kwa zamu, kitongoji kwa kitongoji.

Kwa upande wake Prof. Muhongo aliliambia gazeti hili kuwa leo atafanya harambee nyingine kwa ajili ya kuchangia ujenzi wa sekondari nyingine ya kijiji cha Nyasaungu, unaofanywa na wananchi.

Mbunge huyo alisema, kabla ya kufanya harambee hiyo, asubuhi atafanya kikao na Bodi ya Shule ya Sekondari Bwasi, kushawishi ili shule hiyo inayomilikiwa na Kanisa la Kisabato ianzishe kidato cha sita.

Aliongeza kuwa jimboni mwake kuna shule 21 za sekondari, huku mbili zikiwa za binafsi na pia kidato cha sita zipo mbili tu za Kasoma ambayo ni ya serikali na Nyegina, inayomilikiwa na Kanisa Katoliki.

"Idadi hiyo ni ndogo, tusipochangamka, Mwalimu Nyerere University of Agriculture and Technology itakapoanza kuchukua wanafunzi karibu wote wa masomo ya sayansi, sisi mkoa wa Mara tutakuwa wasindikizaji," alisema.

# Zanzibar yasaidiwa matrekta ya mil. 150/-

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo nchini(TADB) itaendelea kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Zanzibar kutoa elimu kwa wakulima kuhusu umuhimu wa mikopo inayotolewa benki hiyo, ili kuongeza uzalishaji wenye tija na kuinua maisha ya mkulima.

Akizungumza baada ya kumkabidhi matreka mawili yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 150 Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohammed Shein, Mkurugenzi wa Fedha na Uwekezaji wa TADB, Derick Rugemala, alisema matreka yatagaiwa kwenye vyama vya msingi vya wakulima.

"Tumekabidhi matreka haya yaweze kusaidia sekta ya kilimo na kuongeza uzalishaji wa mazao hasa mpunga hali itakayosaidia kuongezeka kwa kipato cha mkulima," alisema Rugemala na kuongeza kuwa zoezi hilo limefanyika sambamba na ufunguzi wa sherehe za Nanenane.

Alisema TADB itaendelea kushirikiana pia na wakulima ndani ya Zanzibar ili waweze kunufaika na uwapo wa Benki ya Kilimo ambayo ndiyo mkombozi katika kutatua changamoto za wakulima nchini.

"Lengo la TADB ni kuona tija katika uzalishaji wa mazao nchini unaongezeka na kwa kuhakikisha hilo linafanikiwa benki inaendelea kuhamasisha wananchi kutumia fursa ya uwepo wa benki hiyo katika kupata mikopo itakayosaidia kukuza shughuli za kilimo," alisema Rugemala.

Aliongezea kuwa benki inawawezesha wananchi kwa kuwapatia mbinu na elimu ya kilimo cha kisasa na pia mitaji katika kuendeleza sekta ya kilimo lengo likiwa kutekeleza azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kati na viwanda.

"Mkakati wa TADB ni kuongeza uzalishaji katika mnyororo wa thamani katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi hivyo tunahakikisha mazingira yanakuwa wezeshe katika uzalishaji na uongezaji thamani wa mazao na kuyafikia masoko," alisema Rugemala.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wakulima waliotembelea banda la TADB katika maonesho ya kilimo Zanzibar waliishukuru benki hiyo kwa kutoa matreka ambayo yatawasaidia katika kuendeleza kilimo.

Mkulima Juma Hajji, alisema changamoto kubwa wanayokutana nayo katika kilimo ni nyenzo za kilimo hivyo kupatikana matrekta haya yatasaidia kilimo kuwa cha kisasa na kuongeza tija na uzalishaji wa mazao.

"Kwa kuletewa treka hizi wakulima tunauhakikisha sasa wa kuongeza uzalishaji wa mpunga na hatimaye kujitosheleza kwa chakula na hata kufikia kuuza katika masoko ya nje," alisema Hajji. Ofisa kutoka Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Nassor Salim Mohamed, alisema utaratibu mzuri utawekwa wa namna bora ya matumizi ya matrekta ili wakulima wengi waweze kunufaika.




Meneja Masoko na Mawasiliano wa GSM Group, Matina Nkurlu (kulia), akimkaribisha Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina (mwenye skafu), jana, kuona bidhaa zinazozaliwa yakiwamo magodoro katika banda lao kwenye viwanja vya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere vya maonyesho ya wakulima, wafugaji na wavuvi ya Nanenane Kanda ya Mashariki inayoshirikisha mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga na Morogoro.

# Wanafunzi waiomba serikali chumba cha kujisitiri

**Na Yasmine Protace**

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Kelezange Kata ya Kivule Wilaya ya Ilala mkoa wa Dar es Salaam, wameiomba serikali iwasaidie kwa kuwajengea chumba cha kujisitiri.

Walisema kutokuwapo na chumba cha kujisitiri na shimo la taka mbichi, kumekuwa kukiwafanya wakiingia katika siku zao wanapatwa na shida.

Hayo yalisemwa na Helen Jacobo wakati akisoma risala kwa ugeni uliofika shuleni hapo ukitokea TGNP Mtandao na kuzungumza na klabu za jinsia ambazo zinasimamiwa na TGNP Mtandao.

"Changamoto kubwa tulionayo hapa shule ni kutokuwa na shimo la kutunzia taka mbichi, kutokuwa na chumba cha kujistiri na tunachangamoto ya upungufu wa matundu ya choo 10," alisema.

Alisema katika shule hiyo kuna klabu ambayo inafundisha masuala ya jinsia na ina wanachama wasiopungua 40.

Alisema wanaishukuru TGNP Mtandao kwa kuwaelisha na kufanikiwa kufungua klabu hiyo ambayo imekuwa mkombozi kwa wanafunzi wote katika kuzijua haki zao katika masuala ya jinsia.


Akizungumzia kampeni ya 1.5.5 namlinda, alisema imezaa matunda kwa wanafunzi ambapo ulinzi wanaanzia shule kwa kuelimishana na hata wakiwa majumbani na maeneo mbalimbali wanaitaja kampeni hiyo kuwa mkombozi kwao.

Wakati huo huo, klabu ya jinsia ya Shule ya Msingi Umoja Kata ya Mabibo, jijini Dar es Salaam, inakabiliwa na changamoto ya kutokuwa na chumba cha kujisitiri na taulo za kike.

Zainabu Said, mwanafunzi wa shule hiyo, ambaye ni mmoja wa wanaklabu wa jinsia wa shule hiyo, alisema wamenufaika na elimu ya jinsia kupitia klabu hiyo kwa kupitia sanaa mbalimbali za maonyesho.

Alisema klabu yao inawanachama 59 na imekuwa ikielimisha wanafunzi masuala ya jinsia.

Akizungumzia changamoto, alisema ukosefu wa taulo za kike chumba cha kubadilishia, upungufu wa matundu ya vyoo 40 kwao imekuwa kikwazo.



# Watu wazima, walezi wabainika kuwafanyia ukatili watoto

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

IDADI kubwa ya watoto wanaolawitiwa na kubakwa katika jamii imebainika wanafanyiwa na watu wazima ambao wanastahili kuwa wazazi wao ambao wangekuwa wanabeba jukumu la kuwalea, lakini wanageuka kuwa wanyama.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki iliyopita na Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Babati Mathias Focus, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu wanavyowasaidia watoto kujikinga na watu wenye nia mbaya.

"Robo ya mwaka iliyopita kesi za ubakaji na ulawiti zilikuwa sita, ambapo watoto wengi wanaobakwa au kulawitiwa ni miaka mitano mpaka miaka tisa au 10," alisema Focus.

Vile vile, alisema idadi kubwa ya watu wanaofanya vitendo vya ubakaji na ulawiti ni watu wazima hasa wanaume ambao wengine wanastahili kuwa wazazi au walezi wa watoto hao.

Alisema, kwa mujibu wa utafiti alioufanya, amegundua chanzo cha wanaume kufanya unyama huo kwa watoto ni kuamini katika imani za kishirikina, mmomonyoko wa maadili na utandawazi.

"Kwa mfano kuna watu wanaenda kuona picha kwenye vibanda halafu baada ya kuona hizo picha wengi wao wanakuja kuzifanyia majaribio na hivyo kujikuta wanaangukia kwenye uovu huo kwa watoto," alisema.

Focus alisema wenye tabia hiyo hawana budi kuacha na kusaidia jukumu la malezi na kuangalia usalama wa watoto kipindi wanapokuwa wanacheza.

Alisema katika kukabiliana na watu wanaowafanyia unyama huo watoto, kitengo chake kimekuwa kikitoa elimu kwenye mikutano ya hadhara ya vijiji na kuwafundisha wanafunzi mbinu za kuwakwepa watu wenye nia ovu au kuwaripoti kwenye mamlaka za serikali ili mtoto akifanyiwa ukatili huo aweze kupata haki yake. Pia, alisema wazazi wakigundua mtoto amebakwa au amelawitiwa kwepuke kumwogesha mtoto ndani ya saa 72 tangu alipofanyiwa kitendo hicho mpaka afikishwe hospitali kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi na daktari.

"Lakini hili wengi wao hawafuati masharti hayo na hivyo kusababisha upotevu wa ushahidi kwa wahusika sababu wengi hukimbilia kuogesha mtoto," alisema.

Alizitaja changamoto zinazowakabili katika kupambana na vitendo vya kikatili kwa watoto kuwa ni ushirikiano duni kutoka kwenye jamii, mashahidi kugoma kutoa ushahidi mahakamani kesi inapofunguliwa au hata katika hatua za awali za kuwasaka wabakaji na walawiti na watu wengine hawajui waripoti wapi matukio ya namna hiyo yanapojitokeza.

Alisema katika kusimamia haki za watoto sheria ya mtoto ya mwaka 2009 ndio inatumika ambayo inaeleza wazi haki za mtoto ikiwamo ulinzi hivyo wazazi wanapowaachia watoto wakaenda kucheza wasikokujua wanachangia kuvunja sheria hiyo, ambayo inawahusu wote, bila kujali huyo unayemtetea ni mtoto wake au laa na wanaoivunja kwa kufanya unyama huo wanakidhana nayo.

Naye Msaidizi wa Kisheria kutoka Shirika la Bapace, Said Mnyaruge, alisema wazazi wanastahili kuwakagua wanapotoka kucheza au wanapotoka vituo vya kulelea watoto au shuleni ili kujiridhisha kama wako salama.

Mkazi wa Negamsi, Jackline Daniel, alishauri serikali kupiga marufuku vibanda vinavyoonyesha picha za aina mbalimbali na kuchangia watoto kufanyiwa unyama huo kwenye maeneo hayo.



Mkuu wa Wilaya ya Kiteto mkoani Manyara, Mhandisi Tumaini Magessa, akimpongeza Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa huo, Ester Mahawe, kwa kuandaa tamasha la wajasiriamali na uvumbuzi wa vipaji juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Serikali yaombwa kuinusuru Shule ya Msingi Loswaki

**Novatus Makunga,** SIMANJIRO

SERIKALI imeombwa kupeleka walimu mapema iwezekanavyo katika Shule ya Msingi ya Loswaki, wilayani Simanjiro mkoani Manyara, yenye wanafunzi 800 na walimu watano pekee.

Ombi hilo lilichukua nafasi kubwa katika hafla ya kukabidhi miundombinu mipya iliyokarabatiwa ya shule hiyo kwa halmashauri ya wilaya hiyo, lilitolewa kwa Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro Mhandisi Zephania Chaula.

Miundombinu hiyo iliyojengwa na kukarabatiwa na shirika lisilokuwa la kiserikali la ECLAT kwa ufadhili wa Shirika la Upendo la Ujerumani na kugharimu Sh. milioni 330.

Mwenyekiti wa Upendo, Dk. Fred Heimbach, alimtaka Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, kuhakikisha shule hiyo inapata walimu wanaohitajika ili wanafunzi waweze kupata elimu bora.

"Sisi tumesaidia uboreshaji wa miundombinu, lakini hatuna uwezo wa kuchukua walimu Ujerumani na kuwaleta hapa, hivyo ni vyema Mkuu wa Wilaya ukaliangalia tatizo hili la walimu kwa uzito mkubwa kwa ajili ya maendeleo ya watoto wetu," alisema.

Dk. Heimbach alisema elimu ni msingi wa maisha duniani kote, hivyo ni lazima jamii iwapeleke shule huku walimu wakiwa na jukumu la kuhakikisha wanafundisha vizuri kwa ajili ya kuwatengenezea maisha bora ya baadaye.

Naye Diwani wa Terrat ilipo shule hiyo, Jackson Materi, alimtaka mkuu wa wilaya kuchukua jukumu la kuhakikisha shule inapata walimu, ili iweze kufanya vizuri na kujinasua kutoka miongoni mwa shule kumi zilizofanya vibaya katika mtihani wa kuhitimu darasa la saba kwa msimu uliopita.

Alisema shule hiyo inahitaji walimu zaidi ya 15.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa ECLAT, Peter Toima, aliitaka jamii ya wafugaji wa Kimasai kutambua kwamba wakiendelea na mila zao bila kuzichuja wataachwa nyuma kimaendeleo na kuwataka kuhakikisha kila mtoto anahitimu baada ya kuanza shule.

"Tutaweza kutatua changamoto nyingi zinazotukabili endapo tu tutazingatia elimu kwa watoto wetu, kwa kuwa mila ambazo tumekuwa tukizikumbatia kwa miaka mingi hazijatupeleka popote pale hivyo tuwe makini," alisema.

Akijibu hoja zilizojitokeza, Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Mhandisi Chaula, alitoa ahadi ya kupeleka walimu katika shule hiyo wilaya hiyo itakapopokea walimu wapya.

Alisema wilaya hiyo ina uhaba mkubwa wa walimu wapatao 460.

Hata hivyo, Mhandisi Chaula aliutaka uongozi wa shule hiyo kuweka mkakati wa kujinasua kutoka katika kundi la shule zilizofanya vibaya katika mtihani wa kuhitimu darasa la saba kwa kufaulisha kwa asilimia 26 pekee. Aliagiza kila shule wilayani humo kuandaa kambi za kitaalamu na kwamba zimeonyesha kuwa na mafanikio makubwa akitolea mfano wa Shule ya Msingi Naisinyai ambayo ilikuwa inashika mkia, lakini kwa sasa inafanya vizuri kutokana na makambi hayo.

Vile vile, Mhandisi Chaula, alikemea vitendo vya kuwapa ujauzito wanafunzi na kuonya kwamba atakayebainika atakamatwa na kufikishwa mahakamani na kusisitiza atakabiliwa na adhabu ya kifungo kisichopungua miaka 30, huku akiacha mke, watoto na mifugo yake.

# RC Mghwira awaasa waandaaji Nanenane

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, amewataka maofisa ugani wa mikoa ya Kanda ya Kaskazini kuacha utamaduni wa kufanya maonyesho ya Nanenane kwa mfumo wa kimaonyesho zaidi badala yake waandae yaendane na uhalisia wa bidhaa zinazozalishwa na wakulima vijijini.

Akizungumza jana jijini Arusha katika maonyesho ya 26 ya Nanenane Kanda ya Kaskazini, Mghwira, alisema, shughuli zinazoonyeshwa katika mabanda zingekuwa katika uhalisia wa kweli sekta ya kilimo, uvuvi na ufugaji, ingepiga hatua.

"Maofisa ugani mnafanya kazi ya kimaonyesho zaidi kuliko ya kiuhalisia zaidi mnatakiwa kufanya kazi hii kutoka katika mabanda na kwenda vijijini kwani walengwa wengi wapo huko," alisema Mghwira.

"Naomba viongozi wenzangu Nanenane hii iwe ya mwisho kufanyika kimaonyesho zaidi na maonyesho yajayo napendekeza tukafanyie huko vijijini angalau tuchague wilaya moja ya kufanyika maonyesho kutoka na maonyesho ya kila mwaka yameshazoeleka na washiriki," alisisitiza.

Hata hivyo, alishauri viongozi kupita mashambani kuona namna uzalishaji unavyofanyika huko vijijini na siyo kusubiri kuona bidhaa katika maonyesho.

Aliongeza kuwa ili kufikia malengo, Mwenyekiti wa maandalizi ya maonyesho anatakiwa kuitisha kikao cha tathmini baada ya kumalizika kwa maonyesho hayo.

"Katika mnyororo wa thamani bado tutawadai maofisa ugani kwa kuwa tunahitaji kuona matokeo ya kazi waliyopewa," alisema Mghwira na kuongeza:

"Changamoto kubwa niliyoiona wakati nikipita katika mabanda, utaalamu wa Tanzania bado haujamkomboa mtaalamu kwa kuwa bado wanatumia elimu ya darasani waliyopata shuleni bado hawajaileta katika uhalisia wa vitendo."

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, Mkuu wa Wilaya ya Arusha Mjini, Gabriel Daqarro, alisema, maonyesho hayo hayatakuwa na maana kama mambo yanayofanyika kila mwaka ni yale yale bila ya kuwapo kwa mabadiliko yoyote.

Daqarro, aliongeza kuwa Mkoa wa Arusha umejizatiti kwa teknolojia waliyoipata katika maonyesho hayo, kuweza kuwasaidia wakulima kuchochea uzalishaji wa bidhaa na mazao ya kilimo, uvuvi na ufugaji.

# Wateule CCM wapita bila kupingwa

**Na Godfrey Mushi,** KILIMANJARO

MADIWANI wateule wawili wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika kata za Makanya Wilaya ya Same na Mahida ya Wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro, wamepita bila kupingwa.

Katibu wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro, Jonathan Mabihya, amewataja waliopita bila kupingwa kabla ya kuingia katika uchaguzi mdogo wa kiti hicho ni Damari Kangaru (Makanya) na Isack Tarimo (Mahida).

"Tuna hakika hiki ni kipimo cha namna ambavyo CCM inakubalika kwa wananchi Mkoa wa Kilimanjaro, huyo Diwani wa Kata ya Makanya, amepatikana kwa sababu aliyekuwapo awali alifariki dunia, lakini diwani wa Mahida, yeye alijiunga na CCM baada ya kuridhishwa na utendaji mzuri wa Rais John Magufuli na chama chetu," ameeleza Mabihya. Ushindi huo wa CCM, unachukuliwa kama kipimo cha siasa za mabadiliko katika mkoa huo, ambao umekuwa ukitikisa kwa siasa za upinzani hasa kutokana na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kuizidi kete mara kadhaa katika baadhi ya maeneo.

Awali, kata hizo zilikuwa zikiongozwa na madiwani wa Chadema walioshinda kiti hicho katika uchaguzi mkuu wa rais, ubunge na madiwani wa mwaka 2015.

Agosti 3, mwaka huu, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), ilitoa taarifa kwa umma kuwa hadi kufikia siku hiyo saa 10:00 jioni ambao ni muda wa mwisho wa kurejesha fomu za uteuzi, wagombea 13 kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM), ndiyo waliokuwa wamerudisha fomu hizo za uteuzi.

NEC ilitangaza kutoa fomu za uteuzi wa wagombea hao kuanzia Julai 29, mwaka huu hadi Agosti 3, iliyopangwa kuwa mwisho wa uteuzi.

Taarifa hiyo iliyosainiwa na Ofisa Habari wa NEC, Hussein Makame, imeeleza bayana kuwa, kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 45 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura Namba 292, Tume hiyo imewateua wagombea 13 kuwa wagombea katika nafasi hiyo.

Uchaguzi mdogo wa madiwani katika kata hizo 13, umepangwa kufanyika nchini kote Agosti 17, mwaka huu.




Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa maonyesho ya 26 ya Nanenane Kanda ya Kaskazini, akimsikiliza Hellen Wakuganda, Meneja wa Pass Kanda ya Kaskazini, wa kwanza kushoto ni Selestine Mofuga, Mkuu wa Wilaya ya Mbulu akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Manyara. **PICHA:ALLAN ISACK**

# Wataka sheria ndogo kudhibiti uchafu

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

BAADHI ya wananchi na wafanyabiashara wa Soko la Sanya Juu lililopo katika Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, wametaka kutungwa kwa sheria ndogo ya kudhibiti utupaji wa taka ovyo ili kukabiliana na kundi la watu wanaotoka na taka majumbani na maeneo ya biashara na kuzitupa sokoni.

Kutokuwapo kwa kanuni au sheria ndogo zinazokazia usimamizi mzuri wa udhibiti taka, ni moja ya sababu ambazo zinaweza kusababisha kuzuka kwa magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu.

Wakizungumzia hali hiyo kwa nyakati tofauti mwishoni mwa wiki, baadhi ya wakazi wa Sanya Juu, wameeleza masikitiko yao kwamba watu wanaokwenda kutupa taka katika soko hilo, hawalengi maeneo maalumu yaliyotengwa kwa ajili hiyo, badala yake huzimwaga taka ovyo ardhini. "Halmashauri inatumia gharama kubwa kuja kuzoa taka, lakini baada ya siku moja au mbili unakuta mrundikano wa taka ukiwa mwingi zaidi, watu wamegeuza soko kuwa jalala kitu ambacho hakikubaliki," alieleza mkazi wa eneo hilo Mwajuma Said.

Naye Zakaria Materu ambaye ni mmoja wa wafanyabiashara, ameeleza kuwa wako baadhi ya wananchi wasio wastaarabu wanakwenda kutupa taka hizo sokoni, wakitokea majumbani nyakati za usiku au katika maeneo yao ya biashara.

"Tunaomba halmashauri yetu ije na sheria ndogo za kudhibiti watu hao ili kuwalinda watumiaji wa soko hilo na wananchi wanaolizunguka, wasipate madhara ya kiafya.

Alipotafutwa Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Sanya Juu, Wema Gasino, kuzungumzia hatua zilizochukuliwa kutokana na malalamiko hayo, alisema soko hilo halina mlinzi na hali hiyo ndiyo inayosababisha watu kutupa taka nyakati za usiku katika soko hilo.

Alisema licha ya kwamba kijiji hicho hakina pesa za kuajiri mgambo wa kukabiliana na uharibifu huo wa mazingira, lakini watajitahidi kuweka ulinzi kulinda soko hilo na atakayebainika sheria itachukua mkondo wake. "Hivi sasa tunaandaa mkutano wa wananchi na tutakaa nao na kujadili suala hili kwa kina na tutaweka utaratibu wao wa kuhifadhi taka katika mashimo ambayo kila mmoja atapaswa kuwa nalo katika nyumba yake, badala ya kuja kuzitupa sokoni," alieleza Gasino.

## Bajeti yakwamisha mradi kukabidhiwa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MRADI wa elimu uliotengewa na serikali zaidi ya Sh. milioni 121.6 katika Kata ya Arusha Chini, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu, umeshindwa kukamilika na kukabidhiwa kwa wakati, baada ya kuibuka changamoto ya kibajeti.

Kwa mujibu wa Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo, Emanuel Mnzava, mradi huo unaotekelezwa katika Shule ya Sekondari Langasani, ulipaswa kukabidhiwa serikalini Julai 30, mwaka huu.

"Ni kweli tuna changamoto ya kibajeti imejitokeza, lakini kimsingi mradi ulipaswa kukamilika kufikia Julai 30, mwaka huu. Sababu iliyosababisha ishindwe kukamilika ni mabadiliko ya hali ya hewa yaliyoambatana na mvua nyingi pamoja na upungufu wa fedha.

"Ingawa kwa sasa mradi uko katika hatua nzuri za umaliziaji, japo bado tunahitaji nguvu za wananchi zaidi. Tunaishukuru serikali kwa fungu ililotoa, lakini bado sisi wananchi wa Moshi hasa Kata ya Arusha Chini ambako mradi upo tunashida katika uchangiaji, tunapaswa tuchangie kwa hali na mali kufanikisha miradi yenye manufaa kwetu ikamilike kwa haraka."

Fedha hizo zimetolewa kupitia mfumo wa serikali wa lipa kwa matokeo (EP4R), baada ya kufanya vizuri katika matokeo ya mtihani wa kidato cha nne mwaka 2018.

Ofisa Elimu ya Sekondari wa Halmashauri hiyo, Juma Tukosa, alisema, "kiasi hicho cha pesa kimepatikana kutokana na Halmashauri ya Moshi kufanya vizuri katika matokeo ya mtihani wa kidato cha nne mwaka 2018, kwa kushika nafasi ya 13 kati ya Halmashauri 195 za Tanzania."

Kwa mujibu wa Tuksa, pamoja na changamoto mbalimbali ikiwamo hali ya hewa, halmashauri hiyo imefanikiwa kusimamia mradi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa mawili, vyoo sita na bweni lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 80.

Tukosa alisema malengo ya ujenzi wa mradi huo wa Sekondari ya Langasani ni kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia pamoja na kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani.

Ujenzi wa majengo hayo unatekelezwa na serikali kwa kutumia mafundi wa kijamii maarufu kama 'force account' na kwamba kwa sasa majengo yote yako katika hatua za maboma na mengine katika kuezekwa.

Mradi huo wa vyumba vya madarasa unahusisha uwekaji wa madawati 80, kila darasa litachukua madawati 40.

# Nipashe Spotika



## UTABIRI UNAVYOIPA MAN CITY UBINGWA WA EPL 2019/2020 UK.16&17



### ISIKUPITE

MAKINDA saba wanaopewa nafasi ya kuwika Ligi Kuu England msimu huu; beki wa kulia Max Aarons, 19, (Norwich City), kiungo Phil Foden, 19, (Man City), kiungo Morgan Gibbs-White, 19, (Wolves), straika Mason Greenwood, 17, (Man United), beki wa kushoto Lloyd Kelly, 20, (Bournemouth), kiungo mshambuliaji Mason Mount, 20, (Chelsea), kiungo Callum Slattery,20, (Southampton).

# MTIFUANO...

Mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford (kulia), akipata upinzani mkali kutoka kwa beki wa AC Milan katika mechi ya kuwania Kombe la Mabingwa wa Kimataifa ambayo ilimalizika kwa United kushinda kwa penalti 5-4 baada ya sare ya mabao 2-2 juzi. **PICHA: MTANDAO**

## SOKA



# MAMBO 6 USIYOYAJUA KUHUSU PEPE

**LONDON,** England

SIKU chache baada ya kutangaza usajili wa Dani Ceballos na William Saliba, Arsenal sasa imekamilisha usajili uliovunja rekodi klabuni hapo wa kumchukua nyota wa Lille OSC, Nicolas Pepe.

**Mchezaji huyu wa kimataifa wa Ivory Coast ameigharimu Arsenal pauni milioni 72 na kuweka rekodi klabuni hapo akiipiku ile ya Pierre-Emerick Aubameyang ambaye alisajiliwa kwa pauni milioni 56. Hata hivyo, Arsenal ada hiyo watailipa kwa mafungu.**

Licha ya kuwa kwenye timu ya Ligue 1 msimu uliopita, pia aliisaidia Lille kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Sasa hapa tunajulisha mambo sita ambayo shabiki wa Arsenal anatakiwa kuyajua kuhusu Pepe kabla ya kuanza kwa msimu mpya wa Ligi Kuu ya England, 2019/20.

**ALIPITWA NA MBAPPE TU**

Licha ya muda wote wa msimu kucheza kama winga wa kulia pale Lille, Pepe alimaliza msimu wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, akishika nafasi ya pili kwa ufungaji bora nyuma ya Kylian Mbappe.

Ukijumlisha pasi za mwisho, Pepe alihusika kwenye mabao mengi zaidi ya ligi kuliko timu nne za mwisho za ligi hiyo, Guingamp, Caen, Dijon (zote zimeshuka daraja) na Amiens.

**ALISHAJIJENGEA JINA**

Pepe pengine wengine wameona kuwa jina lake lilipaa zaidi wakati akiwachezea mabingwa hao mara nne wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Lille, lakini nyota huyo wa Ivory Coast tayari jina lake lilikuwa kubwa kwenye Ligue 1 wakati akicheza pale Angers.

Klabu hiyo imekuwa na utamaduni wa kuzivimbia zile kubwa za ligi, Pepe akiwa na Karl Toko Ekambi walijiimarisha na kuiwezesha Angers kuwa na ushindi wa mara kwa mara kwenye Ligue 1 na haijashuka daraja tangu ilipopanda mwake 2015.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, aliondoka hapo na kujiunga na Lille ambako alipaisha zaidi jina lake na bila shaka, ujio wake pale Arsenal unaweza kumfanya kuwa mmoja wa wachezaji wakubwa zaidi kwenye Ligi Kuu ya England.

**ANA REKODI BORA KULIKO ZAHA**

Kabla Arsenal kukamilisha usajili wa Pepe, awali akili yao ilikuwa ni kutaka kumsajili nyota wa Klabu ya Crystal Palace, Wilfried Zaha ambaye hadi sasa bado anawaniwa na klabu nyingi.

Washika Bunduki hao wakaamua kukunja kona ya ghafla na kuhamishi nguvu zao kwa kumsajili Pepe badala ya kugonga mwaba kwa Zaha ambaye klabu yake ilikuwa ikitaka dau kubwa zaidi.

Lakini uzuri ni kwamba, Pepe ana rekodi nzuri zaidi kwenye mechi za kimataifa kuliko mwenzake Zaha kwa kufunga mabao katika timu ya taifa.

Pepe hadi sasa ana rekodi ya kufunga bao kila baada ya dakika 194 kwa timu yake ya Taifa ya Ivory Coast, wakati Zaha anafunga kila baada ya dakika 282.

**ALIIBULIWA NA MARCELO BIELSA**

Kocha wa sasa wa Klabu ya Leeds United, Marcelo Bielsa ambaye alitumia miezi minne akiinoa Lille OSC kabla ya kuondoka hapo kwenye dimba la Pierre Mauroy, yeye ndiye haswa aliyekuwa na jicho la kuona kipaji cha Pepe na kusamjili kwenye klabu hiyo.

Kocha huyo raia wa Argentina alianza kuangalia kila mchezo wa Ligue 1 ambao Pepe aliichezea Angers kabla ya kumfuata na kushuhudia mwenyewe na baadaye akamsajili kwa euro milioni 10.

**ANAFUNGA KILA DAKIKA 196**

Ana rekodi ya kufunga bao moja katika kila mechi tatu kwenye kipindi chake cha uchezaji hadi sasa. Rekodi ya Pepe ya kufunga mabao kwenye klabu inafanana na ile ya kwenye timu ya taifa, hivyo, Arsenal watakuwa na wakati mzuri zaidi wa kushuhudia mabao yake msimu ujao.

Akiwa anatumia mguu wa kushoto, Pepe amekuwa akipenda zaidi kuanzia winga ya kulia na hilo litafanya kuwa na muunganiko mzuri zaidi na washambuliaji, Alexandre Lacazette na Pierre-Emerick Aubameyang.


**MUIVORY COAST WA TATU KUCHEZA ARSENAL**

Historia ya Arsenal na wachezaji wanaotoka kwenye nchi zinazozungumza Ufaransa wakati wa zama za Arsène Wenger ulikuwa bora zaidi, lakini klabu hiyo hadi sasa imesajili wachezaji watatu wa Ivory Coast kwa muda wao wote kwenye Ligi Kuu ya England.

Beki wa kati, Kolo Touré alijiunga na klabu hiyo mwaka 2002 na alicheza jumla ya mechi 329 katika mashindano yote aliyoichezea Arsenal, akishinda taji la Ligi Kuu, mawili ya FA kabla ya kuhamia Manchester City kwa dau la pauni milioni 16 miaka saba baadaye.

Beki wa pembeni, Emmanuel Eboue alitumia miaka sita kwa miamba hao wa London Kaskazini kabla kutimkia Uturuki mwaka 2011, nafasi yake ikachukuliwa na Gervinho aliyetokea Lille OSC.

**JE, WAJUA?**



HADI sasa barani Ulaya Klabu za Hispania ndizo zinazoongoza kwa kutumia fedha nyingi sokoni majira haya ya joto zikiongozwa na Real Madrid (Euro mil. 303), Atletico Madrid (Euro mil. 243.5) na Barcelona (Euro mil. 237) ya nne ni Juventus ya Italia (Euro mil. 151.5).

# MICHEZO


Ingizo jipya la Yanga kutoka Polisi ya Uganda, Straika Juma Balinya.

# MAJEMBE MAPYA LIGI KUU HAYA HAPA

**Na Adam Fungamwango**

KILICHOBAKI sasa ni kila klabu inasikilizia wachezaji wake watakaopitishwa na Shirikisho la Soka nchini (TFF), kupitia moja ya kamati zake kwa ajili ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2019/20.

**Wale wachezaji watakaoonekana hawana matatizo, watapitishwa moja kwa moja na watakaobainika kuwa na matatizo kwenye usajili itabidi yatatuliwe kwanza kabla ya kuidhinishwa.**

Lakini tayari klabu zote 20 zimeshafanya usajili kwa ajili ya msimu unaokuja wa ligi inayotarajia kuanza Agosti 23. Timu zote 20 ikiwamo ziliopanda daraja, zimeridhika kuwa wachezaji waliowasajili watakidhi au kufanya vile ambavyo kila klabu inataka.

Kila klabu kwenye Ligi Kuu ina malengo yake, zingine kutwaa ubingwa, zingine kuwa ndani ya nne bora na zingine kutafuta pointi tu zitakazozifanya kubaki Ligi Kuu.

Hawa ndiyo wachezaji wapya, au ingizo jipya la wachezaji wa baadhi ya klabu za Ligi Kuu nchini Tanzania kwa ajili ya msimu ujao.

**1. SIMBA**

Imesajili wachezaji kadhaa kama vile Miraji Athumani, Kennedy Juma, na Wabrazil watatu Tairone Santos da Silver, Gerson Fraga Viera, na Wilker Henrique da Silver. Wengine ni Francis Kahata, Deo Kanda, Sahar Shiboub. Ibrahim Ajibu, Gadiel Michael na Benno Kakolanya hawa walisajiliwa kutoka Yanga.

**2. YANGA**

Yenyewe ina maingizo mapya kadhaa ambao ni Patrick Sibomana, Issa Bigirimana, Metacha Mnata, Farouk Shikalo, Selemani Mustapha, Mapinduzi Balama, Lamine Moro, Muharami Issa, Sadney Urkhob, Maybin Kalengo, Juma Balinya, Ally Sonso, Ally Ally. Dakika za mwisho kabla ya usajili kumalizika, ilimshusha straika David Molinga kutoka DR Congo.

**3. AZAM FC**

Msimu huu haikusajili wachezaji wengi sana. Imesajili watano tu ambao ni Richard Djodi, Emmanuel Mvuyekure, Suleiman Ndikumana, Kassim Khamis na Idd Suleiman 'Nado' kutoka Mbeya City.

**4. KMC**

Ikiwa imecheza msimu mmoja tu kwenye Ligi Kuu, imeamua kuja kivingine kwa kusajili wachezaji bora kwa ajili ya michuano ya kimataifa. Imewasainisha kina Salim Aiyee, Ramadhani Kapera, Vitalis Mayanga, kiungo wa zamani wa Azam FC Baptiste Mugiraneza, Kenny Ally, Melly Sivirwa, beki wa zamani wa Simba Besala Bokungu, Abdallah Mfuko, Amos Charles na Mohamed Samatta.

**5. PRISONS**

Inajaribu kufuta makosa yake ya msimu uliopita, hasa mzunguko wa kwanza kabla ya kufufuka mzunguko wa pili. Imewasajili kina Ramadhani Ibata, John Sungura, Prosper Mwangupili, Fred Chudu, Salum Bosco, Jeremiah Kasubi, Dotto Ramadhani, Hamidu Daudi, Samson Baraka, Boniface Chau, Philemon Ramadhani, Adilu Buha na Sijalu Nassib.

**6. NAMUNGO FC**

Ni timu iliyopanda daraja na itacheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza, lakini imeingia kwa mkwara baada ya kunasa nyota wawili kutoka Simba kama Mohamed Ibrahim na Paul Bukaba. Wengine ni Carlos Protas, Nurdin Barora, Steve Nzigamasabo, Abdul Waheed Adesola, Steven Duah, Toure Sie Leopord, Sina Jerome na Bigirimana Blaise.

**7. KAGERA SUGAR**

Baada ya kuponea chupuchupu na kurejea kwenye 'play off' imeamua kumrejesha kipa wao wa zamani Benedict Tinoco na kusajili wachezaji wengine ambao inaona wanafaa kama, Abdul Swamad Kassim, Moussa Hadji, Awesu Awesu, Yusuph Mhilu, Geofrey Mashiuya, Abdallah Seseme, Nassor Kapama, Hassan Isihaka, Evarist Mjwahuki, Zawadi Mauya, Erick Kyaruzi, Erick Mwaijage na Haroun Kheri.

**8. ALLIANCE FC**

Haijafanya usajili mkubwa sana, badala yake ina maingizo matatu tu kama Hussein Kassanga, Danny Manyenye kutoka Biashara United na Erick Muliro.

**9. MBAO FC**

Imeingiza baadhi ya wachezaji ili kujiimarisha kutokana na kutofanya vema msimu uliopita. Wachezaji hao ni Yusuph Athumani, Aboubakar Ngalema, Kauswa Benard, John Mtobesya, Waziri Junior kutoka Biashara United, Mosses Nassor na Grayson Gwalala.

**10. JKT TANZANIA**

Ni moja ya timu ambazo hazijafanya usajili mkubwa sana, badala yake imemrudisha mchezaji wake wa zamani Jabir Aziz kutoka African Lyon, Adam Adam kutoka Prisons, Daniel Lyanga kutoka Azam FC na Adeiyum Seleiman kutoka Coastal Union.

**11. NDANDA FC**

Imesajili wachezaji watatu tu ambao ni Hussein Javu, staika wa zamani wa Yanga, Mtibwa Sugar na msimu uliomalizika alikuwa akiichezea Alliance, kipa wa zamani wa Yanga ambaye msimu uliomalizika alikuwa akidakia Singida United, Ally Mustapha 'Barthez' na Paul Maona.

**12. BIASHARA UNITED**

Baada ya kusumbua kidogo kwenye Ligi Kuu, ikiwa ni msimu mmoja tu baada ya kupanda, imewasajili kina Salum Chuku, James Mwasote, Joseph Kimwaga na Hamisi Batozi.

**13. LIPULI FC**

Timu hii ambayo imeondokewa na baadhi ya wachezaji wake nyota, haijasajili wachezaji wengi, badala yake imewaingiza kina Mwinyi Ahmed Eliasa, Chudu Emmanuel na Aghatony Mkwando.

**14. POLISI TANZANIA**

Maafande wa Polisi ambao watacheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza, hawakuwa nyuma kwenye usajili kwani wamesainisha straika wa zamani wa Klabu za Majimaji, Mbeya City, Njombe Mji na Mwadui, Ditram Nchimbi, wengine ni Mohamed Yusuph, Erick Msagati, Idd Mobi, Hassan Nassor Maulid, Yassin Mustapha, Baraka Majogolo, beki wa zamani wa Yanga Pato Ngonyani, na William Lucian 'Gallas' kutoka Lipuli FC.

**15. SINGIDA UNITED**

Ni moja kati ya klabu ambazo hazijafanya usajili wa kutisha, badala yake maingizo mapya ni wachezaji Ismail Mohamed, Paschal Ndaga, Pius Luchangula, Said Mtikila kutoka African Lyon iliyoshuka daraja, Said Mkwazu na Herman Frimpong.

**16. MTIBWA SUGAR**

Ilishasema tangu mapema kuwa itapandisha wachezaji wake wengi wa kikosi cha pili kilichotwaa ubingwa wa vijana chini ya maiaka 20. Ndiyo maana imesajili wachezaji wachache tu kina Awadh Salum, Said Mohamed 'Nduda' akitokea Ndanda FC, kiungo mzoefu nchini Abdulhalim Humud na Mohamed Abdallah.

**17. MWADUI FC**

Iliponea chupuchupu na kurejea Ligi Kuu kwenye mechi ya 'play off'. Imeamua kufanya usajili ambao yenyewe inaamini utaiweka mahali salama kama Mussa Runi, Augustine Samson, Melikiad Mazela, Venance Ludovic kutoka Kagera Sugar, Mukhsin Ulaya, Marick Kapolo, Abuu Kambi, Fadhil Masoud, Mussa Nampaka, Hashim Mussa, Omari Daga, Emmanuel Memba na Rogers Gabriel kutoka Mtibwa Sugar.

NJE YA UWANJA



## Maguire atua Manchester

BEKI wa Leicester, Harry Maguire amenaswa na kamera akitoka hotelini katikati ya mji wa Manchester wakati huu akikaribia kukamilisha dili la kujiunga na Manchester United.

Kisha Maguire akasafiri kuelekea Carrington kukutana na kocha Ole Gunnar Solskjaer na wachezaji wengine wa kikosi cha United, ambao jana mchana waliivaa Blackburn kwenye mechi ya kirafiki.



# UTABIRI UNAVYOIPA MAN CITY UBINGWA WA EPL 2019/2020



**LONDON,** Egland

MANCHESTEER City itashinda tena taji la Ligi Kuu mbele ya Liverpool, Tottenham itacheza na Manchester United kwenye fainali ya Kombe la Europa na Newcastle itashuka daraja.

**Huu ni utabiri uliotolewa na BT Sport baada ya kukusanya taarifa za kisayansi za klabu zote zinazoshiriki Ligi Kuu msimu huu na kuangalia takwimu zilizopita na hali ya saa ya vikosi vyake.**

Kampuni hiyo ya utangazaji ambayo inafanya utabiri wa mara kwa mara kabla ya kuanza kwa msimu wa Ligi Kuu ya England, hivyo ndivyo ilivyoutabiria msimu huu unaonza wiki ijayo pale utakapofikia kilele chake Mei 17, 2020.

Katika takwimu zake hizo kampuni hiyo imeangalia mechi zote 380 za Ligi Kuu ya England za msimu huu unaokuja, matokeo yake na namna mambo yatakavyokuwa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya pamoja na Kombe la Ligi ya Europa kwa klabu za England.

Pep Guardiola kocha wa Man City atakuwa katika msimu wake wa tatu wa kulitwaa taji la Ligi Kuu, na kuipiku Liverpool kwa pointi sita. Tottenham inatabiriwa kwamba itamaliza nafasi ya tatu, huku Chelsea itabakia kwenye nne bora.

Arsenal na Manchester United hazitakuwapo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, zikiwa nyuma ya Chelsea, ambayo pengine kocha wake, Frank Lampard atahisi amekuwa na mwanzo mzuri kwenye mwaka wake wa kwanza, kwani atakuwa kileleni mwa msimamo wakati wa Krismasi kabla ya kuanguka.

BT Sports ambayo inafanya utabiri huo kisayansi kwa kukusanya data za kila klabu, inaonyesha kuwa baada ya mechi 38 za Ligi Kuu Newcastle itaungana na Norwich City iliyopanda na Sheffield United kushuka daraja na kwenda kucheza kule kwenye ligi ya Championship. Aston Villa itapambana na kumaliza nafasi ya 15.

Kwa michuano ya Ulaya, hakuna timu itakayoweza kuvuka robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini kutakuwa na mafanikio makubwa kwa upande wa Ligi ya Europa kwa mara nyingine tena.

Manchester United, itaifunga Arsenal kutinga fainali ya Kombe la Europa itakayopigwa pale Gdansk na itakutana na Tottenham - ambayo itakuwa imeondolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya makundi na mwishowe kocha, Mauricio Pochettino atalibeba taji hilo.

BT Sports imezipanga timu jinsi zitakavyomaliza kwenye Ligi Kuu msimu huu mpya...

**ARSENAL – 5**

Timu hii ya Kocha Unai Emery itakosa tena kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya, ikimaliza nyuma ya Chelsea na itafungwa mechi zake tatu kati ya tano za ufunguzi wa ligi hiyo.

Washika Bunduki hao watatolewa kwenye Ligi ya Europa na Manchester United ambayo itacheza na Tottenham na kufungwa.

Arsenal haitamaliza ligi ikiwa kwenye nne bora, licha ya mabao yanayotabiriwa kutoka kwa washambuliaji wake, Pierre-Emerick Aubameyang (mabao 23) na Alexandre Lacazette (mabao 16) hayatawasaidia chochote.

**CHELSEA – 4**

Frank Lampard atapoteza mchezo wake wa kwanza kama kocha pale Old Trafford, lakini itakuwa moja ya timu ambayo itacheza kwa muda mrefu bila kufungwa, hadi pale itakapokutana na kichapo kutoka kwa Everton Desemba 7.

Chelsea itapita kwenye hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na wataitoa Borussia Dortmund kwenye hatua ya mtoano wa timu 16 bora, kabla ya Eden Hazard na Real Madrid kuwaondosha hatua ya robo fainali.

Blues hao watamaliza nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya England.

**LIVERPOOL – 2**

Ukame wa taji la Ligi Kuu kwa Liverpool utaingia muongo wa tatu kwani watalikosa tena taji hilo kwa kupitwa pointi sita na watakaokuwa mabingwa Manchester City.

Wakati wakiwa na kumbukumbu nzuri kwenye Ligi ya Mabingwa msimu uliopita kwa kulitwaa taji hilo, msimu huu Lionel Messi atang'ara na kuisaidia Barcelona kuwatupa nje Wekundu hao katika robo fainali ya michuano hiyo.

Kikosi hicho cha kocha, Jurgen Klopp kitapata ushindi wake wa kwanza pale Old Trafford msimu huu na Mohamed Salah atatwaa kwa mara ya tatu tuzo ya mfungaji bora wa Ligi Kuu kwa kumzidi Harry Kane kwani atafikisha mabao 29.

**MANCHESTER CITY – 1**

Man City msimu huu utakuwa mzuri tena kwa upande wao.

Hata hivyo, watatolewa na Real Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya mtoano wa timu 16.

Sergio Aguero atakuwa mchezaji wa kwanza kwenye Ligi Kuu ya England kufunga mabao zaidi ya 20 kwa misimu sita mfululizo na atawaburuza Wayne Rooney na Alan Shearer kwa ufungaji wa wakati wote wa ligi hiyo.

**MANCHESTER UNITED – 6**

United itamaliza nafasi ya sita wakati ambapo kocha Ole Gunnar Solskjaer atakaposhindwa kuwapandisha kileleni mwa msimamo. Watapoteza mechi 12 msimu huu ikiwa ni mara ya pili kwenye zama zake za Ligi Kuu.

Watakuwa na nafuu kwenye Ligi ya Europa, lakini mwisho wake hautakuwa mzuri, kwani watafungwa kwenye fainali. Arsenal watatolewa na United kuelekea kwenye fainali itakayopigwa kule Gdansk... ambako watapoteza kwa bao 1-0 dhidi ya Tottenham.

**NEWCASTLE – 18**

Msimu mwingine mbaya kwao, kwani Newcastle watamaliza ligi kwa kushuka daraja. Watashuka daraja kwa tofauti ya mabao.

**TOTTENHAM – 3**

Spurs itamaliza ligi katika nafasi ya tatu kwenye msimamo, lakini watakuwa na taji la Ligi ya Europa mkononi. Vijana hao wa Mauricio Pochettino watakuwa wakati wa kufurahia mafanikio yao.

Watatolewa na Bayern Munich kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kupokea vipigo mara mbili, lakini wataibukia kwenye Ligi ya Europa na kulitwaa taji hilo, kwa kuifunga United kwenye fainali.

## Nukuu

"Nadhani kila kocha anapenda kuchezesha makinda kutoka katika akademi yake. Swali ni bidhaa gani kutoka katika akademi? Unawezaje kufanya nao na kuboresha. Chelsea ni klabu ya kipekee katika hilo. Ninaweza kutoa mfano: Chelsea inahitaji beki wa kati- Kurt Zouma! Uhitaji kununua, uhitaji kutumia fedha. Unahitaji mshambuliaji kinda - **Tammy Abraham! Ni wakwako," Jose Mourinho akitoa darasa kwa Kocha wa Chelsea, Frank Lampard.**



"Ni hali ambayo kila mmoja anajua, bado klabu inamhitaji na mimi nimezungumza naye kumshauri abakie hapa, namtaka yeye abakie na sisi. Anajua tayari kile ninachofikiria kuhusu hali hii, nimezungumza naye kiungwana na kwa heshima kabisa kumtaka abakie na sisi," **mshambuliaji wa PSG, Kylian Mbappe akizungumzia kuhusu ushawishi wake kwa Neymar kutaka abaki klabuni hapo.**



"Sipo hapa kwa ajili ya kuzungumza kuhusu tetesi yoyote ama fununu kuhusu wachezaji wa timu nyingine, lakini bila shaka, tunafanyia kazi kuhusu mmoja ama wawili, kama nilivyosema hapo kabla, ninatumai tunaweza kutangaza sura mpya ama mbili," **Kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer, akikataa kuweka wazi kuhusu tetesi za kumsajili mshambuliaji wa Juventus, Paulo Dybala.**



# MIAKA 10 SIMBA DAY ITAKAVYOKUWA KESHO




Straika tegemeo wa Simba, Meddie Kagere, akikabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa moja ya mabeki wa Asante Kotoko ya Ghana kwenye mechi ya Simba Day mwaka jana katika Uwanja wa Taifa, timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: MAKTABA**

**Na Adam Fungamwango**

HITIMISHO la Tamasha la miaka 10 ya Siku ya Simba ('Simba Day') litafanyika kesho Jumanne kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, timu hiyo itakapopambana na Power Dynamos ya nchini Zambia.

**Huu ni mwaka wa 10 mfululizo kwa Simba kufanya tamasha hilo ambalo hulitumia kutambulisha wachezaji wake wa zamani, wapya, jezi mpya huku likisindikizwa na mambo mbalimbali kama vile burudani kutoka kwa wasanii mbalimbali.**

Klabu hiyo imetangaza kauli mbiu ya mwaka huu ambayo inaitwa "Iga Ufe This is next level 10 years Anniversary Simba Week".

Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Crescentius Magori amesema mwaka huu utakuwa na utofauti mkubwa kuliko miaka yote kutokana na maandalizi yaliyofanyika.

Kitu ambacho kinaendelea kufanyika ni wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kufanya shughuli za kijamii kama ilivyo kawaida yao miaka yote tangu lilipoanzishwa mwaka 2009, ambapo hutembelea sehemu mbalimbali hospitalini, shuleni, sokoni na makazi ya watoto yatima kwa ajili ya kutoa misaada mbalimbali.

Wachezaji wa klabu hiyo ambao wamerejea kutoka Afrika Kusini Julai 31, Ijumaa walitembelea kampuni shiriki, kabla ya Jumamosi kutembelea wagonjwa kwenye Hospitali ya Ocean Road ambayo inatibu wagonjwa wenye matatizo ya kansa.

Mbali na ratiba ndefu, pia klabu ya Simba ilitarajiwa kuzindua kadi mpya za kielektroniki kwa ajili ya kununua tiketi moja kwa moja ikiwa na punguzo.

Hii itakuwa ni mechi ya 11 ya Simba kwenye tamasha lake. Katika mechi 10 ambazo imecheza, imeshinda tano, sare mbili na kufungwa mechi tatu.

Tofauti na msimu uliopita, Simba msimu huu haitokuwa na mchezaji yeyote aliyekuwapo kwenye tamasha la kwanza mwaka 2009. Mchezaji pekee aliyekuwapo msimu uliopita na alikuwa kwenye tamasha hilo mwaka wa kwanza ni Emmanuel Okwi aliyefunga bao la kusawazisha mwaka jana dhidi ya Asante Kotoko.

Yafuatayo ni matokeo ya mechi zote 1o za Simba kwenye tamasha hilo...

**1. SIMBA 1-0 SC VILLA (2009)**

Hii ilikuwa ni mechi ya kwanza kabisa ya Tamasha la Simba Day ikichezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam dhidi ya SC Villa kutoka Uganda.

Katika mechi hiyo, Simba ilishinda bao 1-0. Bao la washindi lilifungwa dakika ya nane na kiungo Mkenya aliyekuwa ndiyo kwanza amesajiliwa, Hirally Echessa.

**2. SIMBA 0-0 EXPRESS (2010)**

Ikiwa chini ya kocha Patrick Phiri, na wachezaji kama Ally Mustapha 'Barthez', Emmanuel Okwi, Joseph Owino, Mohamed Banka, Patrick Ochan, Rashid Gumbo, Amri Kiemba, Mussa Hassan Mgosi, Jerry Santo, Simba ilishindwa kupata ushindi mwaka wa pili wa Simba Day ilipolazimishwa sare dhidi ya Express ya nchini Uganda. Mechi hii pia ilichezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

**3. SIMBA 0-1 VICTORY (2011)**

Simba ilikiona cha moto kwenye mwaka wa tatu kwa msimu wake wa Simba Day, ilipofungwa kwa mara ya kwanza. Ilichapwa bao 1-0 dhidi ya Victory FC nayo ikitoka nchini Uganda.

Kwa mara ya kwanza na mpaka sasa haijawahi kutokea, mechi hiyo ya Simba Day ilichezwa nje ya Dares Salaam, kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid mjini Arusha. Lilikuwa ni bao la mkwaju wa penalti likifungwa dakika ya 70 na Patrick Sembuya.

**4. SIMBA 1-3 NAIROBI CITY STARS (2012)**

Kwa mara ya kwanza Simba ikacheza mechi yake ya Simba Day kwenye Uwanja wa Taifa mwaka 2012 dhidi ya Nairobi City Stars kutoka nchini Kenya. Ukawa ni msimu wa nne wa Simba Day. Ikiwa ni mara yao ya kwanza kucheza Taifa, Simba ilikubali kipigo cha mabao 3-1 kutoka kwa wageni wao. Dancun Owiti, Bruno Okullu na Boniface Onyango walipeleka maangamizi, kila mmoja akifunga bao, huku la kufutia machozi likifungwa na Mzambia Felix Sunzu.

**5. SIMBA 4-1 SC VILLA (2013)**

Baada ya kupoteza miaka miwili mfululizo, Simba ilirudi kwa kishindo kwenye Simba Day ya mwaka 2013, ilipoisasambua SC Villa ya Uganda mabao 4-1 kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Yalikuwa ni mabao ya Betram Mombeki aliyefunga mawili, Jonas Mkude na William Lucian 'Gallas', yaliyotosha kabisa kuwaangamiza wageni hao.

**6. SIMBA 0-3 ZESCO (2014)**

Simba ilikiona cha mtemakuni Simba Day ya mwaka 2013, ilipochapwa mabao 3-0 dhidi ya Zesco kutoka Zambia na kusababisha kupoteza kibarua kwa aliyekuwa kocha wake mkuu, Zdravko Lugarusic.

Walioifanya sherehe ya Simba Day kugeuka msiba ni Jackson Mwanza, Mayban Mwamba na Claotus Chama ambaye kwa sasa yupo Simba.

**7. SIMBA 1-0 SC VILLA (2015)**

Mwaka 2015, Simba iliingia kwenye mwaka wa saba wa tamasha la Simba Day kwa kucheza na SC Villa kutoka Uganda. Katika mechi hiyo Simba ilishinda bao 1-0. Bao pekee lililowafanya mashabiki wa Simba mwaka huo kuondoka na furaha uwanjani baada ya kipigo cha mabao 3-0 mwaka uliopita, lilifungwa dakika moja tu kabla ya mechi kumalizika na Awadh Juma.

**8. SIMBA 4-0 AFC LEOPARDS (2016)**

Simba ilitoa kipigo kitakatifu mbele ya AFC Leopards ya Kenya mwaka 2016 kwenye mechi ya mwaka wa nane wa Simba Day.

Mabao ya Simba yalifungwa na Ibrahim Ajibu ambaye alifunga mawili, Mrundi Laudit Mavugo akifunga bao moja, na Shiza Kichuya aliyekuwa akiichezea kwa mara ya kwanza akitokea Mtibwa Sugar.

**9. SIMBA 1-0 RAYON SPORT (2017)**

Pasi nzuri ya Emmanuel Okwi, ilimkuta Mohamed Ibrahim kwenye nafasi nzuri dakika ya 15 na kuujaza wavuni, ikawa ni bao pekee kwenye mechi hiyo iliyofanya Simba kuondoka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Rayon Sport kutoka nchini Rwanda.

**10. SIMBA 1-1 ASANTE KOTOKO (2018)**

Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Simba kuleta timu kutoka Afrika Magharibi kwenye tamasha lake hilo.

Timu kongwe Afrika, Asante Kotoko ilitua nchini na kuilazimisha Simba sare ya bao 1-1 kwenye Uwanja wa Taifa. Obed Owussu aliifungia Kotoko bao, kabla ya Okwi kusawazisha.

NDANI YA 18



HADI sasa Aston Villa ndiyo timu pekee iliyotumia kiasi kikubwa zaidi cha fedha (euro milioni 125) kwenye usajili katika Klabu za Ligi Kuu England majira haya ya joto.

## SOKA

# KLABU 5 ZILIZOFANYA KUFURU YA USAJILI



**LONDON,** England

MSIMU mpya wa Ligi Kuu wa soka la Ulaya unatarajia kuanza ndani ya siku chache zijazo. Klabu barani humo zimetumia fedha nyingi katika kuimarisha vikosi vyao ili ziweze kufanya kweli.

**Dirisha la sasa la usajili tayari limeshuhudia usajili wa wachezaji kwa kutumia kiasi kikubwa cha fedha. Klabu chache zimechimba zaidi mifuko yao kwa ajili ya kupata nyota wakali kwenye timu zao.**

Tayari kumekuwa na usajili wa wachezaji watatu ambao kila mmoja ametumia euro milioni 100 au zaidi.

Hapa tunaangalia klabu tano ambazo zimetumia kiasi kikubwa zaidi cha fedha katika dirisha hili la usajili hadi sasa.

**5. ASTON VILLA – EURO MIL. 125**

Aston Villa imerudi kwenye Ligi Kuu ya England baada ya kuikosa kwa miaka mitatu. Aston Villa ilishuka daraja mwaka 2016. Lakini sasa wamiliki wa klabu hiyo hawataki tena kurudia makosa chini ya kocha, Dean Smith. Wametumia kiasi cha karibia euro milioni 125 kwa kusajili wachezaji wapya.

Wesley Moraes alianza kusajiliwa kwa euro milioni 25 na ikawachukua wengine, Tyrone Mings na Douglas Luiz ili kuimarisha timu yao.

Aston Villa imetumia kiasi kikubwa zaidi cha fedha kwenye usajili kuzishinda Manchester City na Manchester United.

**4. JUVENTUS – EURO MIL. 151.5**

Juventus imejaribu kila mbinu kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kipindi cha misimu michache iliyopita. Walimsajili Cristiano Ronaldo mwaka jana ikiwa ni sehemu ya jitihada zao za kutaka kulishinda taji hilo. Msimu huu Juventus imewasajili Aaron Ramsey, Rabiot na nahodha wao wa zamani, Buffon kwa usajili huru.

Usajili mkubwa walioufanya kipindi hiki cha majira ya joto ni Matthijs de Ligt, kwani imemsajili kwa euro milioni 85.5. Higuain amemfuata Sarri kutoka Chelsea baada ya kuitumikia kwa mkopo. Juventus imetumia jumla ya euro milioni 151.5 katika kipindi hiki cha usajili wa majira ya joto.

**3. BARCELONA – EURO MIL. 237**

Mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Hispania walionekana kupungukiwa sehemu msimu uliopita. Walishinda taji hilo la La-Liga bila tabu yoyote mbele ya wapinzani wao Madrid. Lakini nje ya La Liga walikuwa na kibarua kigumu. Uongozi wao wa mabao matatu kwenye mchezo wa kwanza wa nusu fainali dhidi ya Liverpool uliisha pale kwenye dimba la Anfield katika mchezo wa pili. Pia wakajikuta wanaangukia pua kwenye fainali ya Kombe la Copa Del Rey dhidi ya Valencia.

Barcelona imetumia jumla ya euro milioni 237 kusajili wachezji wapya kipindi hiki cha majira ya joto. Barcelona ilimsajili Antoine Griezman kwa euro milioni 120. Frenkie de Jong alijiunga na Barcelona akitokea Ajax kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 75.

Usajili wa Griezman ulisukumwa zaidi na Messi, kwa sasa Barcelona inatafuta beki wa kati ambaye atadumu na kikosi hicho kwa muda mrefu.

**2. ATLETICO MADRID – EURO MIL. 243.5**

Atletico Madrid ilimshangaza kila mtu wakati ilipomsajili Felix kwa euro milioni 126.

Kikosi hicho cha kocha, Diego Simeone kina ndoto kubwa ya kufanya vizuri kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na lile la Europa bila kusahau Ligi Kuu ya Hispania.

Hadi sasa Athletico imetumia kiasi cha euro milioni 243.5 kwa ajili ya kuimarisha kikosi chake kipindi hiki cha majira ya joto. Pia wamewasajili wachezaji kama Trippier na Llorente ili kujiimarisha zaidi.

**1. REAL MADRID – EURO MIL. 303**

Real Madrid ilitabiriwa kwamba itaingia sokoni kwa nguvu kubwa kabla hata msimu uliopita haujamalizika.

Kurudi kwa Zidane kwenye tanuru hilo kumewafanya wachezaji wengi kuvutiwa na kujiunga na Madrid.

Real Madrid hadi sasa imetumia kiasi cha euro milioni 303. Hazard ametumia kiasi cha euro milioni 100. Wachezaji wengine walioijiunga na Hazard pale Santiago Bernabeu ni Jovic, Mendy na Rodrigo.

Real Madrid sasa ni timu yenye wachezaji nyota wengi. Ramos na Marcelo wakiongoza safu ya ulinzi, Modric kiungo, Benzema akifanya yake mbele.

**NDANI YA 18**



TANGU mwaka 2016, Harry Maguire amehusika moja kwa moja katika kuchangia mabao 13 kwa Leicester, akifunga mara saba na kutoa pasi za mwisho sita. Kwa upande wa mabeki anayemzidi ni Sergio Ramos (17) pekee wa Real Madrid.

Nipashe Spotika



MANCHESTEER City itashinda tena taji la Ligi Kuu mbele ya Liverpool, Tottenham itacheza na Manchester United kwenye fainali ya Kombe la Europa na Newcastle itashuka daraja.

Uk. 16&17

# WATOTO WANAOPITA NJIA ZA BABA ZAO UWANJANI



JUSTIN KLUIVERT

**MILAN,** Italia

WAMEAMUA kwenda njia moja ambayo baba zao wamepita kwenye soka na wao wakiwa na ndoto ya kufikia mafanikio kama yao.

Ni watoto wa wachezaji soka wa zamani ambao kwa nyakati zao walitamba wakiwa na klabu mbalimbali pamoja na timu zao za taifa.

Makala haya yanakuchambulia watoto ambao wameingia kwenye soka wakifuata nyazo za baba zao.

**DANIEL MALDINI (17) - AC MILAN**

Paolo Maldini ni gwiji wa Klabu ya AC Milan na klabu hiyo ilijulikana kama 'klabu ya mtu mmoja'.

Beki huyo alicheza mechi 902 ikiwamo mechi 647 katika Ligi Kuu ya Italia, Serie A, na kushinda mataji matano ya Ulaya na saba ya Ligi ya Mabingwa Ulaya akicheza kwa kipindi cha miaka 25.

Na sasa mtoto wake Daniel pia anafuata nyayo za baba yake na babu yake, Cesare ambaye aliichezea Milan mara 300 katika miaka ya 1950-60 kabla ya kuwa kocha wa klabu hiyo.

Daniel alianza kuichezea rasmi AC Milan wiki iliyopita katika mechi ya kirafiki dhidi ya Bayern Munich.

Jezi namba tatu iliofanywa kuwa maarufu na baba yake, Paolo ilistaafishwa wakati Maldini alipostaafu, lakini ameiruhusu klabu hiyo kuitumia tena iwapo mwanawe ataichezea klabu hiyo.

**JUSTIN KLUIVERT (20) - ROMA**

Patrick Kluivert aliichezea miamba ya Uholanzi Ajax, AC Milan na Barcelona wakati wa kipindi chake akifunga jumla ya mabao 205.

Katika mechi 79 alizoichezea Uholanzi alifunga mabao 40 na kuwasaidia katika nusu fainali ya Kombe la Dunia mwaka 1998 kule Ufaransa.

Alishinda mataji machache, ikiwamo lile la Ligi Kuu ya Uholanzi, Eredivise, mara mbili, La Liga na lile la Ligi ya Mabingwa Ulaya ambapo alifunga bao la ushindi wakati alipokuwa na umri wa miaka 18.

Na sasa mwanawe Justina ameanza kucheza, kwani alianza kuichezea Ajax na kufunga bao lake la kwanza miaka kumi na siku moja tangu babaye kufunga bao lake la mwisho.

Pia alishinda medali ya nafasi ya pili ya Ulaya katika kipindi cha mwaka 2016/17. Kisha babaye, alielekea Italia baada ya kusajiliwa na Klabu ya AS Roma mwaka 2018.

Ingawa anajaribu kuingia katika kikosi cha kwanza, alikuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi wa Roma kufunga bao katika Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita baada ya kufunga dhidi ya Viktoria Plzen, likiwa bao lake la kwanza la klabu hiyo.

Anavalia jezi namba 34 kumkumbuka mchezaji mwenza na baba yake, Abdelhak Nouri ambaye alipatwa na mshutuko wa moyo mwaka 2017 na hivyo basi kustaafu katika soka ndiye alikuwa akivaa jezi hiyo.

**TIMOTHY WEAH (19) - LILLE**

Baba yake alikuwa Mwafrika wa kwanza kushinda taji la Ballon d'Or. Kwa sasa ndiye rais wa Taifa la Liberia.

Goerge Weah alijitengenezea jina lake nchini Ufaransa wakati aliposajiliwa na Arsene Wenger kutoka Monaco kwa dau la pauni 12,000.

Alikuwa mchezaji maarufu duniani na nchini Italia na kuisaidia AC Milan kushinda mataji mawili ya ligi, Ballon D'Or na kufunga bao maarufu ambapo alitamba na mpira kutoka upande mmoja wa uwanja kuwapiga chenga karibia wachezaji wote wa klabu ya Hellas Verona kabla ya kufunga.

Licha ya kufunga mabao 200, Weah alistaafu na kuingia kwenye siasa ambazo zimefanya kuwa rais wa Liberia mwaka 2018 na baadaye kushiriki mechi ya kirafiki dhidi ya Nigeria wakati akiwa na umri wa miaka 51.

Mwanawe Timothy sasa ameanza kucheza soka katika klabu ya New York Red Bull ya Marekani, mchezaji huyo wa Marekani amefuata nyanyo za baba yake akitia saini mkataba wake wa kwanza na Klabu ya PSG.

Ni wazi kwamba ingekuwa vigumu kubeba jina lake, huku timu hiyo ikiwa na wachezaji maarufu kama vile Neymar, Kylian Mbappe na Edinson Cavani.

Gianluigi Buffon alianza kuichezea Parma mwaka 1995, akicheza bila kufungwa na Klabu ya George Weah ya AC Milan.

Na miaka 23 baadaye, Buffon alicheza kama mchezaji mwenza wa mwanawe akiwa PSG.

**IAN HAGI (20) - GENK**

Ian Hagi alifunga mabao mawili dhidi ya Romania na kufika nusu fainali ya Kombe la Mabingwa Ulaya Julai mwaka huu akichezea timu ya wachezaji wasiozidi umri wa miaka 21.

Baba yake, Gheorghe Hagi ni mchezaji nyota aliyeichezea Real Madrid, Barcelona na Galatasaray - alitajwa kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani katika miaka 1980 na 1990.

Kiungo huyo mshambuliaji alicheza mara 125 na ametajwa kuwa mchezaji bora wa wakati wote nchini Romania.

Na sasa mwanawe Ian alianza kucheza soka katika taasisi ilioanzishwa na babaye. Ingawa uhamisho wake kutoka Romania hadi Fiorentina haukufanya kazi, Ian alijipatia matumaini katika Klabu ya Viitorul kabla ya kuelekea Klabu ya Genk nchini Ubelgiji - klabu ambayo iliwatoa Kevin De Bryune, Divock Origi na Thibaut Courtois.

Baba yake alimfanya nahodha wa Klabu ya Viitorul Constanta akiwa na umri wa miaka 20.

**LUCA ZIDANE (21) - RACING CLUB SANTANDER**

Zinedine Zidane ni mmoja ya wachezaji bora zaidi duniani, aliyeshinda kila kitu ambacho mchezaji na kocha anatakiwa kushinda.

Hadi sasa Lucas amepanda ngazi katika Klabu ya Real Madrid, akifuzu kuchezea timu ya wachezaji wa ziada na hadi katika kikosi cha kwanza cha timu, huku baba yake akiwa kocha.

Akilinganishwa na wachezaji wengine wa magwiji wa soka waliopita, yeye tofauti na baba yake anacheza nafasi ya golikipa.

Ni mchezaji wa pili kati ya wanne ambao wametoka katika taasisi ya Real Madrid.

**USILOLIJUA**

Nicolas Pepe ni mchezaji pekee katika ligi tano bora barani Ulaya aliyepiga mashuti 100 na zaidi langoni na kuzawadiwa faulo zaidi ya 100 katika msimu wa 2018/19.





HABARI MBEYA

# Ma-RC, DC wapewa somo la viwanda

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, (Tamisemi), Mwita Waitara, amewataka wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya zote za Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kuhamasisha na kusimamia uanzishwaji wa viwanda vikubwa, vidogo na vya kati ambavyo vitajikita katika usindikaji wa mazao.

Waitara alitoa agizo hilo juzi wakati akifungua rasmi Maonyesho ya Wakulima (Nanenane) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambayo kwa kanda hiyo yenye mikoa saba yanafanyika kwenye Viwanja vya John Mwakangale jijini hapa.

"Wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya hakikisheni mnahamasisha na kusimamia uanzishwaji wa viwanda kwenye maeneo yenu, ili kuhakikisha mazao ya wakulima yanaongezewa thamani kwa lengo la kufanya yauzwe kwenye soko la ndani na nje ya nchi kwa bei nzuri itakayowanufaisha," alisema Waitara.

Alisema lengo la serikali lilikuwa ni kuona kila mkoa unaanzisha viwanda vidogo vidogo visivyopungua 100, lengo ambalo limevukwa, lakini bado uhitaji wa viwanda hasa vya kusindika mazao ya wakulima ni mkubwa.

Waitara alisema viwanda vikubwa, vya kati na vidogo zaidi ya 4,000 nchi nzima ambavyo vinaendelea kufanya kazi nzuri ya kuinua uchumi wa nchi.

Alisema mbali na viwanda hivyo kuongeza thamani ya mazao ya wakulima, pia vitasaidia kupunguza tatizo la ajira kwa vijana ambao wataajiriwa katika viwanda hivyo.

Aidha, Waitara aliwataka wataalamu wa kilimo kuhakikisha mbinu na teknolojia zinazoonekana kwenye maonyesho ya Nanenane inahamishiwa kwenye mashamba ya wakulima vijijini ili ziweze kuleta tija badala ya kuishia kwenye mabanda ya maonyesho.

Akizungumza kwa niaba ya wakuu wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema viongozi wa mikoa hiyo wameungana na kuamua kufanya kazi kwa pamoja kuhakikisha wakulima wananufaika na kilimo kwa kupata mbinu na teknolojia kupitia maonyesho hayo ya Nanenane.

"Sisi viongozi wa mikoa hii ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, kuanzia wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, wakurugenzi na viongozi wengine tumeamua kwa dhati kuunganisha nguvu zetu kuwasaidia wakulima ili wanufaike kwa kupata mbinu na teknolojia za kilimo cha kisasa kupitia maonyesho haya ya Nanenane," alisema Chalamila.

Alisema kuwa kazi kubwa iliyopo kuhamasisha wakulima kuachana na kilimo cha kizamani na kuanza kulima kwa kutumia mbinu na teknolojia za kisasa ili waweze kupata tija na kunufaika na kilimo chao.

Kabla ya kufungua rasmi maonyesho ya kilimo ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Waitara alitembelea mabanda ya mbalimbali ya maonyesho na kufurahishwa na teknolojia za kisasa zinazoonyeshwa katika mabanda hayo.

Hata hivyo Waitara alifurahishwa zaidi na hatua ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kutumia kusanyiko hilo kuwasaidia wananchi hasa wakulima kusajili laini zao za simu kwa mfumo mpya wa kielektroniki kwa kutumia alama za vidole kirahisi.

Meneja wa TCRA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, John Asajile, alisema wameamua kuweka mabanda ya makampuni yote ya mitandao ya simu pamoja ndani ya viwanja hivyo vya maonyesho, ili kuwawezesha wananchi wakiwamo wakulima kusajili laini zao kirahisi bila usumbufu.

Alisema pamoja na kuwapo mabanda ya makampuni ya mitandao yote ya simu, pia lipo banda la Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) ili kuwasaidia wananchi wasio kuwa na vitambulisho kujisajili na wale waliokwisha kujisajili wapewe namba zao za vitambulisho ili wazitumie kusajili laini zao kielektroniki.



Wananchi kutoka Wilaya ya Longindo mkoani Arusha, pamoja na wanafunzi wa Shule ya Msingi ya Soweto wakipokea mafunzo kutoka kwa wataalamu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) walipotembelea banda la mamlaka hiyo, katika maonyesho ya 26 ya Nanenane Kanda ya Kaskazini. **PICHA: ALLAN ISACK**

# Busokelo wamlilia JPM malipo ya chai

**Na Nebart Msokwa,** BUSEKELO

WAKULIMA wa chai katika Halmashauri ya Busokelo Wilaya ya Rungwe, wameiomba serikali kuingilia kati suala la bei ya chai wakidai wanunuzi wanawapunja kwa kununua zao hilo kwa bei ndogo isiyoendana na gharama za uzalishaji.

Walitoa kilio hicho, mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano wa hadhara na Mbunge wa Jimbo la Busokelo, Fred Mwakibete, uliofanyika katika Kijiji cha Kandete ambapo walimwomba mbunge huyo kuwasaidia kupigania bei ya zao hilo.

Anna Kabola, alisema kwa sasa wanauza zao hilo, Sh. 315 kwa kilo moja ambayo ni bei ndogo ikilinganishwa na gharama wanazotumia kwenye uzalishaji na hivyo akaiomba serikali kuwasaidia kuongeza bei.

"Tunakuomba utusaidie kufikisha kilio chetu kwa Rais Magufuli atusaidie bei ya chai iongezeke ili tuweze kunufaika kama wengine wanavyonufaika, tusaidiwe angalau iongezeke shilingi 15 kwenye bei ya sasa," alisema Anna.

Irene Mwambonje, alisema bei iliyopo kwa sasa haiwanufaishi chochote zaidi ya kuwa bei inayowanyonya wakulima kwa maelezo kuwa kutunza zao hilo inahitaji fedha nyingi.

Alisema baadhi ya mambo yanayosababisha bei ya zao hilo kuwa na bei ndogo ni ubovu wa miundombinu ya barabara ambayo inawafanya wanunuzi wanunuwe kwa bei ndogo ili kuepuka kuingia hasara.

Aliomba barabara za wilaya hiyo kuboreshwa ili kuwavutia wawekezaji na wanunuzi wa zao hilo kushawishika kununua mazao yao kwa bei kubwa zaidi ya ile iliyopo kwa sasa.

"Barabara zetu ni mbovu sana na ndio maana mazao yetu ikiwamo chai kuwa na bei ndogo, lakini endapo barabara hizi zitaboreshwa kuna uwezekano wa bei za mazao yetu kupanda," alisema Irene.

Akijibu kero hiyo, Mwakibete alikiri bei ya zao hilo kuwa ndogo, lakini akasisitiza kuwa hata hivyo serikali imefanya kazi kubwa ya kuboresha bei ya zao hilo.

Alisema wakati serikali ya awamu ya tano inaingia madarakani bei ya zao hilo ilikuwa Sh. 231 kwa kilo moja, lakini ikapanda mpaka 315 ya sasa kutokana na serikali kupitia Waziri Mkuu, Kasim Majaliwa kupigania. Hata hivyo, alisema ataendelea kushirikiana na viongozi wengine katika kuhakikisha bei ya zao hilo inapanda na kulingana na maeneo mengine ukiwamo Mkoa wa Njombe ambako alisema bei ya zao hilo ni kubwa kutokana na uwepo wa wawekezaji wakubwa.

"Mara ya kwanza alipokuja Waziri Mkuu tulimwomba atusaidie kupambana na changamoto hii na kweli alitusaidia, lakini bado tunatakiwa kupambana kuboresha bei, nalichukua hili na kulipeleka kwa wahusika ikiwemo bodi ya mazao mchanganyiko," alisema Mwakibete.

# Watendaji wakosesha ruzuku vijiji

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

VIJIJI 21 vya Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, havikupata fedha za ruzuku ya maendeleo katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2018/2019 kutokana na maofisa watendaji wa vijiji hivyo kutowasilisha akaunti za vijiji vyao kwenye halmashauri.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Kivuma Msangi, alipokuwa anawasilisha taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo.

Alisema hali hiyo imesababisha wenyeviti na wananchi wa vijiji hivyo kushindwa kutekeleza mipango ya maendeleo waliyojiwekea kwa mwaka husika.

Alisema wilaya hiyo ina vijiji 109, lakini katika mwaka huo wa fedha vijiji 88 viliwasilisha akaunti za vijiji vyao pamoja na taarifa zingine na vikapewa fedha isipokuwa hivyo vijiji 21.

"Kwa sasa tumewaandikia barua wale wote ambao hawakuhuisha taarifa zao ili wajieleze na tukibaini kuwa sababu zao hazina mashiko tutawachukulia hatua kali za kiutumishi ikiwa ni pamoja na kuandikiwa barua za onyo," alisema Msangi.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya, Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Ezekiel Kilemile, alisema ili shughuli za maendeleo ziweze kutekelezwa kuanzia ngazi za vijiji ni lazima watumishi wa serikali wafuate sheria.

Alisema maofisa watendaji wa vijiji wanatakiwa kufanya mikutano mikuu ya mwaka na wananchi ili kuainisha changamoto zilizopo kabla hazijakwamisha maendeleo ya wananchi wa vijiji vyao kama ilivyotokea kwa vijiji 21.

"Haiwezekani wenyeviti wa vijiji mpo, madiwani mpo na watendaji wa vijiji na kata wapo halafu haya yanatokea, hii yote ni kwa sababu ya kutofanyika kwa mikutano, sasa kila mmoja achukuwe hatua kwa nafasi yake," alisema Kilemile.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Francis Mtega, aliwataka watumishi wa halmashauri hiyo, kufanya kazi kwa uadilifu wakizingatia miongozo iliyopo ili kuepusha changamoto ambazo zinaepukika.





# 'Unyonyeshaji usiofaa chanzo vifo vya watoto'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa taratibu zisizofaa za unyonyeshaji wa maziwa ya mama zinachangiCEa kwa kiasi kikubwa vifo vya watoto nchini.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki na Ofisa Lishe Mwandamizi kutoka Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC), Neema Joshua, katika semina ya waandishi wa habari alipokuwa akiwasilisha mada kuhusu umuhimu wa unyonyeshaji maziwa ya mama.

Alisema wamama wamekuwa wavivu kunyonyesha watoto ipasavyo na kufuata taratibu, hivyo kusababisha vifo na magonjwa kwa watoto.

"Wamama wa siku hizi wamekuwa wavivu sana kunyonyesha na hata wanaponyonyesha basi hawafuati zile taratibu zinazofaa kama vile miezi sita ya mwanzo kunyonya maziwa ya mama pekee bila kupewa vyakula vingine," alisema.

Aidha, alisema wengine wamekuwa wakiacha kuwanyonyesha watoto na kuwapatia maziwa ya kopo hali inayowaweka hatarini kutokana na kukosa virutubisho.

"Wamama wanatakiwa kutambua kuwa maziwa ya mwanzo baada ya mama kujifungua yana uwezo wa kumkinga mtoto na magonjwa, kutowajibika ipasavyo kwenye unyonyeshaji ni miongoni mwa sababu za kudumaa watoto," alisema.

Alisisitiza kuwa kuna kila sababu ya kulinda unyonyeshaji ili kuzuia vifo zaidi ya 820,000 kwa mwaka vya watoto, takribani nusu ya magonjwa ya kuhara na theluthi moja ya magonjwa ya njia ya hewa.

Alisema vifo na magonjwa yanaweza kuzuilika kwa kunyonyesha watoto maziwa ya mama ipasavyo pindi wanapozaliwa na baada ya miezi sita ya mwanzo.

Mtaalamu huyo alifafanua vifo 25 hutokea kwa kila vichanga 1,000 waliozaliwa hai kwa watoto wachanga, huku vifo vya watoto chini ya mwaka mmoja vikiwa ni vifo 43 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai.

Vile vile, alisema vifo vya watoto chini ya miaka mitano ni vifo 67 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai nchini.

"Kama tukiweza kufanya uboreshaji huo tunaweza kuzuia vifo zaidi ya 820,000 kwa mwaka vya watoto na magonjwa ya kuhara na ya njia ya hewa," alisema.

Pamoja na hayo, alisema unyonyeshaji wa muda mrefu (yaani hadi miaka miwili au zaidi) unasaidia kupunguza unene uliozidi na magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama vile kisukari kwa watoto.




Mkurugenzi wa Idara ya Hazina na Masoko ya Fedha wa Benki ya NBC, Peter Nalitolela, akizungumza katika kongamano la siku moja kuhusu mitaji ya fedha na usimamizi wa hatari zinazoweza kutokea katika miamala ya kifedha kwa wadau kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Benki Kuu ya Tanzania, Tanesco, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kongamano hilo lilifanyika jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madiwani wapewa angalizo la uchaguzi

**Na Mwandishi wetu,** BAHI

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, wametakiwa kujiandaa kuhakikisha uchaguzi wa serikali za mitaa unafanyika kwa amani na kujiepusha na migogoro isiyokuwa na tija.

Uchaguzi huo unatarajiwa kufanyika Novemba mwaka huu nchini. Hayo yalielezwa na Ofisa Serikali za Mitaa mkoani humo, Emmanuel Kuboja, wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani cha robo ya nne ya mwaka wa fedha 2018/2019. Kuboja alisema kuwa madiwani wana wajibu wa kuhakikisha wanadumisha amani na utulivu kwenye maeneo yao na kutokuwa chanzo cha migogoro itakayoathiri uchaguzi huo.

"Sehemu yoyote yenye utulivu lazima hata maendeleo yake huwa ni makubwa hivyo niwaombe waheshimiwa madiwani kuwa na utulivu tunapoelekea kipindi hiki cha maandalizi ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa dumisheni amani," alisema Kuboja. Awali, akijibu hoja za baadhi ya madiwani kwenye kikao hicho, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Danford Chisomi, alisema kuwa halmashauri itaendelea kutoa mchango wake kadri itakavyohitajika ili kuleta maendeleo kwa wananchi. Chisomi alisema ni lazima kuongeza nguvu kwenye kusimamia miradi mbalimbali iliyopo ndani ya halmashauri.

Aliwataka madiwani kuendelea kushikamana ili kuhakikisha miradi yote iliyoanzishwa inaenda vizuri na inakamilika kulingana na thamani ya fedha iliyotolewa.

Mwenyekiti huyo alisema halmashauri imeanza kutoa zawadi kwa viongozi wanaosimamia kazi zao vizuri ili kuhamasisha usimamizi wa miradi uwe na tija kwa wananchi.

"Tumeanza kwa watendaji wa kata na vijiji ambao wameendelea kufanya vizuri na sasa ni wakuu wa idara mbalimbali," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Dk. Fatuma Mganga, aliwaagiza madiwani kuendelea kuwaelimisha wananchi juu ya ushiriki wao kwenye miradi ya maendeleo.

# Mamlaka yahimiza wananchi usajili laini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Mawasiliano nchini (TCRA), imewataka wananchi kutumia maonyesho ya Nanenane kwa ajili ya kusajili laini zao kwa alama za vidole ili kudhibiti utapeli unaofanywa na watu mbalimbali kwa njia ya mitandao.

Wito huo ulitolewa juzi na Meneja wa TCRA Kanda ya Kati, Antonio Manyanda, alipokuwa akizungumzia usajili huo, kwenye viwanja vya Nanenane jijini hapa.

Manyanda alisema wakazi wa Dodoma wanapaswa kutumia fursa hiyo ili kusajili laini zao kwa kuwa itasaidia kuepusha utapeli unaofanywa na baadhi ya watu kwa njia ya mtandao.

"Naomba wakazi wa Dodoma tumieni maonyesho haya kukamilisha usajili wenu kwa sababu ni jambo muhimu kutokana na kwamba vitu vyako vitakuwa salama tofauti na mwanzo," alisema Manyanda.

Alifafanua zaidi ya kuwa wao kama TCRA wanawahimiza wananchi kufanya zoezi hilo kwa sababu kipindi hiki cha maonyesho huduma zote zinapatikana katika viwanja hivyo na kuongeza kuwa ni vema jamii kujitokeza kwa wingi kwa ajili ya kukamilisha usajili.

Alisema TCRA ipo mstari wa mbele kutoa elimu kwa jamii kuhusiana madhara ya kutosajili laini za simu kwa alama za vidole kwa kutumia vitambulisho vya Taifa ili jamii iwe salama.

Alisema mamlaka hiyo inaendelea na msako wa matapeli wanaowarubuni watu ya kuwa wanasajili laini wakati si kweli.

Aliitaka jamii kutokubali kudanganywa na wakala ambao hawatambiliki na badala yake wanatakiwa kwenda katika mamlaka husika na kwa mawakala ambao wanatambulika ili wasajiliwe kihalali.

"Naomba jamii iwe makini wanaposajili laini zao, wahakikishe wanakwenda katika vituo ambavyo vinatambulika," alisema Manyanda.

Alisema TCRA itaendelea kufanya msako katika maeneo mbalimbali ili kubaini wanaowadanganya wananchi na kuwachukulia hatua kali za kisheria.



# Dk. Shein atahadharisha ufundishaji taaluma ya dini

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, amewataka wahadhiri na wataalamu wa Vyuo Vikuu vya Kiislamu kuhakikisha mitaala wanayoitumia kufundishia taaluma ya dini haitaleta athari kwa wanafunzi ndani ya mfumo wa mabadiliko ya sayansi na teknolojia yaliyopo hivi sasa duniani.

Alisema Uislamu haukatazi waumini wake kujifunza elimu ya dunia, lakini kinachopaswa kuzingatiwa zaidi na wahadhiri na wataalamu hao ni kufuata sheria na miongozo ya uislamu kwa vile dini yenyewe tayari imeshakamilika katika nyanja zote kwa ajili ya kutekelezwa na wanadamu.

Dk. Shein alisema hayo katika hotuba yake iliyosomwa kwa niaba yake na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, wakati akifungua mkutano wa tatu wa kimataifa wa vyuo vikuu vya Kiislamu uliofanyika Zanzibar.

Alisema mwanafunzi wa chuo kikuu anapaswa kujengewa mazingira sahihi ya mfumo wa kisasa yatakayomwezesha kushawishika na kujifunza masomo ya Sayansi, Ufundi na Ustawi wa Jamii ili atakapomaliza awe kiungo na maendeleo katika umma unaomzunguka.

Dk. Shein alisema vyuo vya Kiislamu katika kipindi cha utandawazi vina kazi kubwa kwa wataalamu wake kufanya utafiti wa kina katika masuala ya ustawi na sayansi utakaowawezesha kupata suluhisho la changamoto zinazowakabili waumini wa dini hiyo.

"Vyuo vikuu vya Kiislamu vichukuwe jukumu la kuieneza elimu ya dini sambamba na kujenga hoja za kujibu itikadi zisizo sahili zinazotolewa dhidi ya dini hiyo," alisema Dk. Shein.

Pia alieleza kwamba ufundishaji wa sasa ni vyema ukazingatia matumizi ya tekonojia ya habari na mawasiliano ambayo inamwharakisha mwanafunzi kujifunza kwa haraka. Alisema teknolojia hiyo ya kisasa ni rahisi kwa vile mwanafunzi anayeamua kutumia mfumo huo ana uwezo wa kutafuta kumbukumbu za vitabu anavyovihitaji katika mafunzo yake zikiwamo pia tafiti za wahadhiri tofauti.

Naye Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Abdulrahman Al – Simait, Profesa Amran Rasli, alisema Zanzibar imepata heshima kubwa kutokana na kufanyika kwa mkutano huo wa tatu wa vyuo vikuu vya Kiislamu duniani ukitanguliwa na uliofanyika Morogoro na Uganda.

"Hii ni fursa ya pekee kwa wahadhiri na wataalamu wa Zanzibar kuitumia nafasi ya uwapo wa mkutano huo kuchota fikra kutokana na kuwasilishwa kwa mada na utafiti 50 kutoka kwa wenzao wa mataifa shiriki katika mkutano huu," alisema.

Naye Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, alisema hadhara hiyo itasaidia kuleta ushirikiano baina ya wahadhiri na wasomi mbalimbali.

# Shughuli za kijamii zaathiri usafi wa mazingira

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KUONGEZEKA kwa shughuli za kijamii katika Manispaa ya Mji wa Zanzibar kumesababisha uzalishaji wa taka kwa wingi na kuathiri mazingira.

Akizungumza katika mkutano wa kuongeza mwamko kuhusu kanuni za usimamizi wa taka, Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mihayo Juma Nhunga, amesema Zanzibar inatoa wastani wa taka tani 2,38,712 kwa mwaka mmoja sawa na tani 663 za taka kwa maeneo yote ya Zanzibar.

Alisema Manispaa ya Zanzibar zinatoa taka tani 132,515 kwa mwaka, sawa na tani 368 kwa siku na uwezo wa halmashauri na manispaa ni kuchukua taka wastani wa asilimia 50.

Alizitaka Manispaa na Halmashauri zote za Zanzibar kuhakikisha zinaimarisha usimamizi bora wa taka na sheria, kanuni na taratibu zilizopo ili wananchi wanaondokana na tabia ya kutupa taka ovyo.

Alisema kufanya hivyo kutaisaidia jamii kujiepusha na kujilinda na maradhi ya mlipuko na kuweka mandhari nzuri ya mji kwa faida endelevu ya kiuchumi, kijamii, kimazingira na utalii ambao ndio nguzo kuu ya uchumi wa nchi.

Alisema upo utamaduni kwa baadhi ya wananchi kutupa taka ovyo katika maeneo ya wazi, bustani na katika misingi ya kupitishia maji ya mvua hasa wakati wa mvua hali inayoweza kusababisha maradhi ya mlipuko na maafa.

Naibu Mihayo, alieleza kuwa serikali inaendelea na juhudi kubwa za kuimarisha miundombinu ya usimamizi wa taka pamoja na kutayarisha mkakati wa Zanzibar wa usimamizi wa taka hizo, na kujenga dampo la kisasa katika eneo la Kibele.

Alisema kumalizika kwa dampo hilo kutawezesha kutenganisha taka ngumu na kuwa chachu ya mafanikio ya Wazanzibari kutotupa taka ovyo na kuziangamiza ili zisiweze kusambaa.

Akizungumzia mafanikio yaliyopatikana katika mradi wa majaribio wa usimamizi wa taka katika Shehia ya Shaurimoyo unaotekelezwa na kituo cha Sayansi na Mazingira cha New Delhi cha nchini India, alisema mradi huo umewezesha nyumba 626 za shehia hiyo kutenganisha taka na kutengeneza mbolea ambayo imekuwa ikutumika kuimarisha shughuli za kilimo na kuhifadhi mazingira.

"Mradi huu umekuwa na faida kubwa sana ndani ya jamaii hiyo hasa kwa kuwa na sehemu ya kuongeza kipato kwa wahusika wa miradi, huku wakiweka mazingira safi ndani ya shehia na manispaa ya mjini," alisema Mihayo.

Vile vile, alisema ni matumaini yake kuwa manispaa nyingine zinajifunza kwenye mradi huo na kuanzisha miradi kama hiyo kwa lengo la kutunza mazingira na kuiweka miji katika hali ya usafi kwa usalama wa wananchi.

Naye Balozi mdogo wa India Zanzibar, Shri Raha, alisema utunzaji mzuri wa mazingira utaondoa athari mbalimbali ikiwamo milipuko ya magonjwa pamoja na utupaji taka ovyo ambao huharibu mazingira.



Ofisa kutoka Jeshi la Polisi Dawati la Jinsia, ASP Fatuma Mtalimbo, akitoa mada kwa wafanyakazi wa kampuni ya Bia Tanzania (TBL) wakati wa mafunzo kuhusiana na kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia kwenye jamii, yaliyofanyika jijini Dar Es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CUF Z'bar wamtuhumu Maalim Seif

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Wananchi (CUF) Zanzibar kimesema utaratibu wa kugawana nafasi za wakuu wa mikoa, wilaya na masheha kuanza kupigiwa kura na wananchi umekwama kutokana na ubinafsi wa aliyekuwa Katibu Mkuu wa CUF, Maalim Seif Sharif Hamad.

Hayo yameleezwa na mwasisi wa chama hicho na Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini, Mussa Haji Kombo, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari chimbuko la maridhiano na malengo ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Alisema mpango huo ulikuwa unajadiliwa katika mazungumzo ya Maalim Seif na marais wastaafu wa Zanzibar baada ya kufutwa matokeo ya uchaguzi mkuu, mwaka 2015 kabla ya kurudiwa Machi mwaka 2016.

"Unakataa kuingia katika Baraza la Mapinduzi kama Makamu wa Kwanza Rais na serikali ikiundwa kwa sababu tupo 50 kwa 50, mawaziri tulikuwa tugawane nusu kwa nusu," alisema Mussa.

Alisema katika mashauriano walikubaliana wakuu wa mikoa kati ya watano CUF kuchukua nafasi mbili, wakuu wa wilaya watano kati ya 11 pamoja na masheha kuanza kuchaguliwa kwa kupigiwa kura na wananchi badala ya kuteuliwa na wakuu wa mikoa.

Hata hivyo, alisema mpango huo ulivurugika baada ya Maalim Seif kuamua kujitoa katika mazungumzo kutokana na kutetea maslahi binafsi kabla ya kususia uchaguzi wa marudio na kusababisha kukwama kuundwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mussa, alisema CCM baada ya kuona hali mbaya ya matokeo ya uchaguzi mwaka 2015 ilianza kupanga mikakati ya kuigawa CUF kwa madhumuni ya kuzorotesha ushindi katika uchaguzi wa mwaka 2020.

Alieleza kutokana na sintofahamu iliojitokeza kura za CUF zitalazimika kugawika nyingine kubakia CUF na nyingine kwenda chama cha ACT-Wazalendo na kuwapa nafasi CCM kuendelea kushinda visiwani Zanzibar.

Alisema madhumuni ya kufikiwa maridhiano baina ya CCM na CUF, yalikuwa kudumisha amani na umoja wa kitaifa kwa wananchi wa Zanzibar baada ya kutokea mpasuko wa kisiasa na watu kupoteza maisha na wengine kupata ulemavu wa maisha kwa sababu za kisiasa.

Hata hivyo, alisema Rais mstaafu Amani Abeid Karume na Rais Dk. Ali Mohamed Shein, wanapaswa kupongezwa kutokana na kazi kubwa waliyofanya ya kusimamia mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa baada ya kufanyika marekebisho ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Kwa upande wake Makamu Mwenyekiti wa CUF, Abbas Juma Muhunzi, alisema wananchi wa Zanzibar lazima wafahamu maridhiano yaliyozaa muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni ya CCM na CUF na sio Rais mstaafu Amani Abeid Karume na Maalim Seif Sharif Hamad.

Alisema wakati maridhiano yanaelekea kutimiza miaka kumi tangu kufikiwa, wananchi wanapaswa kuendelea kulinda amani na umoja wa kitaifa pamoja na kujiepusha na siasa za chuki ikiwamo kususiana shughuli za kijamii kama maziko na harusi kwa sababu za kisiasa.

# Tasaf yaahidi kuendelea kuzisaidia kaya maskini

**Na Restuta Damian,**
BUKOBA

SERIKALI imesema imepanga mfumo mpya wenye kuendelea kusaidia kaya maskini nchini ambao utaingia katika mpango wa kunusuru kaya maskini Tasaf 3 sehemu ya pili, kwa kaya zenye sifa za kutokuwa na uwezo wa kufanya kazi kujipatia kipato.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), Dk. Mary Mwanjelwa, wakati akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Kabale Kangaiza Kata Ijuganyondo Manispaa ya Bukoba, Kakindo Kata ya Katoma, Burugo Kata Nyakato wilayani Bukoba mkoani Kagera akiwa katika ukaguzi wa shughuli za TASAF 3 awamu ya kwanza.

Dk. Mwanjelwa alisema katika kipindi cha awamu ya pili mpango utaingiza kaya ambazo hazikuingia kipindi kilichopita ambapo mkoa wa Kagera una kaya 251 zilikuwa nje ya mpango ambazo zitaingia awamu ya pili kwa malipo yatakayoanza kutolewa mwezi huu.

Alisema fedha za uhawilishaji zitaendelea kutolewa kwa walengwa ambao hawawezi kufanya kazi za kujishughulisha na uzalishaji wa kujipatia kipato kama wazee, watoto na wagonjwa, na kuwa vijiji vya Kabale Kangaiza, Kakindo Bujugo tayari kiasi cha Sh. milioni 229 zimeshapelekwa ili kutekeleza mpango wa kaya maskini sehemu ya pili.

"Serikali kwa kujali wananchi wake hasa kaya maskini sana, imeendelea kusaidia wananchi kwa kuboresha maisha yao wilayani Bukoba, Rais Magufuli ametoa kiasi cha Sh. milioni 46 kwa Kijiji cha Kabale Kangaiza, shilingi milioni 94 kijiji cha Rukindo Sh. milioni 89 kwa Kijiji cha Burugo," alisema Dk. Mwanjelwa.

Aidha, alisema katika mpango wa awamu ya pili serikali imefikia Halmashauri 40 kati ya 187 nchini, na kwamba malengo ni kueneza mpango huu kufika maeneo yote nchini kuwainua na kuboreshea maisha ya wananchi.

Aliendelea kusema kuwa fedha inayotolewa inalenga kumsaidia mnufaika kuwa na makazi, maradhi, kupata uhakika wa chakula kwa kuzingatia changamoto zinazobainishwa na wataalamu wanakusanya taarifa kwa kaya husika.

"Pesa inayotolewa ipelekwe kwenye maendeleo na sio kutumia kwenye pombe, kuolea mke mwingine, na matokeo yake kushindwa kuboresha maisha na kujikwamua pamoja kushindwa kutamani kuwa na nyumba ya tofali na bati kufuga, kufanya ujasiriamali, kinamama kuanzisha vikoba hayo ndiyo maendeleo," alisema Mwanjelwa.

Alisema ili kuondoa changamoto, mfumo utakaotumika kwa sehemu ya pili ni kufikia kaya husika, na kuchukua taarifa kamili za kielektroniki ili kuondoa udanganyifu ambao unaweza kuleta uchonganishi kati ya wananchi na viongozi.

Awali akisoma taarifa ya utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini Tasaf 3 awamu ya kwanza, Mtendaji wa Kijiji cha Burugo Kata Nyakato wilayani Bukoba, Anderson Seki, alisema mpango huo ulianza mwaka 2015 na kunufaisha walengwa 119 kati ya 130 waliotambuliwa.

Seki alisema walengwa hao walikuwa katika mazingira magumu yenye kushindwa kupata msaada wa tiba wala chakula cha uhakika na kuishi kwa kutegemea misaada kwa ndugu na jamaa.

Seki alisema baada ya wanufaika hao kupatiwa fedha, walipewa elimu ya uanzishaji wa miradi ya kuboresha makazi, kilimo, ufugaji, kuendeleza watoto kupata elimu na kujiunga na mfuko wa bima ya afya kupitia fedha zinazotolewa na serikali.



Naibu Waziri wa Kilimo, Omari Mgumba (katikati), akizungumza na mmoja kati ya wajasiriamali wadogo waliowezeshwa na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) pindi alipotembelea maonyesho ya Nanenane kitaifa yanayoendelea kwenye viwanja vya Nyakabindi mkoani Simiyu, (kushoto) ni Meneja Uhusiano wa NBC, William Kallaghe (kulia) ni Meneja wa Kanda ya Ziwa, Japhet Mazumira. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Lindi, Mtwara watakiwa kutumia mabonde kwa uzalishaji chakula

**NaSaid Hamdani, LINDI**

WANANCHI wa mikoa ya Mtwara na Lindi wamesisitizwa kuyatumia maeneo ya mabonde yaliyopo kwenye maeneo yao kulima aina mbalimbali ya mazao, ukiwamo mpunga na mahindi ili kupunguza tatizo la kuagiza mchele na unga kutoka sehemu nyingine.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mtwara, Dk. Jilly Maleko, alitoa msisitizo huo alipokuwa akizungumza na wanahabari viwanja vya maonyesho ya wakulima Nanenane katika viwanja vya Ngongo Mjini Lindi.

Amesema Lindi na Mtwara ni mikoa iliyojaliwa kuwa na mabonde mazuri yanayofaa kwa kilimo, lakini bado wananchi hawajayatumia kikamilifu kuzalisha mazao ya chakula.

"Mtwara na Lindi tunayo mabonde mazuri yanayofaa kwa aina mbalimbali ya kilimo, lakini hatujayatumia kikamilifu," alisema Dk. Maleko.

Aliwakumbusha Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Miji mkoani Mtwara kuhakikisha wanatekeleza mkataba walioingia na Mkuu wa Mkoa huo kuwahamasisha wananchi kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.

Maonyesho hayo yalifunguliwa rasmi juzi na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-Tamisemi), Selemani Jafo.

# Wakala mbolea Makambako ashinda droo ya kwenda Harare

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Makambako Agro-Chemicals, ambao ni wakala wa kusambaza mbolea ya Yara mkoani Njombe, imeshinda tiketi ya kwenda Harare, Zimbabwe kwa mapumziko.

Kampuni hiyo imeshinda droo ijulikanayo kama 'YARA Lucky Draw' iliyochezwa jijini Dar es Salaam baada ya mkutano wa wadau wa kilimo unaoitishwa na Yara Tanzania kila mwaka.

Akitangaza matokeo hayo yaliyoshirikisha kampuni sita za uwakala na ambazo zilifanya vizuri na kusambaza mbolea tani nyingi kwa wakulima, Meneja Biashara wa YARA Tanzania, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania, John Meshack, alisema jana jijini Dar es Salaam.

Mmiliki wa Makambako Agro-Chemicals, Bernadetha Sanga na mumewe, Georger Kabelege, watakwenda na kupumzika Harare kwa siku mbili kwa gharama ya Yara.

"Gharama zote zitalipwa na YARA kwa siku zote watakazo kuwa nchini Zimbabwe. Tunajali na kuheshimu kazi inayofanywa na mawakala wetu," alisema

Meshack na kuwaomba kufanya kazi kwa kujituma na uaminifu. Sanga aliishukuru kampuni ya YARA kwa kuwajali na kuwathamini mawakala wa usambazaji wa mbolea na hata kila mwaka kutoa bonasi kwa kampuni kumi zinazofanya vizuri.

Makambako Agro-chemical ni miongoni mwa kampuni 10 zilizofanya vizuri na kupewa bonasi.

Mkurugenzi wa Yara Tanzania, Winstone Odhiambo, alisema mkutano na mawakala na wadau mbalimbali wa kilimo ni sehemu ya utamaduni wa kampuni yao wa kukutana na kubadilisha uzoefu na mikakati kabla ya msimu wa kilimo kuanza.

"Tuna wathamini sana wakulima na hivyo wanapopata mbolea kabla ya msimu ni faraja kwetu kwani inaashiria mavuno mazuri. Tumekutana na mawakala wote tumezungumza na kusaini mikataba," alisema.

Odhiambo aliwataka mawakala kuendelea kutoa elimu kwa wakulima juu ya namna bora ya matumizi ya mbolea na kuhamasisha upimaji wa afya ya udongo.

YARA Tanzania ni moja ya wadau muhimu katika sekta ya kilimo katika kuchagiza mageuzi ya kilimo kwa kutoa elimu juu ya matumizi bora ya mbolea na kupima afya ya udongo ili kufanikisha azma ya serikali ya awamu ya tano ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025.

## HABARI KIMATAIFA

## Kenya kuuza mafuta nje

**NAIROBI,** Kenya

KENYA inajiandaa kuuza nje mafuta ghafi baada ya kupata mnunuzi wa mapipa 200,000 yaliyo na thamani ya dola milioni 12 za Marekani.

Hii itakuwa shehena ya kwanza ya mafuta ghafi yatakayouzwa nje ifikapo kipindi cha robo ya mwisho ya mwaka 2019.

Kwa mujibu wa taarifa ya kampuni ya Tullow, mafuta hayo tayari yamesha safirishwa hadi mjini Mombasa.

Tullow Oil, iliyo na visima vya mafuta katika Jimbo la Turkana, imekuwa ikisafirisha mapipa 600 ya mafuta kwa siku hadi eneo la pwani ya Kenya, lakini tangu Mei imeongeza idadi hiyo na kufikia mapipa 2,000.

Hata hivyo, maelezo ya kampuni iliyoingia ubia na Kenya hayajakuwa bayana. Kenya iligundua hifadhi ya mafuta mnamo mwaka 2012 kwenye Bonde la Lokichar na inakisiwa kiasi ya mapipa milioni 560 huenda yakapatikana baada ya eneo hilo kuchimbwa kikamilifu. **DW**

## EU yatoa tamko kuhusu mapigano Libya

**TRIPOL,** Libya

UMOJA wa Ulaya (EU) umetoa tena wito kwa pande zinazokinzana nchini Libya kusitisha mapigano na kudumisha amani, huku ukionyesha uungwaji wake mkono kwa Mwakilishi Maalum wa Umoja wa Mataifa nchini humo, anayeshtumiwa na Waziri Mkuu wa Libya, Fayez al-Sarraj.

"Mkuu wa sera za kigeni za EU, Federic Mogherini, akizungumza na waandishi wa habari alisema EU na wanachama wake wanakaribisha pendekezo la kusitishwa kwa mapigano lililotolewa na Mwakilishi Maalum wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Ghassan Salamé, kwenye hafla ya Eid al-Adha (Sikukuu ya kuchinja wanyama halali), ambayo ni hatua muhimu katika mwelekeo huo,

"Umoja wa Ulaya unaunga mkono kikamilifu ombi la Mwakilishi Maalum kwa hatua tatu zinazolenga kufufua mazungumzo ya kisiasa na hasa kutekeleza mpango huo wa kusitishwa kwa mapigano," alisema Mogherini na kuongeza:

"Mashambulio ya kinyama kwenye maeneo yenye wakazi wengi yanaweza kuwa na uhalifu wa kivita na wale wanaokiuka sheria za kimataifa za binadamu wanapaswa kufikishwa mbele ya mahakama na wawajibishwe."

Umoja wa Ulaya na wanachama wake wametoa wito kwa wanachama wote wa UN kuheshimu vikwazo vya silaha dhidi ya Libya na umezitaka pande zote husika katika mzozo nchini Libya kujitenga, hadharani na magaidi pamoja na wahalifu wanaoshiriki vita na wale wanaoshtumiwa kutekeleza uhalifu wa kivita.

Wengine ni wale waliowekwa kwenye orodha ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. **RFI**

# Watu 20 wauawa katika shambulizi la risasi

**WASHINGTON,** Marekani

WATU 20 waliuawa na wengine zaidi ya 26 kujeruhiwa kwenye shambulizi la risasi lililotokea katika mji wa El Paso, Texas nchini Marekani, Jumamosi asubuhi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Jeshi la Polisi, mtuhumiwa huyo aliyekuwa amejihami na bunduki alianza kuwashambulia kiholela wateja waliokuwa kwenye eneo la kuegesha magari nje ya duka la Celo Vista Walmart, kabla ya kuingia ndani, ambako kulikuwa na zaidi ya wateja 1,000 na wafanyakazi kadhaa na kuanza kuwashambulia.

Mshukiwa huyo, ambaye alikamatwa na polisi muda mfupi baadaye, alitambulishwa kama Patrick Crusius, mwenye umri wa miaka 21 na anayetokea mjini Allen, Texas.

**Idara ya Upelelezi ya FBI ilitangaza Jumamosi usiku kwamba imefungua uchunguzi wa shambulizi hilo na utafanyika kwa misingi ya ugaidi wa ndani ya nchi.**

Rais wa Marekani, Donald Trump alisema kupitia ujumbe wake wa mtandao wa kijamii wa Twitter kwamba analaani kitendo hicho.

"Hakuna sababu au kisingizio chochote cha kuwaua raia wasio na hatia. Melania na mimi tunatuma rambirambi za dhati na maombi kwa niaba ya watu wa Jimbo la Texas," aliandika Rais Trump kwenye ukurasa wake huo wa habari.

Mgombea urais, Beto O'Rouke, ambaye ni mwenyeji wa eneo ambalo tukio lilitokea aliwaeleza waandishi wa habari kuwa shambulizi hilo huenda limechochewa na kauli za Rais Trump ambazo, alisema, ni za kibaguzi na chuki.

Shirika la Habari la CNN liliripoti kwamba taarifa za chuki na ubaguzi zilizopatikana kwenye mitandao ya kijamii zilikuwa zinachunguzwa kubaini kama ziliandikwa na mshukiwa huyo.

Idara ya Upelelezi ya FBI ilitangaza Jumamosi usiku kwamba imefungua uchunguzi wa shambulizi hilo na utafanyika kwa misingi ya ugaidi wa ndani ya nchi.

Shambulizi hilo lilitokea ikiwa imepita wiki moja baada ya lingine, ambapo watu watatu, wakiwamo watoto wawili, kutokea kwenye Tamasha la Chakula na Muziki mjini Gilroy, California waliuawa.

El Paso ni mji ulio karibu na mpaka wa Marekani na Mexico na wakazi wengi ni wa asili ya Mexico. **VOA**




Mpaka kati ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Rwanda ambao ulifungwa Agosti Mosi kwa uamuzi wa serikali ya Kigali wakati mji wa Goma unaendelea kukabiliwa na mlipuko wa ugonjwa wa ebola. **PICHA: REUTERS**

# Ebola yaendelea kuzua hofu nchi jirani

**KIGALI,** Rwanda

SERIKALI ya Rwanda ilifunga mpaka wake na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kwa muda wa saa kadhaa Alhamisi wiki hii, siku moja baada ya mgonjwa wa tatu aliyeambukizwa virusi vya ebola kubainika katika mji wa Goma, ulio kwenye mpaka na Rwanda, mashariki mwa DRC.

Hata hivyo mpaka huo ulifunguliwa jioni kwa mujibu wa taarifa kutoka Wizara ya Afya.

Awali, kulikuwa na wasiwasi kuwa mgonjwa aliyegundulika mjini Goma alikuwa amekutana na watu wengi na hivyo, kulikuwa na wasiwasi wa kusambaa kwa maambukizi hayo.

Aidha, serikali ya Rwanda imekanusha uvumi ulioanza kuenea nchini humo kwamba, kuna matukio ya watu wawili waliolazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Rubavu baada ya kugundulika kuwa na ugonjwa wa ebola.

Uganda imesema hakuna maambukizi yoyote ya ugonjwa wa ebola yaliyoripotiwa tena nchini humo, baada ya mtoto mwenye umri wa miaka mitano aliyekuwa ameambukizwa kuvuka mpaka na kuingia nchini humo kabla ya kurudishwa tena nchini Congo ndani ya mwaka mmoja wa maambukizi ya ugonjwa huu.

Maambukizi ya ugonjwa wa ebola, yanaendelea kuongezeka, Mashariki mwa DRC, mwaka mmoja, baada ya kuzuka kwa ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO) watu zaidi ya 1,800 wamepoteza maisha na wengine zaidi ya 2,000 wameshaambukizwa virusi vya ugonjwa huo, huku maambukizi mapya 15 yakitangazwa siku ya Jumatano.

Wakati huo huo timu za kupambana na ugonjwa wa ebola katika mkoa wa Kivu Kusini zimetoa chanjo kwa watu arobaini waliotengwa kwa mara ya kwanza katika mkoa huo tangu kuibuka kwa ugonjwa huo mashariki mwa DRC. **RFI**

## Polisi yawakamata waandamanaji

**MOSCOW,** Urusi

JESHI la Polisi mjini Moscow limewakamata watu 800 waliokuwa wamehudhuria maandamanao katika mji huo juzi wakidai kufanyika kwa uchaguzi huru.

Miongoni mwa waliokamatwa yumo mwanaharakati maarufu nchini humo, Lyubov Sobol ambaye ni mshirika wa karibu wa mwanasiasa wa upinzani aliyeko jela, Alexei Navalny. Kundi huru la OVD linalofuatilia hali nchini Urusi, limesema polisi waliwakamata watu 828 na kuwapiga walipokuwa wakijaribu kuwadhibiti.

Hata hivyo, taarifa kutoka Jeshi la Polisi imeeleza kuwa wamewakamata watu 600 na kwamba kiasi cha waandamanaji 1,500 walishiriki maandamano hayo iliyoyaita haramu.

Maandamano hayo yalikuwa ni madogo kulinganisha na yale yaliyofanyika wiki moja iliyopita, lakini yameonyesha nia ya wakosoaji wa Kremlin hususani vijana ambao wanazidi kuongeza shinikizo la mabadiliko ya mfumo wa siasa. **DW**

# Mtoto wa dereva wa RC asababisha ajali mbaya

**Na Beatrice Shayo**

MTOTO wa dereva wa gari la Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima, amedaiwa kusababisha uharibifu mkubwa wa gari hilo baada ya kumshinda wakati akiliendesha na kuliingiza mtaroni.

Kufuatia tukio hilo, deveva wa Mkuu wa Mkoa pamoja na mkewe walizimia na kupelekwa hospitali.

Gharama za matengenezo ya gari hilo zimekadiriwa kufikia Sh. milioni 80.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu jana kuhusu tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara, Juma Ndaki, alisema tukio hilo limetokeo jana baada ya dereva huyo kuliosha gari hilo na kwenda nalo nyumbani kwake.

Alisema alipofika nyumbani hakulizima kwa kuwa alikuwa anataka kumfuata mkuu wa mkoa.

"Huyu dereva alikuwa na safari jana na Malima walirudi usiku, sasa lile gari lilikuwa limechafuka sana ndipo alipolichukua kwa ajili ya kwenda kuliosha. Wakati analiosha alitembelewa na baba mkwe wake na kuliacha gari likiwa linaunguruma," alisema.

Alisema wakati dereva akiwa ndani ya nyumba, mtoto wake mwenye umri wa miaka 24 aliingia kwenye gari hilo na kuliendesha bila ridhaa ya baba yake.

Kamanda Ndaki alisema alipofika eneo la kanisa lilimshinda na kuingia kwenye mtaro kwa sababu alikuwa kwenye mwendokasi.

"Madhara ni makubwa kuna vitu vimekufa katika hiyo gari na kijana huyo ameumia na yeye yupo hospitali," alisema.

Alisema dereva wa gari la Mkuu wa Mkoa ambaye jina lake bado hajalipata, alizimia na kupelekwa hospitali.

"Haikuwa kusudi lake, watoto wa siku hizi ni balaa hawana nidhamu yaani anachukua gari bila kuogopa, mke wa dereva alivyosikia hiyo taarifa na yeye alizimia amepelekwa hospitali," alisema.

Alisema gari hilo lipo katika hali mbaya kwa kuwa mbele limeharibika sana na matengenezo yanakadiriwa kuwa Sh. milioni 80.




Bodaboda ikipita jirani na kibao kinachoonyesha kufungwa kwa barabara maarufu kwa jina la Kanisani kwa Pinda, Kinondoni Dar es Salaam jana, hali inayosababisha usumbufu kwa wananchi na waumini wa kanisa kupita kwa gari kutokana na kutowekewa sehemu mbadala ya kupita. **NA MPIGAPICHA WET**

# Pinda ataka mchango wa Dk. Kanabar kuenziwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, amewataka Watanzania kuenzi mchango wa daktari bingwa wa maradhi ya moyo, Rajni Kanabar kwa kujitoa kusaidia watu wenye shida kwa kuwa alifanya mema mengi kwenye sekta ya afya.

Pinda aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza jijini Dar es Salaam kwenye ibada maalum ya kumwombea Dk. Kanabar, aliyefariki mwezi Juni huko Dallas, Marekani baada ya kuugua kwa muda mrefu. Alisema Dk. Kanabar atakumbukwa zaidi kwa namna alivyosaidia watoto wenye matatizo ya moyo kwenda India kutibiwa bure na wakarejea wakiwa salama baada ya matibabu.

"Dk. Kanabar alijitolea maisha yake kwa ajili ya Watanzania, kwake pesa haikuwa kipaumbele aliweka utu kwanza na sisi Watanzania tunapaswa kuiga mfano huo kwa kusaidia wenye shida mbalimbali. Dk. Kanabar aliitendea haki nchi hii na kwa niaba ya serikali tutaendelea kushirikiana na hospitali ya Regency aliyoianzisi," alisema.

"Ingawa sote tunahuzunika, lakini wale watoto waliokuwa na matatizo ya moyo wakatibiwa kwa msaada mkubwa wa Dk. Kanabar, wangekuwa hapa wangelia sana kuliko sisi kwa sababu wamemkosa mtu muhimu sana aliyeleta nuru kwenye maisha yao," alisema.

Pius Msekwa aliyeshiriki ibada hiyo alisema alipokea kwa mshtuko kifo cha Dk. Kanabar kwa kuwa alikuwa mtu mwenye msaada mkubwa kwa watu wengi hasa waliokuwa na matatizo ya kiafya, lakini hawakuwa na uwezo wa kifedha.

"Ingawa hii ni safari yetu wote, lakini kuna wengine wakitangulia wanaacha pengo kubwa sana kama huyu mtaalamu mimi nawashauri Watanzania waige wema na utu aliokuwa nao Dk. Kanabar wa kujali wengine," alisema.

Naye mtoto wa kwanza wa Dk. Kanabar, Amish alisema familia itamkumbuka baba yao kwa namna alivyokuwa mstari wa mbele kuhakikisha watu wenye shida wanapata msaada.

Alisema baba yake alianzisha hospitali ya Regency kwa lengo la kusaidia watu wenye shida na amekuwa akitoa punguzo la gharama za matibabu na wakati mwingine kuwatibu bure watu wasio na uwezo wa kumudu gharama.

Alitoa mfano kuwa kutokana na utu aliokuwa nao baba yake, hospitali hiyo imekuwa ikitoa punguzo linalofikia Sh. milioni 14.7 kila mwezi kwa watu wanaosafishwa damu kutokana na figo zao kushindwa kufanyakazi.

Waziri wa zamani wa fedha, Basil Mramba, alisema mara kadhaa Dk. Kanabar alikuwa akimkumbusha umuhimu wa kusaidia wenye shida akisema kuwa mali za duniani hakuna mtu atakayekwenda nazo atakapofariki.

Mramba alisema Dk. Kanabar alianzisha mradi wa kupeleka wagonjwa wa moyo kwenda kutibiwa bure nchini India ambao ulisaidia kuokoa maisha ya maelfu ya Watanzania hasa watoto ambao hawakuwa na uwezo.

## Mama, mwana watoweka



**Na Mwandishi Wetu**

AMIDA Khalfani na mtoto wake Tarki Temba (pichani) wanatafutwa na ndugu zao baada ya kutoweka nyumbani kwao Kimara Rombo tangu Agosti 2, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na dada wa Amida, Suzana Shabani, wawili hao waliondoka nyumbani wakiaga kuelekea dukani kununua mahitaji, lakini hawakurudi.

"Amida ana matatizo ya akili, siku anaondoka nyumbani alikuwa na mtoto wake na waliaga wanakwenda kununua chakula, lakini hawakurudi na hii ni mara yake ya pili kupotea," alisema Suzana.

Alieleza kuwa wamewatafuta sehemu mbalimbali ikiwamo kwa ndugu, lakini hawajafanikiwa kuwapata. Alisema wameshatoa taarifa Kituo cha Polisi Kimara na kufunguliwa jalada KIM/RB/3884/2019.

Alisema kwa yeyote atakayewaona atoe taarifa kituo chochote cha polisi au apige simu **0717 283669** au **0652 226351**.

## Madiwani washtukia ufisadi kwenye madini

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

KIKAO cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita kilichofanyika mwishoni mwa wiki kimeazimia kupelekwa mara moja kwa maofisa wa halmashauri hiyo, kwenye masoko ya dhahabu wilayani humo ili kuthibiti mianya inayoweza kutoa fursa ya mapato yanayotokana na tozo ya asilimia 0.3 ya dhahabu kupotea.

Akibariki azimio hilo baada ya mjadala mkali, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita, Elisha Haraka Lupuga, alisema zoezi hilo litatekelezwa mara moja kama ilivyoazimiwa kwa kumwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Ali Kidwaka, kutekelezwa mara moja.

Kidwaka alisema utekelezaji huo utaanza mara moja ili kuepusha uwezekano wa kuipotezea mapato halmashauri hiyo, ili kuziba mianya inayoweza kutoa nafasi kuhujumiwa mapato yake.

Awali akiwasilisha hoja hiyo, Diwani Maimuna Mingisi alisema baadhi ya wanunuzi wa dhahabu wamekuwa wakiwaorodhesha kwenye madaftari wanaouza dhahabu badala ya kuwapatia stakabadhi.

Hali hiyo inaashiria kuwapo uwezakano mkubwa wa kukwepa kulipa tozo za serikali ikiwamo ya asilimia 0.3 inayolipwa kwa halmashauri ya wilaya.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA**

**YAKO KWA BEI NAFUU SANA**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**J/PCF - 54**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Mahakama ya mwanzo CHAMWINO IKULU wilaya ya CHAMWINO**

**MADAI NAMBARI 21/2019**

**MDAI…….. NATHAN MAMTI**

**Kwa………. MAGRETH CHRISTOPHER**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**

**KUJA KUJIBU MADAI YA TALAKA**


Hivyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya tarehe 09/08/2019 saa 2.30 asubuhi kwa kujibu madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ya kukatwa shauri hilo, ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama * hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa Amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 24/07/2019

215359102

## PASSPORT IMEPOTEA



**FARIJI DANIEL ELINEEMA MTANGO** anatangaza kupotelewa na Hati ya Kusafiria (Passport) iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu Dar es salaam mwaka 2005 na kuisha muda wake mwaka 2015.

**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.**

**Taarifa ya polisi,**
**Control No. 991088440183.**

115360102

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**SAIDI YASINI MAIGE** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 485 ABY BAJAJ BOXER.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**MG/RB/2497/2019.**

115360002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Baruapepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Jumatatu** tarehe **05-07-2019** kampuni ya **SUMMER COMMUNICATION CO. LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **TUNDUMA** kuelekea **MBEYA,** gari hizo zenye namba za usajili:
   **T 552 DKN / T 960 CMQ.**


2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 17 |
| Upana | - | mita | 3.5 |
| Kimo | - | mita | 4.6 |

3. Njia itakayotumika **TUNDUMA hadi MBEYA.** Gari litasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**Philipo Kamaka Kimpa** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye namba **TAE 118539** iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi mwaka 2019.

**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa ya polisi STK/RB/7884/2019.**

115360202

## TANGAZO LA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**Musaji lunyilija Makonge** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya sanlg Yenye namba za usajili **T 939CBL.**

Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi
**GEI/MBO/RB/160781/2019.**

115359902


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA**

**YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**au piga simu: 0767 223311**

**Kwa Habari Motomoto**

**usikose Gazeti lako la**

**Nipashe kila siku**

**NJOO UTANGAZE**

**BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# SOLSKJAER HANA SHAKA POGBA KUBAKI UTD




**CARDIFF,** Wales

OLE Gunnar Solskjaer amesema "hana shaka" kwamba Paul Pogba atabakia kuwa mchezaji wa Manchester United mwishoni mwa kipindi hiki cha usajili wa majira ya joto.

Kiungo huyo hakusafiri kwenda Cardiff katika mchezo wa kirafiki dhidi ya AC Milan ambapo Man United walishinda kwa penalti 5-4 na kuacha uvumi kwamba anaweza kuondoka kwenda Real Madrid.

Vyanzo viliiambia ESPN FC mapema Jumamosi kwamba Pogba alikuwa akijiandaa kujiunga na kikosi cha kocha, Zinedine Zidane.

Lakini Solskjaer alisisitiza uamuzi wake wa kumwondoa Pogba kwenye kikosi hicho baada ya Mfaransa huyo kulalamika maumivu ya mgongo na akaachwa ili awe fiti kwa mchezo wa ufunguzi wa Ligi Kuu dhidi ya Chelsea wikendi ijayo.

"Hakuna shaka kabisa," alisema Solskjaer wakati alipoulizwa kama Pogba bado ataendelea kuwa mchezaji wa United baada ya kufungwa kwa dirisha la usajili.

"Sikutarajia kusafiri naye kwenda Cardiff. Nilizungumza naye baada ya mazoezi na alikuwa hajisikii vizuri na hivyo tulimwacha ili ajiandae kuwa fiti kwa ajili ya wiki ijayo.

"Sio majeruhi, ni maumivu tu. Hajaumia, lakini sikutaka kuhatarisha afya yake. Atakuwa tayari kwa ajili ya kuivaa Chelsea."

# Klopp ashangaa tarehe ya kuanza EPL

**LONDON,** England

JURGEN Klopp amehoji kuhusu tarehe ya kuanza kwa Ligi Kuu ya England na namna inavyoweza kuwa na athari kwa wachezaji.

Liverpool ilifungua msimu mpya jana Jumapili kwa kucheza na Manchester City katika mchezo wa Ngao ya Jamii na kikosi hicho cha Klopp kina nafasi ya kushinda mataji kadhaa msimu huu, wakati kitakaposhiriki kwenye mashindano saba tofauti.

Baada ya mchezo wa Ngao ya Jamii, Liverpool ilianza kampeni ya Ligi Kuu kwa kuivaa Norwich Ijumaa wiki hii kabla ya kucheza na Chelsea kwenye Kombe la UEFA Super siku tano baadaye, yaani Agosti 14.

Ligi Kuu ya England pamoja na ile ya Ufaransa, Ligue 1, zote zitaanza wikendi inayokuja, huku ile ya Ujerumani, Bundesliga, ikianza Agosti 16, ya Hispania, La Liga, itaanza Agosti 17 na ile ya nchini Italia, Serie A, wiki moja baadaye.

"Sijui kwa nini wanaanza mapema namna hii," alisema Klopp, ambaye kikosi chake kinaweza kushinda moja ya mataji hayo msimu huu, Ngao ya Jamii, UEFA Super Cup, Klabu Bingwa Dunia, Ligi ya Mabingwa Ulaya, Ligi Kuu, FA Cup na Carabao.

Kipindi hiki cha majira ya joto wachezaji wa Liverpool wameshindana kwenye mashindano mbalimbali ya kimataifa, kwani Sadio Mane alikuwa na kikosi cha Senegal kilichomaliza nafasi ya pili katika michuano ya mataifa ya Afrika, Afcon, Julai 19 na Alisson alishinda Kombe la Copa America akiwa na Brazil Julai 7.

"Nimezungumza na (kocha wa Napoli) Carlo Ancelotti," aliongeza Klopp. "Italia ina timu 20 kama ilivyo kwenye Ligi Kuu ya England na wanaanza msimu Agosti 24.

"Kalidou Koulibaly alicheza na Sadio kwenye mataifa ya Afrika. Ana likizo ya wiki nne za kupumzika na hata hatarajiwi kurudi uwanjani.





# *Kocha Everton majembe zaidi*

**LONDON,** England

KOCHA Marco Silva ameishauri bodi ya Klabu ya Everton kuingia sokoni haraka wakati wakielekea mwishoni mwa kufungwa kwa dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto, baada ya kumpoteza mchezaji mwingine muhimu.

Fabian Delph aliyetua kwa pauni milioni 10 akitokea Manchester City mwezi uliopita, ataukosa mwanzo wa msimu wa Ligi Kuu baada ya kuumia nyonga kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Werder Bremen, juzi Jumamosi.

Delph alitolewa uwanjani dakika ya nne, baada ya kuumia na vipimo vinaonyesha kwamba atakuwa nje kwa wiki kadhaa. Na hivyo uwezekano wa kuanza kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu dhidi ya Crystal Palace Jumamosi ijayo ni mgumu.

Kocha huyo raia wa Ureno amesema: "Bado hatuna uhakika kuhusu hali yake maana hatujapata ripoti ya madaktari. Ngoja tuangalie kwa siku chache sijazo. Nafikiri Jumatatu (leo) tunaweza kupata majibu sahihi."

Kipindi hiki cha usajili wa majira ya joto kimeonekana kuwa kigumu kwa Everton kwani hadi sasa wamekamilisha usajili wa kiungo Jean-Philippe Gbamin kutoka Mainz waliyemsajili kwa pauni milioni 25 na Moise Kean anaonekana yupo kwenye hatua nzuri ya kutua hapo.

Kean mshambuliaji kinda wa miaka 19 wa Juventus, alifanyiwa vipimo vya afya Jumamosi na anatarajia kukamilisha usajili wa pauni milioni 30.

"Siwezi kumzungumzia yeye kwa sasa, hakuna kitu ambacho kipo rasmi kwa sasa," alisema kocha huyo wa pale dimba la Goodison akizungumzia usajili wa Kean.

# Lampard: Mount ataanza dhidi ya Man United

**LONDON,** England

FRANK Lampard amesema Chelsea itatakiwa kujiimarisha zaidi katika mchezo wao wa ufunguzi wa Ligi Kuu ya England pale Old Trafford dhidi ya Manchester United, baada ya kutoka sare na Borussia Monchengladbach, lakini akamsifia Mason Mount.

Chelsea walionekana kuwa kwenye wakati mgumu katika safu ya kiungo kipindi cha kwanza na wakawa nyuma kwa mabao 2-0, hadi walipopata penalti kuweza kusawazisha kupitia Tammy Abraham na Ross Barkley na kuambulia sare hiyo ya 2-2 dhidi ya Wajerumani hao kwenye mchezo wa kirafiki.

Lilikuwa shuti la Mount ndilo lililobadili mwelekeo baada ya kumgonga Keanan Bennetts na kusababisha penalti dakika ya 85 na Barkley akafunga.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, ambaye alicheza chini ya Lampard kwa mkopo kule Derby msimu uliopita, sasa anaonekana amemshawishi kocha wake na amewekwa kwenye nafasi ya kuanza dhidi ya Manchester United.

"Amefanya mengi," alisema Lampard. "Kwa uhakika nina furaha kubwa kwa namna anavyofanya kwenye mazoezi, na namna jinsi anavyocheza kwa kujituma.

"Wachezaji wanaelewa ubora wake na nina uhakika Mason atakuwa na wakati mzuri zaidi msimu huu."




# BARCA YATAKA KUMPELEKA COUTINHO EPL KWA MKOPO




**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imeripotiwa kwamba imetoa ofa kwa klabu za Ligi Kuu ya England kumsajili Philippe Coutinho kwa mkopo wa pauni milioni 27.

Miamba hao wa Catalunya walimsajili kiungo huyo mwenye umri wa miaka 27 kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 142 kutoka Liverpool Januari mwaka 2018 na sasa wanataka pauni milioni 110 ili wamuuze moja kwa moja.

Liverpool, Arsenal, Manchester United na Paris Saint-Germain zote zimekuwa zikihusishwa na mpango wa kumsajili Coutinho kipindi hiki cha majira ya joto.

Kwa mujibu wa Mundo Deportivo, kupitia redio Catalunya, mabingwa hao wa La Liga wanataka pauni milioni 27 kumwachia kwa mkopo wa msimu mmoja.

Maofisa wa Barcelona wana matumaini kwamba wataweza kuzishawishi klabu kumsajili Coutinho ili waweze kuhimili mshahara wake.

Ujio wa Antoine Griezmann kutoka Atletico Madrid kwa pauni milioni 108 pamoja na Barcelona kuendelea kumshawishi Neymar kurudi hapo, nafasi ya Coutinho inaonekana itakuwa finyu.

Barcelona pia imemsajili kiungo mwingine, Frenkie de Jong kutoka Ajax kwa ada ya pauni milioni 67.5.

Coutinho amejikuta kwenye wakati mgumu kuweza kuwashawishi mashabiki wa hapo dimba la Nou Camp tangu alipotua akitokea Anfield.

# *Fernandes aikataa United, aiita Spurs*

**LISBON,** Ureno

BRUNO Fernandes anataka Klabu ya Sporting Lisbon kumruhusu kujiunga na Tottenham wiki hii.

Kiungo huyo wa kimataifa wa Ureno alifanya mazungumzo na Rais wa Sporting Lisbon, Federico Varandas Ijumaa kwa ajili ya kumwarifu mpango wake wa kutaka kuondoka.

Sporting imetoa thamani ya mchezaji huyo kuwa ni pauni milioni 64, huku klabu kadhaa za Ligi Kuu ya England zikimwania ikiwamo Manchester United ambayo licha ya kuamini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 thamani yake ni pauni milioni 35, hataki kujiunga nayo.

Tottenham tayari imetoa ofa kwa ajili ya kumsajili mchezaji huyo, lakini inaamini kwamba, haijafikia ile wanayoitaka Sporting.

Fernandes alifunga mabao 31 msimu uliopita na kocha Mauricio Pochettino anaamini kwamba anaweza kuwasaidia Dele Alli na Son Heung-Min ambao kazi yao ni kumsukumia mashambulizi mshambuliaji, Harry Kane.



# DON SOKA MAGA ULAYA




# MESSI RASMI JELA KIMATAIFA MIEZI 3

## Pia apigwa faini ya dola 50,000, sasa kuzikosa mechi dhidi ya Chile, Mexico na Ujerumani huku...

**BUENOS AIRES,** Argentina

NAHODHA wa timu ya Taifa ya Argentina, Lionel Messi amefungiwa kwa muda wa miezi mitatu kucheza soka la kimataifa baada ya kudai kwamba michuano ya Mataifa ya Amerika Kusini, Copa America, ilijaa rushwa.

Mshambuliaji huyo wa Barcelona mwenye umri wa miaka 32, alitolewa nje kwa kadi nyekundu wakati Argentina ikishinda mabao 2-1 dhidi ya Chile na kutwaa nafasi ya tatu na alidai "Brazil iliandaliwa kuwa bingwa wa michuano hiyo."

Pia amepigwa faini ya dola 50,000 na Shirikisho la Soka la barani Amerika Kusini, Conmebol.

Shirikisho hilo baada ya kutoa adhabu hiyo, limempa siku saba Messi kukata rufani kama hajaridhika na maamuzi hayo.

**Kufungiwa huko kwa Messi kuna maanisha kwamba, atazikosa mechi za kirafiki za Argentina zinazokuja dhidi ya Chile, Mexico na Ujerumani Septemba na Oktoba mwaka huu.**

Argentina itaanza kampeni ya kufuzu kucheza michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2022 nchini Qatar, Machi 2020.

Baada ya Argentina kufungwa mabao 2-0 na Brazil katika hatua ya nusu fainali ya Copa America, Chama cha Soka cha Argentina kililalamika juu ya "makosa mabaya na makubwa ya waamuzi."

Katika kujibu malalamiko hayo, Conmebol ilisema shutuma za kuhoji maadili ya Copa America "hazina msingi" na "zinaonyesha ukosefu wa heshima." Messi alionyeshwa kadi nyekundu katika dakika ya 37 kwenye mchezo huo dhidi ya Chile, baada ya kukwaruzana na Gary Medel, ambaye naye alitolewa nje kwa kadi nyekundu.

"Hatuwezi kuwa sehemu ya rushwa hii," alisema Messi. "Hawakutuonyesha heshima kwa kipindi chote cha michuano hii.

"La kusikitisha, rushwa na waamuzi hawataki kuwaruhusu watu wafurahie soka, wanauharibu mchezo huu."

## ZISIKUPITE

### COUTINHO ANUKIA ARSENAL

ARSENAL inajiandaa kufanya mazungumzo na Barcelona ya kumsajili kwa mkopo nyota wa kimataifa wa Brazil, Philippe Coutinho, 27, dili ambalo limeripotiwa litaigharimu pauni milioni 27. ***(Sun on Sunday)***

### UNITED YAMTAKA NERES

MANCHESTER United imetoa ofa ya pauni milioni 46 kwa mshambuliaji wa Ajax, Mbrazil David Neres, 22. ***(Yahoo - in Portuguese)***

### SANE AKARIBIA KUTUA BAYERN

BAYERN Munich inakaribia kukamilisha dili la kuipata saini ya winga wa Manchester City, Mjerumani Leroy Sane baada ya kukubaliana mkataba binafsi na nyota huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(Sky Sport Germany - in German)***

### GUARDIOLA AJIPANGA KWA ISCO

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola anatarajia kushtukiza mwishoni kwenda kumsajili kiungo wa Real Madrid, Mhispania Isco, 27, na beki wa kati wa Bournemouth, Mholanzi Nathan Ake, 24. ***(Sunday Express)***

### AHOFU KUPANDISHWA BEI

NYOTA wa kimataifa wa Ufaransa, Paul Pogba, 26, anahofu dau lake linaweza kuongezwa ili kumzuia kutua Real Madrid wakati miamba hiyo ya Hispania ikikabiliwa na kutakiwa kutoa pauni milioni 270 ili kuipata saini ya kiungo huyo wa Manchester United. ***(Sunday Mirror)***

### FERNANDES AITAKA SPURS

KIUNGO Mreno Bruno Fernandes, 24, ambaye amekuwa akihusishwa na Manchester United, ameiambia Sporting Lisbon kuwa anataka kujiunga na Tottenham. ***(Mail on Sunday)***

### MADRID, VAN DE BEEK SAFI

REAL Madrid imefikia makubaliano na kiungo Mholanzi Donny van de Beek, 22, lakini bado haijakubaliana ada na klabu yake ya Ajax. ***(Marca)***

### DYBALA, MANDZUKIC WOTE UTD

MANCHESTER United imefanya mazungumzo na Juventus kuhusu mpango wa kubadilishana wachezaji ambao utamhusisha mshambuliaji Muargentina Paulo Dybala, 25, na straika Mcroatia Mario Mandzukic kutua Old Trafford, wakati Mbelgiji Romelu Lukaku, 26, akielekea upande wa pili. ***(Sunday Times)***

### HODGSON AMUONA CAHILL

KOCHA wa Crystal Palace, Roy Hodgson anataka kumsajili beki wa zamani wa England, Gary Cahill, 33, kwa mkataba wa miaka miwili. ***(Sun on Sunday)***

### NEYMAR BADO AWINDWA

BARCELONA inajiandaa kufanya mazungumzo na Paris St-Germain ya kumrejesha tena La Liga mshambuliaji Mbrazil Neymar, 27. ***(Goal.com)***

### KUSHTUKIZA KWA AJER

KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers anapanga kushtukiza kwenda kumsajili beki wa kimataifa wa Celtic na Norway, Kristoffer Ajer, 21, kwa pauni milioni 15. ***(Star Sunday)***

HABARI MICHEZO

## Azam yalia na washambuliaji

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la Klabu ya Azam FC, limeweka wazi kuwa bado safu yao ya ushambulijaji ina mapungufu makubwa na kwamba wanaendelea kuifanyia marekebisho kabla ya kuanza michuano ya kimataifa na Ligi Kuu Bara.

Azam na KMC zinaiwakilisha Tanzania Bara kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho wakati Simba na Yanga zikipeperusha bendera ya Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha msaidizi wa Azam, Iddi Cheche, alisema, safu yao ya ushambuliaji bado ni tatizo lakini wanaendelea kuifanyia kazi.

"Safu yetu ya ushambuliaji hususan upande wa umaliziaji, nimebaini mapungufu makubwa ambayo inabidi 'kudili' nayo sana," alisema Cheche huku akisifu mechi za kujiandaa na msimu mpya ambazo wamecheza kuwasaidia kuendelea kujipanga.

"Michezo yote ya kirafiki tuliyoicheza imewasaidia vijana wetu kujiandaa na mashindano ya Kombe la Shirikisho pamoja na msimu ujao wa Ligi Kuu," alisema kocha huyo.

Aidha, alisema licha ya timu kuendelea kubaki kambini, hawatakuwa na mchezo mwingine wa kirafiki kwa kuwa siku zimebaki chache za wao kusafiri kuelekea Ethiopia tayari kwa mechi ya Jumapili dhidi ya Fasil Katema kwenye Kombe la Shirikisho.

## Z'bar kugeukia elimu makocha

**Na Hawa Abdallah**, ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Chama cha Soka Mkoa wa Kusini Unguja, Abubakar Khatib Kisandu, amesema ipo haja ya kutilia mkazo mafunzo ya makocha kwa klabu katika ngazi mbalimbali ili kuhakikisha soka linapiga hatua.

Aliyasema hayo katika hafla ya kufunga mafunzo ya makocha waliopo katika mkoa huo wa Kusini Unguja ambapo alisema kuna umuhimu mkubwa kwa makocha kupewa mafunzo kwani wao ndio silaha kubwa ya kukuza mchezo wa soka na hata kuzalisha wachezaji wenye uwezo mkubwa.

Alisema makocha wanakazi kubwa ya kulea vijana tangu wakiwa katika madaraja ya umri mdogo, hivyo kupatikana mafunzo mara kwa mara hususan katika mwanzo wa msimu wa ligi kutasaidia kuboresha ufanisi katika ufundishaji wao.

Aidha, aliwataka makocha wa mkoa huo kutochoka kuhudhuria mafunzo ya makocha yanayoandaliwa kwa ngazi ya Taifa na hata kimataifa ili waweze kupiga hatua na hatimaye kuajiriwa katika klabu kubwa nje na ndani ya Zanzibar.

Naye mkufunzi wa mafunzo hayo ya makocha ambaye ni kocha mwenye Leseni A kutoka Shirikisho la Soka Afrika (Caf), Salum Ali Haji alisema nchi nyingi zinazofanikiwa zaidi katika soka zimewekeza vizuri katika kulea vipaji pamoja na kuwa na makocha wao hasa kwa wale wanaofundisha timu za vijana.

# SIMBA YAAHIDI MAAJABU YA MWAKA TAIFA KESHO

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI kesho wakitarajia kutambulisha rasmi wachezaji waliowasajili msimu huu pamoja na wale wa zamani, katika Tamasha la Simba Day litakalofanyika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, uongozi wa Klabu ya Simba umewataka wanachama na mashabiki wao kuhudhuria kwa wingi kushuhudia mambo ambayo hawajawahi kuyaona.

Kesho katika tamasha hilo, Simba itacheza na Power Dynamos ya Zambia ikiwa ni sehemu ya kuwawezesha mashabiki wao kushuhudia nyota wao wapya na sehemu ya kujiandaa na msimu mpya hususan mechi ya Ligi ya Mabingwa mwishoni mwa wiki dhidi ya UD Songo ya Msumbiji.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori, alisema kwa usajili walioufanya wana uhakika wa kufika mbali katika michuano hiyo pamoja na kutetea ubingwa wao wa Ligi Kuu Bara.

**"Msimu ujao tutafanya mapinduzi makubwa kutokana na aina ya usajili tulioufanya, hatujasajili kwa kukurupuka tumeangalia wale wa kutuletea mafanikio Simba," alisema Magori.**

Aliongeza kuwa wamefanya maandalizi ya kutosha kuelekea msimu huo pamoja na mashindano ya Ligi ya Mabingwa.

"Tumefanya maandalizi ya kutosha ikiwa ni pamoja na kuweka kambi nzuri ambayo naamini kabisa itawasaidia wachezaji wetu kufanya vizuri msimu ujao," alisema.

Aidha, aliwataka mashabiki kujitokeza kwa wingi kesho kushuhudia wachezaji wapya katika kilele cha wiki yao, huku akisisitiza wanunue tiketi mapema ili kuepusha usumbufu wa kuingia uwanjani na kudai kesho watafanya mambo ambayo hayajawahi kufanywa hapa nchini.



Mashabiki wa Yanga waliofurika Uwanja wa Taifa wakishangilia wakati wa kutambulishwa wachezaji wao wa msimu huu katika kilele cha Tamasha la Siku ya Mwananchi jana. **PICHA: GETRUDE MPENZA**

# *Samatta aanza kutupia KRC Genk*




**Na Mwandishi Wetu**

STRAIKA wa kimataifa wa Tanzania na nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta, ameanza kazi yake ya kucheka na nyavu baada ya juzi kutupia bao lake la kwanza la msimu, lakini bahati mbaya timu yake ya KRC Genk ikajikuta ikichapwa mabao 3-1 na wenyeji, KV Mechelen katika mchezo wa pili wa Ligi Daraja la Kwanza A Ubelgiji.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa AFAS- Achter de Kazerne mjini Mechelen, Malines, Samatta alifunga bao hilo dakika ya 45 na akimalizia pasi ya kiungo Mbelgiji Bryan Heynen.

Bao hilo lilikuwa la kusawazisha baada ya KV Mechelen kutangulia kuziona nyavu kupitia kwa Muivory Coast, William Togui dakika ya 18, kabla ya washambuliaji wenzake, Msweden Gustav Engvall kufunga la pili dakika ya 77 na Mbrazil, Igor Alberto de Camargo kutupia la tatu dakika ya 80.

Kwa ushindi huo Mechelen ni kama imelipa kisasi kufuatia kuchapwa mabao 3-0 kwenye mchezo wa Super Cup Julai 20, mwaka huu kwenye Uwanja wa Luminus Arena mjini Genk.

Katika mechi yake ya kufungua msimu, Genk ilianza vema kwa ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Kortrijk kwenye Uwanja wa Luminus Arena.

Samatta, 26, kwa bao lake hilo linamfanya sasa kufikisha jumla ya mabao 63 hapo Genk katika mechi 158 za mashindano yote tangu alipojiunga nayo Januari mwaka 2016 akitokea TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

# Michezo



Jumatatu Agosti 5, 2019
Nipashe

Messi rasmi jela kimataifa miezi 3 UKURASA 30

UMETAPIKA...



Wachezaji wa Yanga wakiingia uwanjani jana. **PICHA: GETRUDE MPENZA**

# Yanga haijawahi kutokea U/Taifa

## ●●● Yaandika rekodi mpya, uwanja watapika, yaonyesha makubwa huku...

**Shufaa Lyimo, Adam Fungamwango**

ACHANA na matokeo ya sare ya bao 1-1 Yanga iliyopata katika mechi ya kilele cha Siku ya Mwananchi Uwanja wa Taifa dhidi ya Kariobangi Sharks ya Kenya, kwani tamasha hilo liliandika historia mpya kwa klabu hiyo kutokana na namna lilivyofana ikiwa ni pamoja na uwanja kutapika.

**Wanachama na mashabiki wa Yanga walijitokeza kwa wingi kushuhudia wachezaji wao wa msimu mpya wakitambulishwa rasmi pamoja na mchezo huo ambao kwa ujumla timu hiyo ya mtaa wa Twiga na Jangwani ilionyesha kandanda la kuvuti.**

**MSOLLA AWEKA REKODI**

Mwenyekiti wa Yanga, Mshindo Msolla, jana aliweka rekodi katika mechi ya awali kati ya Yanga Veterani dhidi ya Pamba Veterani kutoka mkoani Mwanza ambapo alikuwa nahodha.

Msolla ambaye aliichezea Yanga Veterani, alicheza kwa muda mfupi na kuomba kutolewa na kabla ya kuruhusiwa kutoka aliamua kujitokeza nje mwenyewe na kumkabidhi unahodha Ally Yusuph (Tigana) kabla kipindi cha kwanza hakijaisha.

**BONGO MUVI VS BONGO FLEVA**

Katika mchezo kati ya Bongo Muvi na Bongo Fleva ndio uliofungua tamasha hilo la kilele cha Wiki ya Mwananchi na hadi kipindi cha kwanza kinamalizika hakukuwa na mbabe.

Bongo Fleva, ambayo ilijizolea mashabiki wengi katika mechi hiyo, hadi mechi inamalizika ilishinda kwa bao 1-0.

**YANGA 1- 1 KARIOBANGI**

Kwenye mechi ambayo wanachama na mashabiki wa Yanga walijitokeza kwa wingi, ilijawa na kosakosa nyingi za mabao mengi kipindi cha kwanza ambayo kama ingetumia vema nafasi ingeibuka na ushindi mnono.

Dakika ya nane tu, straika mpya aliyesajiliwa kutoka Polisi ya Uganda alikosa bao, baada ya kupiga kichwa mpira wa kona na kutoka nje ya goli.

Dakika ya 31, Balinya alikosa tena bao la wazi alipopiga shuti akiwa karibu na lango la Kariobangi, lakini mpira uligonga mwamba na kurejea uwanjani.

Straika mwingine mpya wa Yanga Mnamibia Sadney Ukhrob naye alikosa mabao mawili kipindi cha kwanza, dakika ya 12 aliachia kombora lililookolewa na kipa wa Kariobangi na kuwa kona butu, lakini dakika ya 37 alikosa bao lililokuwa la wazi zaidi, alipobaki na kipa, lakini akampa mikononi.

Shambulio pekee hatari kipindi cha kwanza kufanywa na Kariobangi lilikuwa ni dakika ya 27 baada ya Patrick Otieno kubaki ana kwa ana na kipa mpya wa Yanga, Farouk Shikalo, lakini akachelewa kupiga na kipa akauwahi.

Otieno alirekebisha makosa yake kipindi cha pili, alipoiandikia timu yake bao la kwanza dakika ya 48, baada ya kuachia shuti kali akiwa nje kidogo ya eneo la hatari, kabla ya Yanga kusawazisha kwa mkwaju wa penalti iliyopigwa na kiungo wao mpya Patrick Sibomana dakika ya 57, baada ya beki mmoja wa Kariobangi kuunawa kwenye eneo la hatari.

# Kaseja aivusha Stars CHAN

**Na Mwandishi Wetu**

KIPA Juma Kaseja ameipeleka timu Taifa ya Tanzania 'Taifa Stars' hatua inayofuata ya kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) baada ya kuokoa penalti moja, huku straika Salum Aiyee akipigilia msumari wa mwisho kwa kutupia tuta la nne wakati wakiitupa nje Harambee Stars kwa matuta 4-1 ugenini nchini Kenya jana.



Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Kasarani jijini Nairobi, timu hizo zilimaliza dakika 90 zikitoka suluhu, hivyo kulazimika kuingia katika changamoto ya mikwaju ya penalti kufuatia matokeo kama hayo Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam wiki moja iliyopita.

Kwa matokeo hayo, Taifa Stars sasa itakutana na Sudan na ikipata matokeo ya jumla nyumbani na ugenini itafuzu moja kwa moja fainali kwa mara ya pili, ambazo zitafanyika mwakani nchini Cameroon.

Kikosi cha Stars kinachonolewa na Mrundi Etienne Ndayiragije, kimefanikiwa kusonga mbele kupitia penalti za Erasto Nyoni, Paul Godfrey, Gadiel Michael na Aiyee.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042